

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 17 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu, nimuite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya maswali. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kumuuliza maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tutaanza na Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Serikali ya Tanzania imepitia Awamu Sita za uongozi; Awamu ya Kwanza ilijikita kwenye kujenga viwanda kwa ajili ya kuboresha ajira na uzalishaji, Awamu ya Tatu iliamua kubinafsisha viwanda hivi ili kuviboresha zaidi pamoja na kuongeza ajira, Awamu ya Tano ilikuja tena na Sera ya Ujenzi wa Viwanda ili kuongeza ajira pamoja na uzalishaji.

Swali langu; viwanda vilivyobinafsishwa kwenye Awamu ya Tatu vingi havifanyi kazi iliyokusudiwa, kwa mfano viwanda vya korosho Mkoa wa Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma. Nini msimamo wa Serikali wa Awamu ya Sita kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifayi kazi iliyokusudiwa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania majibu kwa swali hilo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba uchumi wa nchi yetu hutegemea nyanja nyngi ikiwemo na ujenzi wa viwanda ambavyo vina faida pana kwa Watanzania na mifano yote ulioieleza kutoka Awamu ya Kwanza mpaka ya Tatu. Awamu ya Tatu ya Serikali yetu illengen kutoa fursa kwa Sekta Binafsi kuhakikisha kwamba nazo zinaingia kwenye mchakato wa uchumi kwa kushika viwanda na kuviendeleza. Lakini nasikitika kwamba baadhi ya waliopewa viwanda hivyo hawakufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini Serikali imefanya ni kuchukua viwanda vyote ambavyo havikufanya vizuri na tuliunda Tume iliyoongozwa na Msajili wa Hazina pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya mapitio viwanda vyote vile ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi ikiwemo na viwanda vya korosho. Na kwa bahati nzuri mimi ni mdau wa korosho na natambua viwanda vyetu kule vingi hata

vilivyopo Mkoani Pwani na Tanga wameshindwa kuviedesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tulichofanya, tumechukua viwanda vyote na sasa vinafanyiwa uchambuzi na Serikali na timu iliyoongozwa na Msajili wa Hazina baadaye tupeleke kwenye Baraza la Mawaziri. Malengo yetu ni kutoa viwanda hivyo kwa watu ambao wana uwezo sasa kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anasisitiza pia kwamba Sekta Binafsi lazima iwe karibu na Serikali ili kuweza kupanua wigo wa uchumi kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baadaye tukipata wale ambao wana nia ya kuendesha tutawapa kwa masharti ambayo tutayaweka ili kuendeleza ule mkakati wetu wa uchumi wa viwanda hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie tu mheshimiwa Mbunge kwamba viwanda hivi ambavyo havifanyi kazi tayari vimesharatibiwa na vitatolewa kwa watu ambao wenyе uwezo. Kwa hiyo, niwakaribishe Watazania wenyе nia ya kuwekeza kwenye viwanda kuwa tayari kupokea baada ya Baraza la Mawaziri kufanya maamuzi ili waweze kuviedesha viwanda hivyo kwa ufanisi mukubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi iliyelekeza Serikali kuhakikisha kwamba usambazaji umeme vijijini unakamilika kufika mwaka 1922. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni kuititia Bunge hili Waziri mwenye dhamana ya nishati amekuwa akitueleza kwamba jukumu hili litakwenda kukamilika 2022 lakini pia ametupa

mpaka namba za wakandarasi ili tufuatilie mwendelezo wa usambazaji umeme vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo masikitiko makubwa kwamba pamoja na agizo hilo, lakini sio vijiji vyote ambavyo vimeingizwa katika mpango huu; hivi tunavyozungumza wakandarasi wapo *site* lakini wanaruka baadhi ya vijiji kwa maana kwamba hawajapewa *scope*. Na zaidi ya hilo, badala ya nguzo 40 ambazo ziliikuwa zinatolewa kwenye kila Kijiji sasa wanatoa nguzo 20. Sasa nilitaka kufahamu ni ipi kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2022 nchi nzima itakuwa inawaka umeme? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imeazimia kupeleka umeme kwenye vijiji vyote na bado tumeweza dhamira ya kupeleka umeme mpaka vitongojini ikiwemo na maeneo ya visiwani. Utaratibu ambao tumeuweka ndani ya Serikali kwa zoezi hilo la kusambaza umeme, tunaenda kwa awamu na sasa tupo kwenye awamu ya tatu na hii awamu ya tatu tumeigawa kwenye awamu mbili; awamu ya tatu moja na awamu ya tatu mbili. Awamu ya tatu mbili imeanza siku za karibuni na wakandarasi tumeshawasambaza kwenye halmashauri zote ili kukamilisha vijiji vyote vilivyobaki vipate umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye awamu ya tatu hii mbili tumeongeza mkakati ambao nimeueleza awali wa kupeleka umeme kwenye vitongoji na kwenye visiwa kama vile kule Ukerewe, Mafia na maeneo mengine ya visiwa. Mkakati huu tayari umeshatangazwa, zabuni zimetolewa, wakandarasi wamepatikana, ujenzi wa umeme utaanza kazi mara moja. Lengo letu ni kupeleka umeme kila Kijiji na kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote ikiwemo na visiwani

ambapo tunaweza tukapeleka umeme juu ili nao wapate pia umeme kwa ajili ya matumizi ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, dhamira ya Serikali bado imebaki palepale na nakumbuka mwezi wa pili nilikuwa Mlalo kwa Mheshimiwa Shangazi kwa hiyo inawezekana ameuliza swali hili kama alivyokuwa amechangia siku ile kwenye mkutano wa hadhara na nikamhakikishia kwamba Serikali itapeleka umeme kwenye Jimbo la Mlalo lote, vijiji mpaka vitongojini. hivyo ni pamoja na nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme vijiji uko imara na sasa hivi tume-cover sehemu kubwa sana; tumebakni na vijiji vichache sana ili tuweze kuvimaliza vijiji vyote, kazi inaendelea na kwa kweli kazi inaendelea. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, swali la kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. JUSTINE L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za dini zimekuwa zikikumbwa na adha kubwa, vikwazo vingi na urasimu wakati wa kushughulikia misamaha ya kodi wanapopata vifaa au misaada mbalimbali kutoka nje ya nchi na kusababisha wakati mwagine vifaa hivyo kukaa muda mrefu bandarini na kuingia tena tatizo la *storage charges* ambazo mwisho wake wanashindwa kuvitoa.

Ni nini kauli ya Serikali kuhusu tatizo hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kutoa misamaha kwa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma za jamii, zinazolenga kuisaidia Serikali katika utoaji wa huduma hizo. Na misamaha hii ambayo inatolewa inaratibiwa na taasisi zetu zote kama inatoka nje ya nchi inakuja nchini kuanzia mahali pa forodha kama ni bandarini, *airport* na maeneo mengine taratibu zimeandalishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la urasimu ambalo Mheshimiwa Mbunge amelieleza linatokana pia na wale wenye hizo bidhaa/mali inayoingizwa nchini kwa au kutofuata utaratibu na kuratibu jambo zima bila kufuata utaratibu wake hilo pia nalo linaweza kusababisha kuwa na urasimu wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, bidhaa hizi zinaposafirishwa kutoka nje ya nchi kuingia ndani ili ziweze kupata msamaha, hawa wenye bidhaa hiyo taasisi ya kidini au taasisi yoyote ambayo inapata msamaha ni lazima iwe imeandaa utaratibu wa kupeleka maombi lakini pia kupeleka idadi ya orodha ya mali zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu ambao tumeupata Serikalini ni kwamba watu wanaweza kuomba msamaha lakini anachokileta nchini sio kile alichokiombea msamaha. Kwa hiyo, kunakuwa na hatua ndefu ambazo wengine wamesema kwamba hii ni urasimu wa Serikali, hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito sasa kwa taasisi ambazo zinapata misamaha, kwanza kueleza kikamilifu wanataka kuleta nini ambacho kinatakiwa kipate msamaha lakini bidhaa hiyo inayoletwa kwa misamaha lazima ikidhi matakwa ya Serikali kwamba lazima iende ikatoe huduma ambayo inakusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuondoa urasimu ni lazima taratibu hizi zifuatwe mapema ili mzigo unapofika kwenye vituo basi uweze kutoka mara moja. Kwa hiyo, tunaendelea kusimamia taratibu hizi huwa zinakamilka na kwa wito nilioutoa kwa wateja wetu kuhakikisha wanafuata taratibu kwa mapema zaidi ili mzigo unapofika uweze kutoka mara moja. Tumejipanga vizuri na tumetoa maelekezo bandarini, viwanja vyaa ndege na kwenye mipaka yetu kote nchini ili wateja wetu wapate huduma za haraka sana ikiwemo na wanaopata msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa majibu hayo kwa Mheshimiwa Nyamoga. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za Wilaya zilizokuwa na ofisi maeneo ya mjini zilizo nyingi zilitakteleza maagizo ambayo yalitolewa na Serikali ofisi zao ziweze kuondoka pale mjini ili zipelekwe katika halmashauri zao. Na kitendo hiki kilifanya halmashauri nyingi na wananchi wengi kukosa huduma bora ambazo walizoea. Lengo la kuzachaa pale mjini ilikuwa wananchi waweze kupata huduma na utawala bora kama ilivyokuwa lengo kubwa lakini kwenda kule kumeongeza kwanza umbali kwa sababu lazima wafike mjini ndio waende kule lakini pia gharama inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua kule vijijini usafiri ni wa mabasi, mabasi yanatoka asubuhi alfajiri yanafika na yanarudi mchana kwa hiyo akikosa huduma kwa wakati anashindwa kurudi kwa hiyo inamlazimu kulala. Je, nini kauli ya Serikali ya kuwapunguzia wananchi adha hii na kuhakikisha kwamba wanapata huduma kwa gharama nafuu na kwa utawala bora uweze kutekelezeka. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la mheshimiwa Tendega, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni agizo la Serikali la Halmashauri hasa za Wilaya ambazo zilikuwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya zake ambapo pia waliacha wahudumiwa wako mbali na maeneo ya kutolea huduma. Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wa Awamu ya Tano alitoa maelekezo kwamba Halmashauri za Wilaya ziondoke kwenye Halmashauri za Miji walimo badala yake wajenge kwenye Halmashauri za Wilaya hukohuko ambapo wananchi walipo kwa lengo la kutoa huduma kwa urahisi ili kumuondolea gharama mwananchi aliyeo kwenye halmashauri hiyo. Kwa hiyo, lengo ilikuwa ni kumuondolea gharama mwananchi aliyeo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wapi makao makuu hiyo inajengwa ilikuwa ni maamuzi ya wananchi wenyewe kuititia wawakilishi wao Baraza la Madiwani ambalo pia lenyewe limejadili pamoja na watalaaam na kuchagua maeneo ya kujenga. Baada ya uchaguzi huo, sasa ujenzi utanza na Serikali tulikuwa tunapeleka fedha na tumepeleka fedha; tumeanza awamu ya kwanza kugawa fedha kupeleka kwenye halmashauri mpya ili wajenge Makao Makuu ya Halmashauri; tumepeleka pia awamu ya pili na tutapeleka awamu ya tatu kwa sababu bado hatujakamilisha halmashauri zote. Lakini bado kuna halmashauri ambazo pia zina miundombinu kongwe, nazo pia tunazijengea makao makuu mpya. Kwa hiyo, tutapeleka pia na fedha kwenye halmashauri kongwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, malengo yetu ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hizi kwa ukaribu kuondoa gharama ulioisema kwa kupeleka mahali ambapo wao wamepanga na ndiko kunawarahisishia kupunguza gharama hizo, hayo ndio malengo. Sasa

inawezekana pia huko wamepanga vinginevyo inawasababishia wengine kuwa na gharama kubwa lakini njukumu lao kupanga wapi wanaweza kujenga Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua yapo maeneo ambayo jiografia yake haiwezekani; Wilaya kama Uyui tulipata shida sana tulipoamua wajenge makao makuu maeneo yalipo sasa kwa sababu Halmashauri ya Uyui iko kama yai imezunguka Manispaa ya Tabora. Kwa hiyo, mtu anayetoka huku lazima apite Makao Makuu ya Mji ili aende kwenye Makao Makuu mpya. Zipo halmashauri jiografia yake ni ngumu lakini lazima tuanze mahali halafu tuende mahali vizuri. Kwa hiyo, tutaendelea kusikiliza maeneo yote yenye jiografia ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hivi karibuni nilikuwa Wilayani Mbanga Mkoani Ruvuma, nilikuta hiyo, Halmashauri ya Mbanga Vijiji ambayo Mheshimiwa Mbunge hapa yupo ramani/jiografia yake ni ngumu kidogo, popote utakapoweka Makao Makuu ya halmashauri, lazima kutakuwa na mgogoro lakini bado tunapokea changamoto hiyo na tutaifanya kazi. Malengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hizo ili iwarahisishie katika kutoa huduma na wananchi wapate huduma kwa ukaribu kwa gharama nafuu, hayo ndio majibu ambayo kwa sasa Serikali inayafanya kazi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, swali kwa Waziri Mkuu.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba tumekuwa na Benki ya Kilimo na Tanzania *Investment Bank* ambazo zimekuwa na riba kubwa vilevile mtaji wake ni kidogo. Lakini pia tumekuwa na mifuko ya kuchochea

maendeleo mingi. Je, Serikali haioni kama tuna haja ya kuwa na mfuko wa kuchochea maendeleo ya kilimo na viwanda ili wananchi waweze kwenda kupata mikopo ya kuijwezesha kujiedeleza katika kilimo na viwanda kwa riba nafuu? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kainja, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua mkakati wa Serikali wa kuanzisha mfuko ambaao unaweza kutoa mikopo kwa urahisi na kwa gharama nafuu hasa kwenye riba baada ya kuwa ameringanisha uwepo wa benki *TADB* na *TIB*. Ni kweli kwamba Serikali inaendelea kuhamasisha taasisi za fedha zote pamoja na mifuko mbalimbali inayolenga kukuza kilimo, ili iweze kuwafikia wakulima wadogowadogo, wa kati na wakubwa ambaao watawekeza kwenye viwanda na mashamba yenewe iliwaweze kupata mikopo tena kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho kinafanyika sasa ni kwamba mazungumzo yetu kati ya Serikali na mabenki binafsi tumekubaliana mabenki haya kutoa mikopo tena wajitahidi kupunguza riba na hata Mheshimiwa Rais juzi amesilitiza benki zipunguze riba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, tukasema tuanzishe benki yetu inayoshughuikia kilimo ili iweze kutoa mikopo kwa gharama na riba nafuu. Na tunayo tayari *TADB* ambayo inashughulikia kilimo lakini tuna benki ambayo pia Mheshimiwa Mbunge ameitaja *TIB* (*Tanzania Investment Bank*) ambayo pia na yenewe ina eneo linashughulikia kilimo. Wakati huohuo tunayo mifuko mingi sana imejikita kwenye maeneo mbalimbali ambayo sasa tunaishughulikia ili kuipunguza idadi kubwa ya mifuko ili tuwe na mfuko angalu mmoja utakaokuwa unashughulikia kuratibu shughuli za kilimo kwa kukopesha na kuhakikisha kwamba inahudumia sekta nzima ya kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili litakapokamilika, sasa tutakuwa na mfuko unaoshughulikia kilimo ambaao ni wetu wenyewe Serikali ambaao pia utakuwa unaungana na Benki yetu ya Kilimo na mabenki mengine ili ihudumie wananchi wa kawaida wanaojishughulisha na kilimo kuanzia kule kwenye ngazi za vitongoji, vijiji na wale wakulima wakubwa ambaao pia wanawekeza kwenye viwanda vinavyochakata malighafi za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yetu sasa ni kihakikisha kwamba Sekta ya Kilimo inakua kwa kasi na juzi nilikuwa Mkoani Singida kuzindua kampeni ya kilimo cha alizeti nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya mambo makubwa ambayo wadau walichangia ni kukosekana kwa mitaji ya kuanzisha killmo lakini nimetoa maelekezo kwa mabenki yetu na tulikuwa na mabenki pale ikiwemo na hizi benki zetu ambazo tunazo mpaka vijiji kama vile *CRDB, NMB* lakini pia tuna *NBC, Azania Bank* na hiyo *TIB* na *TADB* yenyewe kuhakikisha kwamba inakuwa na matawi mpaka ngazi ya wilaya na inatangaza hiyo fursa ya wakulima kwenda kukopa lakini pia kila benki ihakikishe inawezekana pia inapunguza riba zao ili ziweze kuwawezesha wakulima kumudu kukopa na kurejesha kwa wakati. Wakati mwingine nao wasaidie pia namna ya kuzipata hizo fedha kwa sababu iko tabia ya kila mmoja anataka kukopa lazima awe na andiko, mwananchi wa kawaida hajui andiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumesema lazima waanzishe dawati la kusaidia kutengeneza hilo andiko na halmashauri nazo tumeziagiza na zenyewe ziwe na maafisa wanaoshughulikia namna ya kumuwezesha mkulima kuwa na andiko linalomuwezesha kupata mikopo. Haya yote yatapelekea sasa kwenda kutoa huduma kwa wakulima ili waweze kulima lakini kutoa huduma kwa wawekezaji wa sekta ya kilimo wapate mikopo na wawekezaji kwa kiwango cha katika nao wapate mikopo ili mkakati wetu wa Serikali wa kuboresha kilimo nchini uweze kushamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yetu ya Serikali ambayo pia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amesisitiza ni kuhakikisha kwamba kilimo kinashamiri nchini ili sasa maazimio ya uchumi wa mtu mmoja mmoja yatatokana na kila mmoja kujishughulisha kwenye kilimo kwa kupatiwa mitaji na vinginevyo. Kwa hiyo, Serikali tunaendelea na utaratibu huo ili tuweze kutoa mikopo kwa wakulima wetu kwa riba nafuu, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali nyingi zilizojengwa hivi karibuni hasa hizi Wilaya mpya hazina vifaa tiba vya kupimia wagonjwa kwa maana ya *X-ray* pamoja vifaa vingine. Ni lini kauli ya Serikali itapeleka kwenye haya maeneo hapa nchini vikiwemo Urambo, Mbogwe pamoja na Msalala, Chamwino hapa Dodoma na Tanzania Visiwani. Nataka kujua azma ya Serikali ni lini itapeleka vifaa tiba hivyo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nicodemas Maganga ahsante sana. Swali lako atalijibu Mheshimiwa Waziri wa Afya atakapopata fursa ya kujibu maswali. Mheshimiwa Jerry William Slaa, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe Sita ya mwezi Aprili Mheshimiwa Rais katika shughuli ya kuapisha Makatibu Wakuu alitoa kauli ya kusikitishwa kwa jinsi wawekezaji wanavyokwamishwa kwenye vibali vya kazi. Katika kauli yake alitoa maelekezo ya Serikali kutengeneza utaratibu mzuri wa kuwasaidia wawekezaji kutopata mkwamo katika suala la vibali vya kazi ili kuweza kuboresha uwekezaji. Mheshimiwa

Waziri Mkuu, kauli hii imepokelewa kwa furaha sana na wawekezaji wengi na imetoa sura mpya katika sekta ya uwekezaji nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo kauli hii imechukuliwa tofauti na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waadilifu wameanza kuleta wafanyakazi kwenye maeneo ambayo wazawa wanawenza kufanya kazi hizo. Mfano ni marubani kwenye baadhi ya kampuni binafsi za ndege. Naomba kujua kauli ya Serikali, ni nini mkakati wa kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais katika kuwaondolea vikwazo na urasimu wawekezaji kupata vibali vyataga, wakati huohuo kuendelea kutimiza matakwa ya sheria *The Non-citizens Employment Act, 2015* Kifungu cha 11(2) ambacho kinalinda ajira za Watanzania kwenye maeneo ambayo wana uwezo wa kufanya kazi. Ahsante. (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameeleza utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa alipokuwa anawaapisha Makatibu Waku una hasa katika kuboresha uwekezaji nchini. Uwekezaji nchini ni mkakati mpana kwa sababu kwanza tunahamasisha kujenga uchumi wetu na katika ujenzi wa uchumi moja ni kukaribisha wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwenye uwekezaji lakini wawekezaji hawa nao wanao watu ambao wanaamini wanawaamini kushiriki kwenye shughuli zao za uendeshaji wa uwekezaji wao. Sasa nasi Serikali tumeweka sheria kidogo kwa wawekezaji ambayo haipanui wigo mpana ukapoteza fursa ya Watanzania kushiriki kwenye uwekezaji huo ikiwemo na ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anapotaka kujua tunachukua hatua gani ya wale ambao wanatumia nafasi hii vibaya, Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa bahati nzuri hili jambo lipo ofisini kwangu na tunalismamia vizuri. Kwanza tunahamasisha wawekezaji wote

kuja nchini kuwekeza kwenye sekta mbalimbali kwa fursa tulizonazo lakini mbili tunawahamasisha Watanzania kushiriki kwenye uwekezaji huu ili na wao wawe sehemu ya ujenzi wa uchumi kupitia uwekezaji. Pia kwenye uwekezaji huu tumetangaza fursa zilizopo ajira lakini pia bidhaa tunazosalisha kuwa kama malighafi ya uwekezaji huo ikiwemo na kilimo na vinginevyo kwamba Watanzania washiriki huko ili waweze kunufaika na uwekezaji huu kwenye maeneo hayo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale ambapo Mwekezaji anataka kuja kuwekeza na fedha yake lakini ana idadi ya watu anaotaka kufanya kazi, nalo pia tumeliangalia kwamba mwekezaji huyu asije akaleta idadi kubwa halafu akapoteza fursa za Watanzania kuingia pia kwenye ajira. Nini tunakifanya sasa tunatengeneza sheria na maboresho ya sheria zetu zinazoweza kuwafanya wawekezaji wasikwazwe kuwekeza nchini lakini na sisi Watanzania tusipoteze fursa ya kuweza kuajiriwa ili tuweze kwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, matumizi ya fursa hiyo vibaya nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunasimamia vizuri na hasa maboresho ambayo tunayafanya kwenye uwekezaji. Maboresho haya yana nia njema sana hasa katika kutoa fursa kwa Watanzania kwenye maeneo mengi tu, kwamba maeneo haya yote ambayo tunayalenga yaweze kuwanufaisha Watanzania, ndiyo malengo yetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na mashaka maelekezo ya Mheshimiwa Rais tumeyapokea na tunayasimamia ili yasitumike vibaya na wale wenye nia mbaya kwenye maeneo haya. Haya ndiyo malengo ya Serikali kwa hiyo niendelee kutoa wito kwa wawekezaji waje nchini tuna ardhi ya kutosha, maji, umeme, malighafi ya kutosha lakini pia tuna *labor* inayojituma sasa ya Watanzania kwamba mwekezaji akija Tanzania hawezikujuta kwa nini amekuja kuwekeza Tanzania. Tunaanza kuona idadi kubwa ya wawekezaji wanakuja na huduma

wanaendelea na wanapata vibali kwa siku chache sana kutoka siku wanapoomba kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara zetu za Uwekezaji na Viwanda na Biashara lakini pia Wizara yetu ya Ardhi zote hizi zinafanya kazi kwa pamoja ili kumwezesha mwekezaji kupata huduma yake kwa haraka sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba swalii kwa Waziri Mkuu.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuuliza swalii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuwa na mpango mzuri juu ya uwepo wa nishati ya gesi asilla nchini lakini mpaka sasa kumekuwa na sintofahamu juu ya mwendelezo wa uwekezaji wa miradi ya gesi, kwa mfano gesi ya Mkoa wa Mtwara. Nini kauli ya Serikali juu ya mwendelezo wa miradi hii nchini, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swalii hilo atajibu Waziri wa Nishati kwa wakati ambao utapangwa. Kwa hiyo, nadhani upeleke kama swalii ili ajibu Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa majibu, muda wako wa kujibu maswali umekwisha. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi Mbunge wa Msalala sasa aulize swalii lake.

Na. 440

Halmashauri ya Wilaya ya Msalala Kuwa Wilaya

MHE. IDDI K. IDDI aliuliza: -

Je, lini Serikali sasa itaipandisha Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kuwa Wilaya kamili

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA ZIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuanzisha Mkoa na Wilaya mpya umebainishwa kuitia Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya. Kwa mujibu wa Sheria hii, utaratibu wa kuanzisha Wilaya mpya huanzia kwenye Serikali za Vijiji/Mitaa ili kupata ridhaa ya wananchi kisha hupelekwa kwenye Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*). Baada ya hatua hiyo, maombi hayo huwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na kujiridhisha na baadaye kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili akiridhia atoe kibali cha kuanzishwa kwa Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala iko katika Wilaya ya Kahama ambayo ni moja kati ya Wilaya tano zinazounda Mkoa wa Shinyanga. Halmashauri ya Wilaya ya Msalala bado haijaanza mchakato wa kuomba kuwa Wilaya kwa kadri ya matakwa ya sheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Msalala yapo

katika Kata ya Ntobo na ukizingatia Kata zake zilivyokuwa mbalimbali hususan Kata za Isaka, Mwalugulu, Jana na Mwakata kupata taabu sana kupata huduma za ki-Halmashauri. Sasa nini mpango wa Serikali wa kuanzisha Mamlaka ya Mji mdogo katika Kata ya Isaka ili kuwawezesha wana Isaka nao sasa waweze kupata huduma kwa urahisi. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA ZIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kassim Iddi Iddi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba tu kwamba kwa nini sasa Serikali isianzishe Mamlaka ya Mji Mdogo katika eneo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Msalala kwenye Kata ya Ntobo kama alivyoeleza. Kwa hiyo, ametaka kujua ni lini lakini jibu langu la msingi utaratibu ni uleule kwamba mkitaka tuanzishe haya Mamlaka maana yake mfuate taratibu hizi ambazo tumezianisha, mlete maoni yapitie katika ngazi zote na sisi tutafanya tafakuri na tathmini na baadae tukishajiridhisha basi maomba hayo tutayapeleka kwa Mheshimiwa Rais ambaye ndiye ana mamlaka ya mwisho kabisa ya kutangaza maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ndilo jibu la Serikali anzisheni mchakato nasi tutakuja tufanye tathmini. Ahsante.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza Mamlaka ya Mji wa Vwawa inahudumia Mkoa wa Songwe. Je, ni lini Serikali itaupandisha hadhi Mamlaka ya Mji wa Vwawa kuwa Halmashauri ya Mji.

NAIBU SPIKA: Japo naona majibu yanafanana na ulilotoka kusema lakini naona anataka asikie yeye

mwenyewe kwamba mchakato waanzishe wao. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA ZIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunisaidia kujibu. Kikubwa ni kwamba kwanza na mimi mwenyewe nina *interest* kwa sababu natokea katika Mkoa huo huo wa Songwe na ninaufahamu vizuri Mji Mdogo wa Vwawa ambaa unahudumia kwa sasa Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Songwe.

Kwa hiyo, kikubwa mimi na wewe pamoja na Mkuu wa Mkoa wetu ambaye anatusikia sasa hivi nafikiri tuanzishe tu mchakato mapema halafu ikishafika katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ninaamini tuki-*meet* vigezo vyote basi tutafanya hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliomba, ahsante.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwa kuwa utaratibu wa kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Sumve ulishafuata taratibu zote ikianzia vikao vya ngazi ya Halmashauri mpaka vikao vya ngazi ya Mkoa na sasa suala hilo lipo TAMISEMI. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha mchakato huu wa kuanzisha Halmashauri ya Wilaya ya Sumve ili watu wa Sumve waweze kupata huduma kwa ukaribu zaidi.

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Kasalali Mageni kwa sababu umesema la kwenu limeshafika huko Wizarani na Naibu Waziri anaweza kuwa hajapata hiyo kabrasha, kwa hiyo, atakujibu atakapokuwa amepitia hilo kabrasha kuona kwamba ni lini, maana hapa atakuja apige maneno tu wakati hajapitia hilo kablasha.

Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi sasa aulize swali lake.

Na. 441

Daraja Linalounganisha Wilaya ya Kilindi na Kiteto

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Wilaya ya Kilindi na Kiteto kupitia Kijiji cha Sambu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA ZIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mnadani – Sambu - Pagwi ni barabara ya mkusanyo (*Collector Road*) yenye urefu wa kilomita 38. Barabara hii inaanzia barabara ya *TANROADS* ya Kwaluguru-Songe-Kibirashi inapita katika maeneo ya Changanyikeni, Kigunga, Sambu, Makelele, Lumotio, Pagwi na kuishia katika eneo la Lugira katika Wilaya ya Kiteto ambako inaungana na barabara ya Kijungu – Sunya – Dongo katika Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 barabara hii imetengewa kiasi cha shilingi milioni 182.52 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 10.5, ujenzi wa kalvati tisa na vivuko mfuto (*drift*)vinne.

Mheshimiwa Spika, barabara hii itaendelea kutengewa fedha kulingana na upatikanaji wa fedha kila mwaka ili kutatua changamoto iliyopo ya kutopitika kwa barabara hii.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya ya kusema kwamba huu wa fedha unaoanza

keshokutwa hapo tumetengewa shilingi milioni 182 kwa ajili ya kutengeneza kalavati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi lilikuwa linazungumzia kwamba ni lini Serikali itatengeneza daraja, kama katika maelezo yake alivyosema kwamba eneo hili lina kilometra 38 zinazounganisha Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Kilindi. Eneo hili lina changamoto kubwa kwa sababu daraja ni kubwa sana, kiasi hiki kilichotengwa hakitoshi hata kidogo kwa ajili ya kujenga daraja.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakwenda yeye au wataalam wake kwenda kuangalia upana wa daraja hili ili Serikali iweze kutenga fedha za kutosha? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; miaka ya nyuma Serikali ilishatenga pesa kwa ajili ya daraja hili, lakini nina uhakika thamani ya fedha kwenye daraja hili haikufanyika.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutuma timu kuona kama fedha hizi zilitumika ipasavyo? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa anachokieleza Mheshimiwa Mbunge, kwamba daraja lile ni kubwa na Bonde la Mto Sambu kama alivyokuwa amelianisha hapa ni bonde ambalo limeongezeka na linakadiriwa kuwa urefu wa mita 75. Na kwa tathmini ya awali ambayo ilikuwa imefanyika kwenda kufanya matengenezo katika eneo hilo ambalo linahusu hilo daraja, kuna makaravati kama 18, pamoja na *drift* yaani vile vivuko mfuto vidogo zaidi ya 30 na kitu. Na ilivyofanywa tathmini ya fedha ya awali ni

kwamba eneo hilo linahitaji zaidi ya bilioni 2.9 ili kuhakikisha hiyo barabara iwe inapitika muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi tu niseme kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema mimi mwenyewe nitafika eneo hilo ili niweze kushuhudia, na vilevile nitaituma timu kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenda katika eneo husika. Lakini kikubwa ni kwamba kwa sasa tuna ufinyu wa bajeti ndio maana umeona tumetenge hizi fedha chache. Lakini Bajeti Kuu ya Serikali ikipita, na kile chanzo kipyaa ambacho tunapelekea fedha kuongezea *TARURA* ninaamini tutazingatia hili ili barabara hii iweze kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge mpitishe Bajeti Kuu ya Serikali ili tupate kile chanzo cha uhakika na ninaamini katika mwaka ujao wa fedha hili swali halitalizwa tena, tutakuwa tumeshalifanya kazi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 442

Ujenzi wa Barabara ya Kibaoni – Kasansa hadi Mlowo

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza: -

Je, ni lini Barabara ya kutoka Kibaoni – Kasansa – Muze – Illemba – Kilyamatundu hadi Mlowo itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) aliijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakangáta, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kibaoni hadi Mlowo ni barabara ya mkoa yenyé jumla ya urefu wa kilomita 363 na inaunganisha mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe. Barabara hii inapita katika bonde la Ziwa Rukwa ambalo ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na uvuvi na hivyo kuwa kichocheo kikubwa cha kiuchumi katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali ilianza mipango ya kuijenga kwa kuanza na ujenzi wa Daraja la Momba ambalo lilikuwa kikwazo kikubwa cha mawasiliano kati ya mikoa hii mitatu ya Rukwa, Katavi na Songwe ambao umekamilika. Ili kukamilisha ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami kuanzia Kibaoni hadi Mlowo ambayo ni kilomita 363, Serikali ipo katika hatua ya awali ya kufanya upembizi yakinifu na usanifu wa kina ambapo kazi inaendelea kwa sehemu ya Kibaoni – Majimoto yenyé urefu wa kilomita 27 iliyopo mkoani Katavi na sehemu ya Muze – Kilyamatundu yenyé urefu wa kilomita 141 iliyopo Mkoaa wa Rukwa. Kwa upande wa Mkoaa wa Songwe, kazi ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Mlowo – Kamsamba yenyé urefu wa kilomita 130.1 imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa upembizi yakinifu na usanifu wa kina, Serikali itanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyogeza. Kwanza kabisa nipende kuipongeza na

kuishukuru Serikali kwa kutujengea hilo daraja liligharimu zaidi ya karibu bilioni 17. Tunashukuru sana. Iakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Serikali sasa ina mpango gani wa kutujengea hata basi kuitengeneza hiyo barabara hata kwa kiwango cha changarawe ili wananchi waweze kupita katika barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini swali la pili ninaomba sasa *commitment* ya Serikali, kwa sababu barabara hiyo ni muhimu sana kwa uchumi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe. Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni kweli kwa mwaka jana na mwaka huu ilikuwa imeharibika sana. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi ninavyoongea madaraja yote yameshajengwa, bado madaraja mawili ambayo mkandarasi anakamilisha. Kwa sasa barabara hii inapitika vizuri kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni lini tutaanza ujenzi; kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi. Barabara hii tunatambua umuhimu wake ndiyo maana tayari tumeshakamilisha usanifu wa kina kwenye kilomita zote, na bado kilomita 27 ambazo wako tayari wanafanya usanifu ili barabara yote ikamilike kwa usanifu na baada ya hapo ndipo ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa niaba ya Wizara nimshukuru kwamba ameipongeza Serikali kwa kujenga Daraja la Mto Momba ambalo lilikuwa ni kikwazo kikubwa. Hiyo ndiyo adhma ya Serikali; na sasa mizigo yote kutoka Rukwa inapita daraja la Momba kwenye Mlowo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Morogoro Manispaa ambayo Mheshimiwa Naibu Spika unaifahamu na unaitumia kila mara unapokwenda Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari pale Msamu? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayosema ambayo itakuwa barabara ya *by-pass* ni barabara ambayo muhimu, binafsi nimepita na Mheshimiwa Ishengoma tumeongea naye. Ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu na tutaingiza kwenye mpango ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kupunguza msongamano wa kupita magari yote katikati ya Mji wa Morogoro. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Ishengoma kwamba mpango huo upo na katika siku zinazokuja kadri ya fedha zitakapopatikana barabara hii itajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna barabara ambayo inatoka Lumecha – Kitanda, Londo inakwenda mpaka Malinyi kutokea Lupilo, Ifakara na ipo katika llani ya Uchaguzi na barabara ile ya Serikali Kuu.

Je, Serikali inaweza ika-concentrate kuanza kuifungua ile barabara kutokea Kitanda – Londo mpaka Kilosa kwa Mpepo mpaka Malinyi ili ianze kuitika wakati utaratibu wa kujengwa kwa lami unaendelea?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoisema ya Lumecha – Londo Kilosa kwa Mpepo – Malinyi hadi Ifakara na Mikumi ni barabara kuu kama alivyoisema. Tunafikiria kuifungua barabara hii ili iweze kutumia, na hasa kuanza na kipande ambacho kina miinuko mikali kati ya Londo na Kilosa kwa Mpepo. Ikishafunguka nadhani itapitika kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira Serikali itafute fedha ili hapo paweze kukamilika na kupatengeneza vizuri, kwa sababu ndiyo changamoto kubwa ya hiyo barabara kushindwa kuitika muda wote wa mwaka. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhe. Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Iko nia ya Serikali ya kujenga barabara ya kutoka Mkiwa kwenda Noranga kilometra 56.9 ambayo

ilikuwa imetangazwa mwaka 2017, na sasa hivi katika bajeti iliyopita alisema kwamba wataitangaza. Je, ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massare kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara iliyotajwa ni barabara ambayo imepata kibali na taratibu zote zimekamilika; muda wowote itatangazwa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Mbunge tumeongea naye mara kadhaa, pamoja na Mbunge wa Chunya Mheshimiwa Kassaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inatarajiwa kutangazwa muda wowote kwa sababu imeshapata kila kitu na imekamilika, kwa maana ya kutangazwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu ni kwamba, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Daraja la Mto Luhulu linalouganisha Wilaya ya Nyasa na Ludewa linakamilika? Kwa sababu kwa sasa hata ile Pantoni iliyokuwa inatumika nayo imeharibika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mhandisi Stella Manyanya Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja analolisema linaunganisha Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Ludewa. Katika bajeti yetu ni katì ya madaraja ambayo yamepangiwa fedha kwa ajili ya kujengwa katika bajeti inayokuja. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara bajeti itakapoanza kutekelezwa daraja hili litaendelezwa kujengwa ili liweze kukamilika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na 443

Upanuzi wa Uwanja wa Ndege Musoma

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza: -

Je, ni lini ukarabati na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma utakamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalì la Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi atakaetekeleza mradi huu. Aidha, mkataba katì ya Serikali na mkandarasi *Beijing Construction Group Co. Ltd* umesainiwa Disemba, 2020 na utekelezaji wa mradi huu utakamilika kwa kipindi cha miezi 18, baada ya kuanza hatua za utekelezaji. Hivi sasa Serikali imemaliza awamu ya pili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huu ili kuruhusu mkandarasi kuanza hatua ya utekelezaji wa ujenzi.

Hata hivyo, Serikali imeshamkabidhi mkandarasi eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Esther N. Matiko kwamba, Serikali ina nia ya dhati ya kukarabati na kupanua Kiwanja cha Ndege cha Musoma na utekelezaji wake utakamilika baada ya miezi 18 kama nilivyosema nilivyosema. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Uwanja wa Ndege wa Musoma ni uwanja wa kimkakati, kwa maana Mkoa wetu wa Mara umejaaliwa madini, mbuga za wanyama, makumbusho ya Baba wa Taifa, samaki na biashara mbalimbali, hivyo ungeweza kunufaisha taifa iwapo ungejengwa kwenye kiwango cha kimataifa ili ndege ziweze kutua moja kwa moja tofauti na ilivyosasa hivi watalii wanatua Nairobi au Arusha ndipo wanakuja kwenye mbuga ya Serengeti.

Ningependa kujua sasa, huu ujenzi na ukarabati ambao unaokadirwa kukamilika ndani ya miezi 18, unatarajia kuwa na *run ways* pamoja na jengo la abiria la kiwango cha kimataifa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, pale Tarime tuna Uwanja mdogo wa Magena ambao hutumiwa na watalii na wale ambao wanakwenda migodi kwa kutua na ndege ndogondogo. Na sasa hivi upo chini ya halmashauri ambapo unaikosesha mapato Serikali, kwa maana imekodiswa kwa makampuni binafsi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuchukua uwanja ule ili uje kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwenye Serikali Kuu ili pia uweze kukarabatiwa na kuweza kutumika na kuongeza kipato cha taifa? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uwanja wa ndege wa Musoma ni uwanja ambao ni wa kihistoria, ni uwanja ambao uliasisiwa na Baba wa Taifa hili. Vilevile upo kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na viongozi wetu wa mkoa wanausimama pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Mara. Na mimi pia ni sehemu ya eneo hilo la mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie kwamba uwanja tayari, kulikuwa na eneo limebakia, kama mita 105, ili kila aina ya ndege hata kama iwe kubwa iweze kutua pale. Tumeshalipa, fidia imekamilika. Kwa hiyo, ndege zote muhimu zitatua katika eneo hilo na watalii kutoka Kenya watatua Musoma watakwendwa Serengeti kwenye shughuli zao, na uchumi wa Mkoa wa Mara na maeneo mengine utafunga.

Vilevile swali lake la pili linalohusu Uwanja wa Ndege mdogo pale Magena. Wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi alikuwa pale, amefungua mnada wetu pale wa Magena, maana yake itaongeza soko la kibiashara katika eneo hilo, kuna mifugo itauzwa katika eneo hilo. Uwanja huu upo chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalipokea wazo hili, tufanye tathmini, tuangalie uwezo wa Serikali, ikiwezekana upanuliwe na kusimamiwa ili ndege ndogo za watalii ziweze kutua pale, na hivyo itapunguza msongamano pia kuja Musoma na badala yake watakuja kule Tarime ambapo kimsingi watalala Tarime, watakula Tarime, watafanya kazi Tarime na uchumi wa Tarime utafunguka. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Maji, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 444

Tatizo la Maji Kata la Jimbo la Kilwa Kaskazini

MHE. FRANCIS K. NDULANE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafikisha huduma ya Maji kwa Wananchi wa Kata za Kipatimu, Kibata, Chumo, Kandawale, Namayuni, Miguruwe, Njinjo, Mitole na Kinjimbi katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ili kuwaondolea adha ya maji inayowakabili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis K. Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji kwa kutekeleza miradi Wilayani Kilwa ambayo imehusisha uchimbaji wa visima virefu nane, ukarabati wa tanki la maji la lita 45,000 katika Kijiji cha Kipatimu, ukarabati wa mradi wa maji Mtubei Mpopera katika Kata ya Kandawale na ujenzi wa vituo 11 vya kuchotea maji. Kukamilika kwa kazi hizo kumeboresha upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 68.5.

Mheshimiwa Naibu Spika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza katika Wilaya ya Kilwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ikiwemo uchimbaji wa visima virefu sita katika Vijiji vya Mitole Kata ya Mitole, Zinga kibaoni Kata ya Miguruwe, Namayuni Kata ya Namayuni,

Kisima-Mkika Kata ya Njinjo, Kibata Kata ya Kibata na Ruhatwe Kata ya Kikore. Pia, ujenzi wa miradi mitano ya mitandao ya mabomba ya matanki ya kuhifadhi maji katika Vijiji vya Kinjimbi Kata ya Kinjimbi, Chapita Kata ya Migumbi, Chumo Kata Chumo, Marendego Kata ya Somanga na Kipindimbi Kata ya Njinjo. Aidha, katika vijiji hivyo kutajengwa vituo 50 vya kuchotea maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu namba moja la nyongeza ningependa kufahamu, kwa kuwa katika Mikoa ya Kusini kumekuwa na vyanzo vingi vya maji vinavyotokana na mito mikubwa kama ule wa Rufiji, Ruvuma, Mavuji, Lukuledi, Luhuhu pamoja na Ketewaka kule Njombe. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inamaliza tatizo la maji kwa asilimia 100 kama ilivyofanyika Kanda ya Ziwa kuititia vyanzo hivi vya maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Ndulane kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri. Nipende tu kumjibu swali lake la nyongeza la matumizi ya maji yote yanayopatikana kwenye mito na vyanzo vyote vikubwa vyenye uhakika kwa miradi endelevu. Sisi kama Wizara, mikakati yetu katika mwaka ujao wa fedha na kuendelea, ni kujenga miradi mikubwa inayofanana na mradi huu wa Ziwa Viktoria. Mikakati imekamilika na kwa Kusini pia tumepanga kutumia Mto Ruvuma, Mto Rufiji na Ziwa

Tanganyika. Hii yote tutakuja kuitekeleza kadri tutakavyokuwa tukipata fedha. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Naomba kuuliza swalii moja la nyongeza kwamba, katika Jimbo la Newala Vijijini, kuna Mradi wa Maji wa Mnima Miuyu, mradi huu ulikuwa ni wa miezi tisa, ulikuwa ni mwaka 2018 na hadi leo hii haujakamilika. Je, ni lini mradi huu utakamilika ili wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini waweeze kupata maji ya uhakika? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Naomba kujibu swalii la Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ambayo utekelezaji wake umeanza na ipo katika process, yote lazima itakamilika kadri fedha tunavyozipata na kadri ya muda ulivypangwa. Hivyo nipende kumtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, namna ambavyo amekuwa akizungumza nasi mara kwa mara, tuendelee kuwasiliana kwa karibu na tutakwenda pia kuona kazi imefikia wapi na kazi itakamilika kadiri inavyotakiwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Wakati tukimalizia hicho kipindi kuna mambo machache.

La kwanza, ni swalii la Mheshimiwa Nicodemus Maganga, niliagiza Wizara ya Afya, nadhani Wizara ya Afya na TAMISEMI, mmojawapo atakuwa anahusika na hilo swalii la kupeleka vifaa kwenye hospitali zetu. Ni muhimu sana

Waheshimwa Mawaziri siku ambayo wazi Mkuu anakuwa na maswali hapa Bungeni kuwepo, maana mnaweza kutakiwa nyle kujibu badala ya yeye. Yeye anajibu maswali ya kisera, maswali ya lini, sijui nini kitafanyika wapi, ni kazi yenu nyie, kwa hiyo Wizara hizo mbili ziangulari hilo swali la Mheshimiwa Maganga Nicodemas, majibu yake yatakapokuwa tayari Ofisi ya Katibu wataweka kwenye orodha.

Pia swali la Mheshimiwa Shamsia Mtamba, aliuliza kuhusu uwekezaji kwenye gesi na hiyo miradi. Kwa hiyo Waziri wa Nishati na Waziri wa Uwekezaji wataangalia linamuhusu nani hasa, ili anayehusika aweze kuja kujibu hilo swali na litawekwa kwenye orodha ya maswali.

Waheshimiwa Wabunge, hapa mbele huwa tunasikiliza sana maswali yenu na wakati mwengine ni kweli sisí kama wawakilishi wa wananchi, tunataka kusikia wananchi wetu wanasemaje. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika alishawahidi kutoa hapa ushauri wa jumla na tuna changamoto sana kwa sababu wakati mwengine akiwa anazungumza, Wabunge wengine nao wanakuwa wakizungumza, kwa hivyo hawasikilizi, wanarudia makosa yale yale.

Waheshimiwa Wabunge, swali lako likipata hapa majibu, ulishikilie hilo bajeti ijayo mwakani uweke kuliuliza lazima uwe umeliuliza vizuri. Uwe umeangalia Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano, umeangalia Mpango wa Serikali wa mwaka mmoja, umeangalia sasa hivi tupo kwenye kipindi cha bajeti. Hiyo barabara yako unayouliza iko kwenye bajeti au haiko, ili akikujibu Waziri kama haipo wewe unamtafuta mwakani, maana sasa hivi hata ukisisitiza sana, jibu atakalokupa halitaleta majibu chanya kwenye jimbo lako.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo lazima tusome hizi nyaraka tunazoletewa, usiseme tu nilishauliza Bungeni si mmesikia, hapana; wananchi ukishauliza wanataka mabadiliko kule kwenye Jimbo lako. Sasa ili wayapate lazima uulize swali kwa namna ambayo Serikali itatoa majibu ambayo wewe utaweza kuyafuatilia. Nadhani ni vizuri sana

tukiufuata ule ushauri alikuwa ameutoa Mheshimiwa Spika, itatusaidia kujua namna ya kuuliza maswali yetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa ya wageni mbalimbali waliotufikia siku ya leo.

Kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni viongozi wa CCM, Madiwani na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo ndugu Said Kaondo. Karibuni sana viongozi wetu na watumishi kutoka Ruangwa. (*Makof*)

Nadhani leo mmebahatika kabisa kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu maswali. Mmetuletea kiongozi shupavu, kiongozi mnyenyekevu sana huyu, anasikiliza kila mtu, mmemlea vizuri, tunawashukuru sana. Pia mtusaidie maana hapa nimeambiwa wapo na Madiwani na Viongozi wa Chama. Jamani mtutunzie Jimbo kule kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ili awe Waziri Mkuu lazima Jimbo lake likae salama. Kwa hiyo mtusaidie Jimbo lake liwe salama ili hapa awe anatujibu maswali akijua kwamba kule kuko shwari, hakuna mtu anamsumbuwa sumbuwa. (*Makof*)

Mwenyekiti wa Chama ndio yupi, Mwenyekiti tafadhalii tutunzie Waziri Mkuu, ahsanteni sana, mnaweza kukaa sasa. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Catherine Magige ambaye ni mdau wa utalii kutoka Jijini Arusha, Ndugu Jacqueline Mafuru. Karibu sana. (*Makof*)

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na wageni 30 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Hawa walishiriki shindano la ulimbwende wakiongozwa na Daudi Kitiku. Hili tangazo liko sawasawa

Daudi Kitiku, wako wapi hawa wageni wa Mheshimiwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa hapa naona mambo yamechanganywa kidogo, lakini walioshiriki shindano la ulibwende ndio wepi tena au wote mmeshiriki. Haya jamani hawa ni viongozi wa Serikali ya wanafunzi *UDOM*, sasa nadhani tutangaze matangazo mawili; wale walioshiriki ulimbwende hebu wakae kwanza.

Sawa sasa tuanze na Viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Ni hao waliosimama, karibuni sana, naamini hawa wanatoka kwenye majimbo yetu mbalimbali, tumefurahi sana kuwaona. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo ambao wameongozana na hawa, wao walishiriki shindano la ulimbwende na wote hawa sasa kwa ujumla wao wanaongozwa na Daudi Kitiku. Sasa wasimame wale walioshiriki shindano la ulimbwende. Haya karibuni sana, sasa hapa nimeambiwa tu walioshiriki sijajua mshindi ni yupi kati yenu, lakini tunawatachia kila la kheri. (*Makofi*)

Wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt Faustine Ndugulile, ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni wadau wa mitandao ya kijamii kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Samora Julius. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa 30 wa Mheshimiwa Omar Kipanga ambae ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Nicholaus Mbaga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mhehimiwa Ummy Nderiananga ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anasimamia watu Wenye Ulemavu. Hawa ni ndugu Angela Kilasi na Anuarite Mhiche. Karibuni sana. Ndugu Angela Kilasi ni yupi kati yenu, haya.

Waheshimiwa Wabunge huyu Angela Kilasi mnawoma amevaa miwani pale, ana ulemavu wa kuona na hakuzaliwa hivyo, amepata ulevu huo ukubwani. Baada ya kupata ulemavu huo hakukata tamaa na ameendelea kuendesha maisha yake na amejifunza namna mbalimbali za kuendesha maisha yake.

Waheshimiwa Wabunge, ili watu wengine wajifunze kwamba ulemavu sio mwisho wa kila kitu, hata ukiupata ukubwani au hata ukizaliwa nao, kwamba unaweza kufanya mambo mbalimbali, ndugu yetu huyu Angela Kilasi yeeye ameandika kitabu, ili kuwatia moyo watu wenye ulemavu na pia hata wale ambao hawana ulemavu, kwa sababu hata yeeye aliupata ukubwani na hujui lini linaweza kukupata, pamoja na kwamba tunajiombea na tunaombeana kwa Mwenyezi Mungu yasitupate, lakini yakikupata usikate tamaa. (*Makof*)

Sasa kitabu chake kinaitwa, " *NIMEPOTEZA MACHO SI UTU*" . Kitabu hicho Waheshimiwa Wabunge kinauzwa Sh.15,000 na Katibu wetu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi amemruhusu kuingia hapa ndani siku ya leo, amepewa meza hapo nje kwa ajili ya kuweza kuuza hivi vitabu vyake. Tumuunge mkono, tujifunze na pia hata kama sio kwa ajili yetu tuwanunulie na watu wengine kwenye maeneo yetu ya uwakilishi, ili wakisoma kitabu chake basi wanaweza kutiwa moyo kuendelea kufanya vizuri hata kama wamepata ulemavu wa kudumu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Mohamed Monni, ambao ni wanafunzi, walezi na wafanyakazi wa Chuo cha Maendeleo ya Kijana na Mtoto Mirambo Goima kutoka Chemba Mkoani Dodoma, wakiongozwa na Mheshimiwa Mwanaharusi Bato, huyu ni Diwani? Karibuni sana. Mheshimiwa Mwanaharusi Bato ambaye yeeye ni Diwani amewaongoza vijana wetu, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Samwelii Hhayuma ambao ni familia yake kutoka Hanang Mkoani Manyara,

wakiongozwa na mke wake ndugu Elizabeth Sukum. Karibuni sana. Kati ya nyie Elizabeth ndio yupi, wifi yetu jamani, shemeji kwa wengine. (*Makof*)

Pia Mheshimiwa Hhayuma anao wageni wengine 10, ambao ni Wachungaji na Wazee wa Kanisa la TAG (WARETA) kutoka Hanang, Mkoani Manyara wakiongozwa Mchungaji Patris Paulo, karibuni sana viongozi wetu. (*Makof*)

Tunao pia wageni 61 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambao ni viongozi wa CCM na Serikali, kutoka Kata ya Kikuyu Kaskazini Jijini Dodoma, wakiongozwa na Mheshimiwa Izrael Mwansasu. Karibuni sana wenyeji wetu hapa Dodoma. (*Makof*)

Tunao pia wageni 34 wa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambao ni wanafunzi wa Chuo Kukuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Tasneem Twaha. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na ndugu Saidi Amir. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambao ni marafiki zake kutoka Kibaha Mkoani Pwani wakiongozwa na ndugu Iren Matawana. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Soud Jumah ambao ni marafiki zake kutoka Idara ya Misitu na Maliasili Zanzibar na hao wanaongozwa na ndugu Ameir Ali. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Kata, kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara wakiongozwa na ndugu Faustine Ware. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni watano wa Dkt Florence Samizi ambao ni familia yake wakiongozwa na ndugu Naomi Mugendi. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Saashisha Mafue ambao ni wananchi wazaliwa wa Hai wanaoishi Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Vaola Mafue, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge hapa imeambiwa hawa ni wananchi wazaliwa wa Hai, sasa nasikia Vaola Mafuwe, nadhani naye huyu ni mzaliwa tu wa huko Hai hamna taarifa nyingine hapa. (*Makof*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Abdulhafar Idrissa ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, wakiongozwa na ndugu Rehema Karingo. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *Theology* - Nassa kutoka Busega Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na ndugu Doto Nhandi. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 14 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni Wanachama wa Chama na Viongozi wa *Tanzania Music Foundation* kutoka mikoa mbalimbali Tanzania. Mheshimiwa Pallangyo yeye ni mlezi wa chama hicho, karibuni sana. (*Makof*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara na huyu ni Ndugu Malkiori Sulle. Karibu sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambao ni watu wenye mahitaji maalum kutoka mikoa mbalimbali, wakiongozwa na Balozi wa utalii aliyefanikiwa kuupanda mlima wa Kilimanjaro ndugu Deogratus Chami. Karibuni sana. Aliyepanda Mlima wa Kilimanjaro ndio yupi hapo jamani, huyo hapo hongera sana. (*Makof*)

Waheshimiwa wabunge tunasisitizwa utalii wa ndani jamani, mmemwona ndugu yetu hapo Deogratus Chami, kama ye ye alipanda wewe unashindwa ninijamani. Nadhani safari ijayo inabidi tumshawishi Mheshimiwa Waziri Mkuu twende naye ndio watu wataelewa vizuri kwamba tunafanya utalii wa ndani. (*Makofi*)

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Juliana Masaburi ambae ni Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Mkoa, kutoka Mkoa wa Mara na huyu anaitwa Fidelis Manyerere. Sijui amekaa upande gani huyu, karibu sana kiongozi wa UVCCM. (*Makofi*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala Mheshimiwa Flora Sagasaga na Ndugu Leonard Mabula. Karibuni sana. Mwenyekiti wa Halmashauri ndio Flora, ahsante sana. Mmemwona Mwenyekiti wa Msalala huyo, wanawake tupo vizuri. (*Makofi*)

Tunao pia wageni mbalimbali walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni 10 ambao ni Viongozi na Wanachama wa *anti-corruption* kutoka Chuo cha St. John wakiongozwa na Ndugu Brighton Bernard, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni kutoka Jijini Dodoma aliyejuka kujifunza namna bunge linavyoendesha shughuli zake na huyu ni Ndugu Marick Burhan. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 26 na Walimu sita kutoka shule ya msingi Amani ya Chamwino ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu James Nyingati, karibuni sana, naamini mmejifunza mawili, matatu, katika hayo ambayo mmeshuhudia yakifanyika hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba kuna kikao cha uzinduzi wa Umoja wa Wabunge wapigania haki za Watanzania kunufaika kiuchumi, kutokana na mabaki ya mjusi aliyeihadhiwa Jijini Berlin Ujeruman. Mwenyekiti wa

Umoja huo, Mheshimiwa Riziki Lulida anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanachama wa Umoja huo kwamba siku ya leo Alhamisi tarehe 17, Juni saa 7.00 mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na kikao cha uzinduzi wa umoja huo kitakachofanyika ukumbi namba 44 Jengo la Utawala Annex. Waheshimiwa Wabunge ambaao ni wanachama wa Chama hiki mnasisitizwa kuhudhuria huko kwa ajili ya uzinduzi huo. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Umoja huo, Mheshimiwa Riziki Lulida anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanachama wa umoja huo kwamba siku ya leo Alhamisi tarehe 17, Juni saa 7.00 mchana mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na kikao cha uzinduzi wa umoja huo kitakachofanyika ukumbi Na. 44, jengo la utawala Annex. Waheshimiwa Wabunge, ambaao ni wanachama wa chama hiki, mnasisitizwa kuhudhuria huko kwa ajili ya uzinduzi huo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji, Wabunge sasa hivi wanakuwa kama na mazoea hivi ya kusema nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano, halafu Wabunge wanajibu. Niwakumbushe tena, ili mtu apate fursa ya kuzungumza humu ndani kwa Kanuni zetu, lazima awe ameruhusiwa na Kiti.

Kwa hiyo, Mbunge usiwafanye Wabunge wenzako waanze kukujibu. Kwa hiyo, hiyo salamu anaruhusiwa kusema Spika hapa mbele kwa sababu yeye ndiye anayeweza kuwaruhusu Wabunge kusema na sio Wabunge mmoja mmoja kusema hivi halafu ukitarajia Wabunge wenzio wakujibu. Kwa sababu, iko siku nyingine mtafika mahali mtasema nipigieni makofi. Nadhani mnanielewa. Kanuni zetu haziruhusu Mbunge kumwuliza mwengine ili kujibizana hivi. Ndiyo maana huwa tunazuia Mbunge kukujibu, inabidi wewe utulie, mwenzio aseme.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo huo hairuhusiwi kufanya hivyo isipokuwa aliyekaa hapa, kwa

sababu ndiye anayeweza kuwapa Wabunge fursa ya kuzungumza. (*Makofii*)

Baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, na hapa nimeshaletewa majina ya Wabunge mbalimbali ambao wanataka kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga atafuatia na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ajiandae.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na ushauri. Kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Fedha kwenye Sekta yetu ya Kilimo bajeti yake yote ni 0.93 ya bajeti kuu. Kwa hiyo, nashauri sana, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha kwenye jambo hili mnapokuja na bajeti ya mwakani kwenye Wizara yetu hii ya Kilimo ambayo inachangia pato la Taifa kwa asilimia 26, vile vile inachangia chakula kwa asilimia 100, basi mlete mpango ambao utakuwa endelevu, utakaoifanya Wizara hii iweze kukimbilia. Hii tumeshapitisha, lakini naomba sana Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo mtakapokuja mwakani, msije tena

na bajeti ya kilimo ambayo haifiki hata 1% ya *gross budget* ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote mnajua kabisa kwamba kwenye kilimo ndiyo tunategemea malighafi zote za kiwanda, kwenye kilimo ndiyo huko tunakotegemea kwenye chakula, kwenye kilimo ndiyo hiyo asilimia 26 ambayo kama inaleta pato la asilimia 26 halafu unawekeza asilimia 0.93 maana yake hatukitendei haki kilimo. Kwa hiyo, ni rai yangu na ombi langu kwa Serikali mwakanii mnapoleta bajeti ya kilimo, leteni bajeti iliyojaa ili itusaidie.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mliosimama naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge, mnapiga kelele sana. Yaani hapa mbele mimi huletewa malalamiko lakini huwa sipendi sana kuwaambia keleleni kwa sababu watu wanaskilliza. Watu wamekuja hapa Bungeni kujifunza. Sasa siyo jambo zuri mtu aliyeko hapa mbele kila wakati akawa anasema keleleni, keleleni, keleleni. Tujizue kuongea kwa sauti kama huko nje. Pia huyo anayechangia hapa, wewe msikilize ili hoja yake uielewe, siku nyininge kwenye Kamati yako labda itakusaidia, siyo kwamba akiwa anachangia mwingine, basi wewe uendelee na mambo yako, hapana. Uko hapa kama Mbunge ukiishauri na kuisimamia Serikali. Kila mmoja atimize wajibu wake. (*Makofi*)

Sasa wakati nazungumza hilo niwakumbushe, ukiacha Waziri wa Fedha ambaye anaongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo ya msingi kabisa, Waheshimiwa Wabunge kuna ambaao mnaenda kwenye Kiti kile pale mnakaa nusu saa. Waziri Mkuu atasikilliza saa ngapi hoja za Wabunge na yeye ndiyo msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni?

Kwa hiyo, tafadhalii. Sasa hivi nikiona mtu pale amekaa muda mrefu, nitakunyanyua. Nadhani tumeelewana vizuri. Mheshimiwa Spika, alishaeleza hilo, nadhani hatujalitilia mkazo sisi wasaidizi wake, sasa tutaanza kuona mifano leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena. Nilikuwa nasisitiza tu kuwaomba Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo wanapoleta bajeti ya kilimo mwakani, basi waongeze fungu la bajeti ya kilimo kwa kuwa kilimo kinachangia pato la Taifa kwa asilimia 26 na kinachangia chakula kwa asilimia 100. Sasa ukilinganisha bajeti yetu hii ya kilimo ya 0.9 percent haioneshi kwamba tunakwenda kukifanyia kilimo yale mabadiliko ambayo tunayahitaji. Kwa hiyo, ni maombi yangu sana kwa Serikali hii ya CCM Sikivu, kwenye hili mlibebe kwa ajili ya bajeti ya mwakani, mlifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana bajeti hii. Tarehe 31 ya mwezi wa 12 mwaka 2020, watu wa *TRA* waliandika barua kipeleka kwenye vyama vyetu, kwa Wakuu wa Mikoa wakitaka wakulima watoe tozo kwenye korosho ya *Income Tax* ya 30 percent. Sasa kwa sababu Wizara imekwishatoa maelekezo na wanaopaswa kulipa *Income Tax* pato lao ni lazima lianzie shilingi 270,000/= na kuendelea, ukifanya overall ya wakulima wa korosho wote, kwa maelezo ya Wizara kupitia Naibu Waziri Mheshimiwa Bashe, mkulima wa kawaida anazalisha shilingi 1,400,000/= kwa mwaka. Maana yake pato la kawaida kwa mwezi halizidi hata shilingi 120,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Fedha liambie *TRA*, wakulima hawa ambao wanachangia *Export Levy* kama korosho inakuwa shilingi 3,000/=, 15 percent *Export Levy* ni shilingi 400/= na kidogo. Ukijumlahisha na cess shilingi 50/=, mkulima huyu anachangia zaidi ya shilingi 506/=.

Sasa unapokaa ukawataka wakulima tena walipe *Income Tax* hii ni kutaka kuigombanisha Serikali na Chama cha Mapinduzi ambacho kinaongoza dola, kwa sababu hawa ni watu ambao ni wa chini sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana Wizara ya Fedha na Msaidizi wako, mwaambie watu wa Mamlaka ya Mapato maana ninanyo hapa barua waliyoandika tarehe 31 kutaka wakulima walipe *Income Tax*; mwaambie wakulima hawa pato lao haliwafanyi wao kulipa

Income Tax. Kwa hiyo, nawaomba sana. Hawa wakulima kuna tozo nyingi ambazo wanapita kulipia bila hii ambayo mnataka kuwatoza tena. Kwa hiyo, mtoe maagizo kwa *TRA* waiondoe hii kitu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kwa Wizara, nimeona mnaleta Miswada ya Sheria ya Fedha hapa, ile *Export Levy* tunayoiomba ambayo 2017 tuliondoa kifungu kile Na. 17(a) tunaomba mnapoleta Mabadiliko ya Sheria ya Fedha, kwa sababu na yenyewe iko ndani ya Mabadiliko ya Sheria ya Fedha, basi na ile muiletete tena ili tuirudishe *Export Levy* wale watu wa *CIDTF* wapate fedha ili kwenye korosho mpunguze mzigo wa haya mambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu walishagusia hapa mambo ya Madiwani. Naiomba Wizara, wakati mnajandaa kufanya maboresho ya mambo haya, hata ile posho kama mnaweza, bajeti ya mwakani itawaruhusu vizuri, basi mwongeze posho ya Madiwani, *at least* wao ndio wanafanya kazi kubwa na ndio wasaidizi wetu kule chini wakati wote tunapokuwa tuko kwenye shughuli zetu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena Wizara ya Fedha kama itawapendeza, wenzangu wamesema sana, zile fedha ambazo mmesema kuwapa wale watendaji wetu wa Kata, basi ikiwezekana mztroe moja kwa moja na kama hamna hiso fedha, mwandike waraka kwa Wakurugenzi. Wakurugenzi hawa na Watendaji wetu wa Kata; Mtendaji wa Kata hawezikwenda kwa Mkurugenzi kumwombwa hiyo shilingi 100,000/=. Hata ingepita miezi mitano hajapewa, hawezikwenda kumwombwa. Fuatilieni mifano rahisi sana kwenye ofisi hizi za ma-*DC*, Maafisa Tarafa hiso posho walishakaa na Mheshimiwa Rais Marehemu Dkt. Magufuli lakini hiso posho bado hawapati kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana, mnapokwenda kutekeleza hii sheria mbayo mmetaka wapewe posho hizi la shilingi 100,000/=, basi ikiwapendeza Wizara ya Fedha mzipeleke ninyi wenyewe moja kwa moja ili

kuondoa *conflict* baina ya Watendaji wa Kata na Wakurugenzi na mara nyingi Wakurugenzi wanaweza wasiwepe kabisa kwa sababu tunajua hali za Halmashauri zetu. Wakati mwingine wanafanya bila kukusudia kwa sababu mapato yao na makusanyo yao siyo mazuri. Nawaombeni sana kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuomba, kilio cha Wenyeviti wetu wa Serikali ya Vijiji kwa kweli kimekuwa kikubwa sana. Hata hiyo posho ndogo ya shilingi 10,000/= ambayo baadhi ya maeneo wanasema wapewe, unaweza ukashangaa miezi minane hajapata hata shilingi 10,000/= moja. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara, kama itawapendeza hawa Wenyeviti wetu wa Serikali za Vijiji nao mwaandalie posho, siyo hii shilingi 10,000/=; mtakayoona inafanana na maisha ya sasa ili wafanye kazi zao kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo ajiandae.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nami kupewa nafasi hii adhimu kabisa kwa ajili ya kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza nami nianze kumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa upendo wake mkubwa na usikivu mkubwa ambao ameuonesha kwa sisi Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla. Namshukuru kwa sababu ya yale ambayo tayari wenzangu wameshayazungumza kwa kupewa zile shilingi milioni 500 kwenye Majimbo yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Rais kupitia Waziri wake wa TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambapo Wabunge tumeelekezwa kwamba tupeleke mapendelekezo ya eneo gani tutapenda shule zetu zijengwe

angalau shule moja ya Kata. Hii inanifanya niendelee kuamini misemo mingi ambayo imekuwa ikitsemwa na majukwaa mengi ya Kimataifa, hata *World Economic Forum* wakati fulani walisema, nanukuu: "*Having women in leadership roles is more important now than ever.*"

Nikiendelea kunukuu makala moja iliyoandikwa na mama mmoja anaitwa Lynn Camp ambaye ni *CEO* wa *EVERGREEN*, hawa wanajihuisha na biashara za mitando na digitali, anasema: "*Women led Government is taking bigger steps forward on behalf of the state economy, they have shown the real desire to listen to experts in wider world of business.*" (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kunukuu anasema: "*the survival of planet requires new thinking and strategies we are in the pitched battle between the present array of resources and the attitude and the future struggling to be born. Women get it, young get it, they are creating a whole different mindset.*" Sasa ukisoma hizi nukuu zote zinaonesha huko tunakoelekeea sasa akina mama pamoja na vijana wanachukua nafasi. Inaonekana kwamba wameleta mchango mkubwa sana katika kufikiri na kuleta mikakati mipyä ambayo itakwenda kukuza uchumi wetu kama nchi na biashara za dunia kwa ujumla. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, hata *Deloitte and Tosh* walisema kwamba; *companies led by women in leadership they have six times innovative than other companies and also, they meet financial targets two times.* Kwa hiyo, wakimaanisha kwamba kampuni ambazo zinaongozwa na akina mama inaonekana zina ubunifu mara sita dhidi ya kampuni nyingine ambazo zinaongozwa na akina baba. Kwa hiyo, kwa kweli namshukuru sana Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na hilo nitumie nafasi yangu ya Kibunge kuishauri Serikali na kumshauri Mheshimiwa Mama Samia, kwa kuwa sasa imeonesha kwamba mwelekeo sasa katika uongozi wanawake na vijana sasa wanachukua hatamu, nilikuwa napendekeza kwamba

hata katika miradi mikubwa ambayo tunafanya sasa, tuanze sasa kutaja wanawake ambao walileta mchango mkubwa kwenye Taifa hili...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda nimpe Mheshimiwa Kiswaga taarifa. Nampongeza sana kwa jinsi anavyotambua kwamba wanawake na vijana watachukua hatamu. Kwa maana hiyo, mwaka 2025 ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Mama Tendega atakuja kwa Jimbo la Kalenga. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo ina utata kwa sababu Jimbo lile la Kalenga lilitawaliwa na Chifu Mkwawa. Kwa hiyo... (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga, sina hakika kama hii ilikuwa ni taarifa, lakini malizia mchango wako. (*Kicheko*)

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa hiyo, nimesema kwamba tuwe na maeneo sasa ambayo yanatajwa kwa ajili ya akina mama. Kwa mfano, wako akina mama ambao walileta michango mikubwa katika Taifa hili kama akina Mheshimiwa Gertrude Mongella na Mheshimiwa Anne Makinda. Tunaweza hata tukajenga hospitali fulani ya akina mama tukaiita Anne Makinda au Gertrude Mongella. Tunafanya hivyo ili ku-*inspire* vijana wengi wa kike. Hata mimi nina binti ambaye ninatamani aje awe mtu mkuu sana. Kwa hiyo, wakianza kuona waliotangulia wanahesimiwa, basi na wengine watafuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bajeti hii ina mambo mengi sana mazuri ambayo nimeyaona yametajwa humu. Moja ya jambo muhimu sana ambalo nimeliona ni lile la kuwa na sensa. Ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu, kuwa na *data* muhimu kwa wakati. Unajua katika mipango mingi ya maendeleo duniani inategemea sana takwimu. Unaweza ukasema kwamba tunahitaji shule 10 katika Jimbo la Kalenga; kwa sababu ya takwimu tulizonazo ambazo siyo za kweli, kumbe takwimu halisi zinataka tujenge shule 20. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kutenga bajeti karibu shilingi bilioni 328 kwa ajili ya kufanya sensa mwakani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na msaidizi wake na pia pamoja na Mwenyekiti ambaye ni jirani yangu hapa kwa kuchambua bajeti vizuri na kuzingatia mawazo mengi ya Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii kuna mambo mengine ambayo tunataka tuchangie kidogo labda kwa kuboresha. Kama nilivyosema mimi nimekuwa kwenye mitandao miaka mingi; kwenye hii kodi ambayo tumeianzisha kwenye mitandao hasa kwenye laini za simu, tumesema tuna-charge katika shillingi 10/= mpaka shillingi 200/= kwa siku. Ukweli ni kwamba ukiangalia kwenye watumiaji wa simu, asilimia 65 ya wateja wao, wengi wana-charge kwa mwezi shillingi 500/. Asilimia 59 mpaka 65 wanaweka shillingi 500/= kwa mwezi. Sasa ukisema kwamba uta-charge kila siku shillingi 10/=, maana yake unasema shillingi 300/. Kwa hiyo, maana yake kuna kundi kubwa ambalo linakwenda kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pengine kuna shida kwenye uchapishaji, tuseme kwamba labda tuna-charge shillingi 10/= kwa kadri mtu anavyoweka fedha. Tukiangalia pia kwenye ile miamala, tumesema kwamba tuta-charge katika ya shillingi 10/= mpaka shillingi 10,000/=. Ukiangalia muamala wa juu kwa mfano shillingi 1,000,000/= tuna-charge shillingi 8,000/=. Hili limeleta malalamiko sana wakati hivi viwango vinapandishwa kwa wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilikuwa nafikiri Serikali ione uwezekano. Kodi tunaitaka kwa sababu tunataka kufanya mambo mengi na mama ameshaonesha njia kwamba tunataka kufanya *transformation* kwenye uchumi. Ingekupendeza ungekaa na watu wenyewe mitandao wakupe uhalisia wa hili jambo, kwa sababu tukiongeza shilingi 10,000/= kwenye shilingi 1,000,000/= inakuwa shilingi 18,000,000/=.

(*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa mfano *Airtel*, imechukua muda mrefu sana kufanya miamala ya bure ili angalau kuchochea watu wengi waweze kufanya hiyo miamala. Wamechukua muda mrefu sana. Sasa leo tukisema tunaongeza kwenye shilingi 10,000/= inaweza ika-*slow down* na hiyo kodi ambayo tunategemea kuipata tusiweze kuipata. Kwa hiyo, hili ninaomba pia tukaliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye mambo ya kodi yanayohusiana na ardhi, kuna viwanja ambavyo vimepimwa vingi na Watanzania wengi hawalipi. Tunakushukuru umesema kwamba kwenye *Property Tax* tutaweka kwenye Luku. Watu wengi wamechangia hapa, najua utapata hekima ya namna gani utaweza ku-*charge* kama mtu ana kiwanja, ana nyumba nyingi ana Luku nyingi, hiyo hekima Mungu atawaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo hili lingine la viwanja, watu wengi sana hawalipi kwenye *land rent*, na huko tuangalie tutafanya nini? Kwa sababu kuna kodi nyingi huku zimelala na zinaweza kusaidia sana uchumi wetu na tukafanya mambo mengi ya kimaendeleo. Kwa hiyo, hilo nalo tunaweza tukatengeneza *task force* ambayo itakwenda kusaidia kukusanya hizi kodi, vyovyote mtakavyoona inafaa naomba tuweze kutupia jicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine ambalo nilikuwa nalifkiria, huko tuendako uchumi mwingu utatoka kwenye kilimo. Sasa ningeomba kwamba, mkakati kwenye kilimo uwe namna hii kwamba, tumekuwa tuki-*acquire* ardhi kuwapa wawekezaji, sipendi hilo jambo la

kuchukua ardhi kwa wananchi kuwapa wawekezaji; napenda hivi kwamba, tuwe na ardhi kwa ajili ya uwekezaji kama walivyofanya Dubai wanasesma *land for equity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija pale Iringa kwangu, nina eka zangu 2,000 sijaziendeleza, Chalamila ana eka 2,000 hajaziendeleza, Mkoa naye 5,000 hajaziendeleza, tunazitambua zile eka kwa pamoja tunasema eneo hili lina eka 20,000 wanaomiliki hapa ni Mheshimiwa Kiswaga, ni Mkwawa, ni fulani. Muwekezaji aje awekeze pale na tumeshaianisha ardhi, lakini sisi tuchukue asimilia 20 ya uwekezaji. Akae miaka 33, miaka mingapi, lakini sisi tuwe na hisa kutokana na ardhi tuliyonayo na ye ye anakuja na pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana Dubai leo watu wamekuwa matajiri kwa sababu walikuwa na ardhi. Hili suala la kuichukua ardhi tuwape wawekezaji linaleta shida, unakuta kwamba, muwekezaji anakwenda kwenye kijiji anapewa eka labda 500 eti kwa sababu amejenga ofisi ya vyumba vivili. Baada ya hapo mnakwenda kumuomba pesa ya maendeleo 500/= tu, labda 100,000/=, anasema mpaka muandike barua, hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ile ardhi kijiji kingeamua kushirikiana naye kwamba, wewe njoo wekeza katika eka hizi 500 tunakupa, lakini katika mazao utakayopata utupatie sisi asilimia 20 kwa miaka yote, sisi tutakuwa na uchumi wetu kama kijiji na hatutakuwa na tatizo tena la kwenda kuombaomba. Tukiacha hili jambo ardhi yetu itapotea na Watanzania hawatakuwa na ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. ninaunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, naanza na kauli ya Waziri wa Nishati alipotoa kauli kuwa nchi nzima umeme utakuwa ni 27,000/= lakini kwa llala hiyo bei hakuna. Jiulize kwa nini llala itozwe laki tatu, laki nne, kuunganisha umeme, lakini nchi nzima mikoa yote ambayo Mwanza, Arusha, wanalipa bei ya chini zaidi ya llala; tatizo liko wapi na kwa nini kuna *formula* kama hiyo kwa kuletewa watu wa wilaya hii yetu ya llala? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ada ya tozo ya *fire*. Tulitoa taarifa yetu ndani ya Bunge kuwa ni kubwa mno, sio kwa mjini tu maeneo yote nchini, tozo ya ada ya *fire* kwa majumba ya ghorofa ni zaidi ya 250,000 kwa mwaka, ni kubwa zaidi ya kodi ya majengo, kitu ambacho wananchi hawawezi. Tulikubaliana itolewe na ipunguzwe isiwe 250,000 ishuke mpaka 10,000 kwa mwaka kutokana na *extraction* ambazo hawa watu wa *fire* wanafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye mitandao ya simu. Kuna mambo mengi yanazungumzwa kwenye mitandao, kuna kashfa nyingi zinapitishwa kwenye mitandao, kuna taarifa nyingi ambazo si za ukweli ziko kwenye mitandao kuhusu gharama na ada mpya ambayo Serikali na kodi inaitaka kwenye simu nchini mwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina watu zaidi ya milioni 55. Walipaji kodi kwenye nchi hii hawafiki milioni tano, hawa milioni tano kwa kweli, kodi wanayolipa wao inaweza ikabeba maendeleo ya nchi hii kwa watu milioni 50? Haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujitoe muhanga, lazima tukubaliane na mabadiliko ya nchi yanavyokwenda. Yesu Kristu kipindi chake na kwenye kitabu alichokujanacho alisema ya Kaisari yaende kwa Kaisari na ya Mungu yaende kwa Mungu. Mtume Muhamad (SAW) na kwa waislamu alianzisha vita na mataifa ya kiarabu kwa kutokutaka kutoa zakaa. Unachukua kwa mwenye nacho unampa asiyekuanacho. Leo wananchi wanalilia barabara,

wanataka maji, wanataka elimu, wanataka bima za afya, pesa zinatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe wananchi huu utaratibu wa kwenye mitandao wa kutoa maneno ya kashfa, kutukana viongozi, kitu ambacho mnashindwa kuelewa kila uki-post tangazo lako la matusi au tangazo la kashfa ujue unalipa kodi. Kila ukutukana, kila uki-post, elewa unalipa kodi hiyo ndio nia yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameweke vizuri sana kwenye miamala hii kodi hii ya simu ameweke kuanzia 10 mpaka 200. Hebu tuchukue kwa wale ambao watalipa 20 kwa siku, 20 tu ambayo ni 600 kwa mwezi kwa watu milioni 30 ni bilioni 216. Tumejaribu kupanua wigo wa kodi hata yule mwananchi wa kawaida naye awe na mchango wa barabara, awe na mchango wa bima, awe na mchango wa masuala ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema vijana wengi wako katika mitandao vijana hawa wazazi wao wanataka kwenda hospitali. Vijana hawa Ndugu zao wanataka kwenda kujifungua. Vijana hawa wanataka bima kwa wote. Vijana hawa wana wazazi wao wagonjwa. Vijana msipotoshwe na taarifa ambazo zinatolewa ambazo hazina ukweli. Sasa mtu kama mimi nillyekubuhu hata nikipigwa madongo sijali, wala siogopi, sababu najua wananchi wanataka maendeleo. Maendeleo yatakuja na kodi. Isipokuwa Waziri wa Fedha, nikuombe, ada hizi za simu, kodi hii maalum ambayo Wabunge wote tumekekubaliana, lazima *ui-ring fence*; inakwenda kwenye maji, inakwenda kwenye barabara, inakwenda kwenye bima kwa wote, isiwe pesa hii inatumika kwenye posho, isiwe pesa hii inatumika kwenye semina, isiwe pesa hii inatumika kwenye mambo ambayo hayana tija kwa ... (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais, Mama Samia Mama yetu, amempa kila Mbunge milioni 500 kwa jimbo. Kila shule, kila kata isiyokuwa na sekondari,

nampongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa TAMISEMI, leo ametutangazia kila kata isiyokuwa na sekondari milioni 600 wanapewa. Hizi hela zitatoka wapi kama sio kodi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na tuna uwezo wa kulipa hizi kodi kwa kiwango cha kila mtu. Yule mwenye uwezo mkubwa atalipa kodi kubwa, *the rich will pay more, the rich will be taxed more and taxes are collected they are not paid; kodi inachukuliwa hailipwi.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watu tujiandae na mabadiliko ya kufunga mikanda kusaidia Taifa letu liende mbele. Tuna miradi ya *SGR* inataka hela, tuna miradi ya bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere linataka hela, tuna miradi mipya ambayo Serikali inataka hela kwa hiyo, lazima tulipe kodi tupate hela. Kuna barabara za vijijini, tunataka mazao ya wakulima yafike kwenye masoko kwa uhakika, kuna maeneo ambayo barabara hazipitiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wa llala ndio walionitura, nawazungumzia wao, najua hawa wote wanaoponda ponda kwenye mitandao hawakai llala, wao wanakaa Kivule, Bombambilii, sijui Majimatiitu, sisi watu wa llala tunataka maendeleo. Tunataka barabara, tunataka miundombinu ya mifereji, tunataka lami kwenye majimbo yetu ya mjini tuweze kuchangia pesa za kutosha tusaidie majimbo ambayo hayana uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo llala tunakusanya 1,100,000,000 kwenye ada ya ku-park magari. *Parking* za magari kwenye Wilaya ya llala *one billion* kwa mwezi Mheshimiwa Waziri na hizi pesa wala haziji kwetu zinakwenda kusaidia maeneo mengine. Sasa tuboreshe maeneo yetu ya mjini, ili tuweze kusaidia... (*Makofi*)

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zungu kuna Taarifa.

TAARIFA

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Zungu kwamba, kodi hii ya simu imejibu kilio cha muda mrefu cha Watanzania cha kutaka kila Mtanzania aliye kodi kwa usawa. Kwa hiyo, kodi hii ya simu Wabunge tunalipa, viongozi wakubwa wanalipa, mpaka mtu wa chini analipa kwa usawa. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nadhani uli...

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa. Na kulingana na matumizi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hakuna mtu anaandikiwa barua, leo hakuna mtu ananunua *stamp*, leo hakuna mtu anakwenda posta. Leo sio lazima ukamtembelee Ndugu yako kulipa nauli ya 2,000 ya nauli ya basi, unapiga simu unazungumza naye, watu hawayaoni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo uko Mwanza unauliza bei ya soko ya ng'ombe Pugu, huna haja ya kumtuma mtu aje Pugu unauliza kwenye simu kwa hiyo, simu hizi ni chocheo kubwa la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Serikali kuanzisha kodi hii, isipokuwa matumizi ya pesa hizi yalindwe yasiende kutumika kwenye maeneo ambayo hayastahiki kutumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali ina mpango wa bima kwa wote. Wananchi wetu wanalamika dawa hakuna, wananchi wanalamika wanakwenda kujifungua maisha magumu, wananchi wanalamika huduma za hospitali zinapungua. Kwa ada hii na pesa hizi ambazo tutazipata ndio kimbilio la wananchi wetu kupata maisha bora. Ndio kimbilio la uzazi salama kwa mama zetu. Ndio kimbilio la lishe salama kwa mama zetu. Tukubaliane, tusaidiane, tuunge mkono jitihada za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaokataa kodi hii wanataka kuirudisha nyuma Serikali hii, hilo hatutakubali. Hatutakubali kurudi nyuma tunakwenda mbele, mbele kwa mbele. Tumetoka katika matatizo makubwa sana ya kutokuwa na mapato, sasa tunaanza vyanzo vipyta, lipa kodi yako ya simu, tumia simu yako unavyopenda ukitumia kidogo utalipa kidogo ukitumia sana utalipa sana wala halina mjadala. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao sasa hivi kuna *tools* za kujua *every user* kwa kila mtu wa mtandao wa simu. Kwa hiyo, wale ambao mapato yao ni madogo watalipa kidogo, lakini wanachangia Taifa lao kwenye maendeleo ya barabara. Atatoka Kivule, Bombambilili, atakuja mjini mapema, atakaa Tabata atakuja mjini mapema sababu barabara ni safi za lami kwa hiyo, tuungane na Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena na wale wanaoendelea ...

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, mmanipotezea muda sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zungu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tarimba.

TAARIFA

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimpe Taarifa Mheshimiwa Zungu kwamba, kodi hii kwa Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza, hata Marekani wanatoza kodi kama hii, hivyo, Watanzania wasipate wasiwasi kwamba, sisi tumejitengenezea kodi ambayo ya kumuumiza, bali inachukua *at least 19%* ya *consumer bills* katika nchi ya Marekani hivyo Watanzania... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ongea Kiswahili, hatujaelewa hapo ulipoongea kингereza, ongea Kiswahili.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui tafsiri ya *consumer bills*. Natoka Kinondoni na sijui.

NAIBU SPIKA: Sasa kama wewe hujui na ndio mnasema Kiswahili kifundishwe Watanzania...

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, *consumer bills* ni gharama za matumizi ambayo ni karibu asilimia 19 ya wamarekani wanalipa kodi hii. Hivyo, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuweza kulipa kodi kama hii, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sasa hebu ngoja Taarifa yako tuielewe vizuri, samahani Mheshimiwa Zungu. Kule wanalipa asilimia 19 hapa tutalipa asilimia ngapi?

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, hizo asilimia 19 ni gharama nzima za matumizi ya wananchi wa Marekani katika *utilities*. Inaonekana ni asilimia 19 imo katika kodi kama hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zungu, malizia mchango wako.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nakubali Taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo sasahivi Mkoa wa Dar es Salaam wanataka kuzitengeneza ni zaidi ya bilioni 700. Na hizi pesa zinataka zilipwe, hizi pesa zinakopwa, hizi pesa zinakuja kwa niaba ya Serikali yetu ambayo inasifikasi kwa kulipa madeni yake na lazima tuchangie tulipe deni hili ili barabara zetu ziweze kuboreka, ili miundombinu ifurahishe na watu waweze kutembea na waweze kupata huduma bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Narudia kusema wanaoendelea kutukana kwenye mitandao mnalipa kodi mjue hivyo. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji kwenye bajeti ya Serikali. Nitajielekeza sana kwenye namna ya kuonesha mikakati ya upatikanaji wa fedha, lakini pia nitatoa ushauri kwenye namna bora ya kuweka matumizi yaliyo sahihi, ili walipa kodi waweze kujiona wanachokifanya kina tija katika maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza kwenda katika maeneo hayo nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa bajeti hii nzuri na kubwa ambayo wametuletea. Na ninafurahi sana kuwa mionganii kwenye bajeti inayosifiwa kwa sababu, hata Wabunge wazoefu waliosimama wanakiri kwa maneno yao hii ni bajeti ya kwanza yenye faraja kubwa kwa wananchi. Hivyo, najisikia faraja sana mimi, kama Mbunge mgeni jimboni kwenye Bunge hili, kuwa sehemu ya mtu ambaye nasifiwa kupokea bajeti yenye tija ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya maneno hayo niitumie nafasi hii kuieleza Serikali, kwenye michango yangu ya awali nilipokuwa natoa nilizungumza sana suala la namna bora ya kuwapanga watumiaji wa ardhi, kwa maana ya wakulima na wafugaji katika maeneo mazuri ili kuweza kuongeza vipato vyao waweze kuweza kuisaidia Serikali yao kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nitumie kidogo muda mfupi kuifahamisha Serikali jimboni kwangu juzi kumetokea tukio la Afisa Kilimo

kushambuliwa na mfugaji eti kwa sababu, Afisa Kilimo huyu alikuwa anakwenda kuangalia maeneo ambayo wakulima wameliwa mazao yao, imesikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii kumpa pole Afisa Kilimo huyu na kumtia moyo huko aliko aendeleee kuchapa kazi kwani Watanzania wana lengo la kuzalisha. Lakini pamoja na hayo niwaombe viongozi wa Kata ile ya Ruvu kwenye kijiji kile cha Ruvu *Station*, waendelee kuwaasa Watanzania wananchi wa eneo lao wawe na amani kwani Serikali yao itachukua hatua stahili kwa wakosaji na wala wasiji-organise kufanya mambo ambayo yatavunja sheria ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo mchango wangu wa kwanza nataka nijielekeze kwenye mapato ya ndani, hasa yanayohusiana na masuala ya halmashauri, halmashauri zetu zimekuwa na vyanzo vingi vya mapato na ni mjambe wa Kamati ya Utawala wa Serikali za Mitaa. Tulipokuwa tunapitia bajeti zao Halmashauri nyingi nchini hawana vyanzo vipya, vyanzo vyao ni vile walivyozowea siku zote, inaonekana kuna tatizo labda kwenye ubunifu wa vyanzo vipya.

Niombe Serikali ifike sehemu ikiwezekana iwe inafanya vikao na timu za halmashauri wawasadie kuwaonesha njia na mipango mbalimbali ya kuanzisha vyanzo vipya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimegundu kwenye zile taarifa zao mapato mengi ambayo wanayakusanya hawafikii malengo. Na hawafikii malengo nikiangalia inawezekana ni kutokana na kukosa wataalam wanaofahamu ukusanyaji wa mapato. mapato mengi wameyakabidhi kwa watendaji wa vijiji, mapato mengi wameyakabidhi kwa watendaji wa kata, watu ambaa tunaamini wana majukumu mengine makubwa wanayoyafanya kwenye maeneo yao. kwa hiyo, ningiombaa Serikali ifanye utaratibu ikiwezekana, ili iweze kusaidia kukuza mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukikuza mapato ya halmashauri maana yake unakuza pia pato la uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, ni vizuri zaidi ikiwezekana tunapoitazama *TRA* kwenye *level* ya kitaifa tufikirie namna bora ya kuangalia chombo kitakachosimamia mapato ya halmashauri. Kwa sababu, mapato yale yanakusanywa katika mazingira ambayo unaona kabisa kwamba, wakusanyaji inawezekana wanakosa *skills* za ukusanyaji. Sasa ningeshauri sana Serikali iangalie eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa tukumbuke tu kwenye miaka kdhaa ya nyuma kwenye *level* za chini za Serikali za Vijiiji na Kata kulikuwa na watu wanaitwa *Revenue Collectors*. Watu ambaao walikuwa anafanya kazi ya ukusanyaji wa mapato na takwimu ya mapato yale ilikuwa inatunzwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi kwamba, hawa watendaji wa vijiji na kata wanashindwa kufanya au hawana uwezo wa kufanya, lakini najaribu kuyaangalia majukumu yao, wana majukumu ya kusimamia migogoro ya ardhi, wana majukumu ya kuhakikisha wanasimamia majengo, wana kazi ya kuhakikisha kwamba, wageni wanapokuja, Wabunge wanapofanya ziara na wao wapo. Ni muda gani mzuri watapata wa kusimamia mapato katika muda wao wote? Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikajielekeza kuangalia mapato mengi ya halmashauri inawezekana yanapotea kwa sababu chombo kinachokusanya mapato hayo kinakosa uwezo wa kukaa muda wote kusimamia mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala zima kwa wawekezaji. Tukiangalia utaratibu wa nchi yetu na sheria zetu wawekezaji wengi ambaao tunawategemea labda wanaweza kuja *boost* maisha yetu au kipato chetu cha nchi tunatazama sana watu wa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kukiwekwa sera nzuri, kukiwa na utaratibu mzuri wa kuhamasisha wananchi wa ndani, ili waweze kuwekeza kwenye maeneo haya

ambayo wanawekeza wenzetu kuna uwezekano kukawa na kiwango kikubwa sana cha upatikanaji. Cha msingi hapa Serikali itengeneze mazingira rafiki ya kuwafanya watu waweze kuwekeza na wanapowekeza ndipo watakapoweza kusababisha Serikali ipate fedha kwa sababu watalipa kodi na watafanya shughuli nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo nizungumzie jambo moja la mfano katika maeneo haya; tumeona Serikali imeweza kuanzisha, TAMISEMI, wameanzisha miradi ya kimkakati. Tangu ianzishwe hii miradi ya kimkakati kwenye nchi hii ni miradi 38 tu ambayo ndio imetimiza sifa, lakini katika miradi hiyo ni miradi sita tu ndio imetekelezwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nizungumzie jambo moja la mfano katika maeneo hayo tumeona Serikali - TAMISEMI imeweza kuanzisha miradi ya kimkakati, tangu waanzie hii miradi ya kimkakati kwenye nchi hii ni miradi 38 tu ambayo ndio imetimiza sifa, lakini katika miradi hiyo ni miradi sita tu ndio imetekelezwa imekamilika. Kwa maana nyingine ni nini pamoja na Serikali ilikuwa ina wazo jema la kuhakikisha kwamba Halmashauri inakuwa na miradi ya kimkakati kuongeza mapato lakini inaonekana fungu la Serikali kwenye kuifanya miradi iliyopitishwa kutekelezwa ni dogo, ningeishauri Serikali ikae chini na mabenki badala ya Serikali wao kupeleka fedha kwenye ile miradi ya kimkakati wawaunganishe na Halmashauri zile, wao Serikali kuu wawe madhamana wa hizo Halmashauri, hayo mabenki waziwezeshe hizo Halmashauri ambazo miradi yao imepitishwa iweze kutekelezwa kwa sababu inavyotekelizwa ni kweli kwamba kipato kitaongezeka na watu wale wataendelea kuhakikisha kwamba wanaingiza mapato ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili ninalotaka kuchangia kwa leo ni namna bora ya kutunza matumizi, na matumizi haya yatumike kwa ubora wake ili fedha ziende na ninazungumza hapa kwa kupitia *document* moja tu ya Mkaguzi wa Serikali. Mkaguzi wa Serikali alipokuwa anafanya

ukaguzi kwenye mradi wetu wa mwendo kasi kipande cha kutoka Dara es Salaam mpaka Morogoro inaonesha tu kwa kushindwa kuwalipa wakandarasi kwa wakati Serikali imetumia sio chini ya milioni 11.2 kuwalipa kama adhabu ya kuchelewesha kuwalipa wakandarasi kwa wakati, sasa niwaombe Serikali ni vizuri tukawalipa wakandarasi hawa kwa wakati ili tukaepusha fedha ambazo tunalipa kama adhabu ili hizo fedha zifanya shughuli nyingine, tukifanya hivi hata hii mikakati mikubwa iliyowekwa hapa ya ukusanyaji wa kodi fedha hizo zinaweza zikaenda kwa wakati kwenye maeneo yanayokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sambamba na hilo kwa maana hiyo sasa ni vizuri sana tukatengeneza utaratibu mzuri na tukaisimamia sheria yetu vizuri wenyewe tukaji-*control* kwenye matumizi. Wabunge wengi hapa wamepongeza juu ya uanzishwaji wa kodi ya kwenye simu lakini wamesema pia ni vizuri zaidi Serikali ikajielekeza kuhakikisha kwamba fedha hizo zinaelekezwa kwenye jambo ambalo limekusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini, kama kweli Watanzania hawa ninahakika kabisa kwa bajeti hii ya kwanza wakiona fedha zinazokatwa kwenye simu zao zimefanya kazi kwenye Majimbo yao kwenye barabara zao nina hakika hata mwakani tunaweza tukawaeleza tofauti na tulivyowaeleza mwaka huu na wakaridhika kutoa michango hiyo pasipo tatizo lolote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nilieleze ndugu zangu, tulitazame kwenye imani zetu za dini, nani anamlazimisha mtu kutoa sadaka, wanatoa sadaka kwa moyo kwasababu wanaamini wanachokifanya wanakifanya kwa sababu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu anataka wafanya hivyo, na wanafanya wanaona yale majukumu na ukiangalia kwenye zile sadaka zinazotolewa Makanisani na Misikitini wala hakuna *auditor* anayekagua kule na watu wanaridhika na wanaendelea kutoa siku zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa serikali watafurahi sana Watanzania hawa wakiona barabara zinajengwa kweli watafurahi wakiona shule zinajengwa kweli, watafurahi wakiona maji yanatoka kwa uhakika, kwa hiyo na mimi naungana na wabunge wenzangu kuiomba Serikali fedha hizi fungeni mikanda na ninyi msizielekeze kwenye matumizi mengine, zielekezeni kwenye matumizi ambayo mmewatamanisha Watanzania waone kwamba ndiyo kitu kinachokwenda kufanyika na ninahakika Watanzania hawa wapo watu amba wanaweza kutoa kodi hizi pasipo lawama yoyote kama wataona yanayofanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu mara baada ya bajeti ile kusomwa nimepokea meseji, nimepokea simu nyangi kutoka kwenye Jimbo langu watu wakipongeza na wananihauri wananiambia hebu sisitiza Serikali tuzione barabara zilitengenezwa kweli, wanasema hebu sisitiza Serikali tukiona huduma ya afya inatolewa kweli tutaweza kutoka kodi zaidi ya hivi na salamu hizi niseme zimetolewa kwa makundi tofauti na wengine ambao wamenitumia salamu hizo na kunipigia simu kunieleza wakitoa pongezi hizo katika hali ya kawaida kwa maisha tunayoishi kule sikutegemea kama wangkuwa sehemu ya watu wanaopongeza, kwa mazingira yetu tunayojua lakini wamepongeza kwa sababu wanaiamini Serikali yao na wana uhakika kinachokwenda kufanyika kitakuwa kikubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Festo Sanga ajiandae.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii nami nipate nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyonipatia kuweza kuzungumza tena siku ya leo katika bajeti hii kuu. Mwanzo kabisa niipongeze sana hotuba ya bajeti kuu iliyosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akimwakilisha Rais na mimi naunga mkono hoja hii kwanza kabla hata sijazungumza kwa sababu yapo mambo mengi mazuri yaliyooneshwa kwenye hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shabaha za uchumi zilizoelezwa kwenye hotuba tunayoizungumzia hapa ni kuongeza kasi ya ukuaji wa kiuchumi kutoka asilimia 4.7 tuliyokuwa nayo kwenda kwenye asilimia 5.6, lakini vilevile imeonesha wazi kwamba tunataka kwenda kwenye asilimia 6.3 mwaka 2023 lakini mfumuko wa bei tunataka uwe kati ya asilimia Tatu (3) na asilimia (5) kwa mwaka huu. Vilevile mapato ya ndani tunataka yaongezeka na mapato ya kodi tunataka yaongezeka sasa inaonekana kuna kazi kubwa sana ya kufanya kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mahsusini ambayo matarajio yetu makubwa ya ukusanyaji wa kodi hii yanatakiwa yawafikie nayo ni barabara za mijini na vijijini *TARURA*, kuna maji safi na salama, kuna bima kwa wote, kuna habari ya shule tunatakiwa tujenge shule, ukienda kwenye afya tu unaona kuna maboma ya zahanati karibu 8,000 yanahitaji kukamilishwa. Lakini ukienda kwenye vituo vyta afya hotuba hii inaonesha kuna vituo vyta afya zaidi ya 1,500 vinatakiwa kukamilishwa kwa hiyo ni dhahiri kwamba tunahitaji fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vyanzo vyetu vyta fedha ukiviangalia vyta mwaka jana na mwaka huu vimebadilika kidogo sana japokuwa inaonekana kuna hii tumezoea kusema *indirect tax*, hii kodi ya *LUKU* iliyoongezeka na inayotoka kwenye *LUKU* mwa maana ya majengo (*property tax*), lakini na hii nyingine iliyoongezeka kupitia kwenye mitandao ya simu kwa matumizi ya siku tulizonazo. Ukiona kuna Trillioni Mbili imeongezeka hapa lakini tukiangalia kwa uhalsia vyanzo vile ukiangalia kwa *percentage* tumeongeza

tu mapato ya ndani ya kodi kwa asilimia 72 vingine vimebaki kama vilivyokuwa tumepunguza kule kwenye mikopo ya ndani na ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja kubwa tuliyonayo ni ukusanyaji wa mapato, kwamba kazi kubwa tuliyonayo hapa ni ukusanyaji wa mapato lakini ukiangalia mikakati iliyowekwa kuna ile *EFD Management System*, kuna habari ya kuhakikisha kwamba ile *blue print* inatekelezeka na uwekezaji mwingine ambao tunauona kwenye maeneo hayo. Binafsi niishauri sana Serikali iongeze nguvu katika ukusanyaji wa kodi ni kweli tunesema tutakusanya kodi sahihi kwa sheria sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuongeze sana eneo hilo kwa sababu kama hatutakusanya kodi ya kutosha haya ambayo tunayaona leo kama hotuba nzuri sana tutakapokutana tena kujadili tutaanza kulaumiana sisi kwa sisi, kwa nini. Nina mfano mzuri wa mwaka jana, tulikuwa na hotuba ambayo inaonekana imeandikwa kama nilivyo sema inatofautiana kiasi na hii lakini nikienda kwenye kilimo, mfano kilimo tu *development budget* iliyotekelawa mwaka jana ilikuwa kama *30 percent* sasa tunataka kwenda mbele tunataka kuhakikishe kwamba tunakwenda kufanikiwa kusogeza uchumi kutoka asilimia 4.7 kwenda kwenye asilimia 5.6. Hoja ambayo ninaiona kwenye bajeti yetu hapa ambayo ningependa nitoe ushauri kwa Serikali zile sekta ambazo ni za uzalishaji kwenye bajeti hii hazina fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukiangalia *percent* ya hiyo Bilioni 294 ya kilimo kwenye *development budget* nzima utagundua ni 0.08 ambayo ni kama asilimia 0.8 haifika hata asilimia moja lakini hiyo inaa jiri watu asilimia 65 wa nchi hii na tunataka sasa twende mbele, kama mchango wenyewe ndio huo yaani unataka kitu fulani kitokee lakini *input* yako ni ndogo kiasi hicho maana yake hata hawa Mawaziri wa Kilimo tulionao watajitatihidi kadri wanavyoweza lakini hawataweza, kwa sababu hawana fedha ya kutosha wana mipango mingi tupate mbegu, wana

mipango mingi tuanzishe mashamba darasa, tuanzishe tulime Alizeti kwa fedha hii tuliyonayo Bilioni 294 ambayo haifiki hata asilimia moja haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tufikirie ninajua tayari bajeti ipo mezani tutakwenda kuitekeleza lakini matokeo yatakayokuja huko mbele hayawezi kuwa ya kushangaza sana, hatutasogea sana kwa sababu asilimia 65 ya watu ambao tunagemea tuwawezeshe hawataweza na bahati mbaya sana hata viwanda vinawezeshwa na uzalishaji wa kilimo, sasa kilimo hakijawezeshwa vyakutosha maana yake na viwanda havitafanya vizuri, kwa hiyo mwisho wa siku tutakapokuja kuzungumza hapa tutagundua hata hao tunaotaka kuwatoza kodi watakuwa wachache. Kwa mfano, Halmashauri nyingi nchini zinakusanya ushuru wa mapato kutoka kwenye mazao, sasa kama fedha iliyokwenda kwenye killimo ni kidogo tutakusanya nini kutoka kwenye Halmashauri? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawatakusanya sana watakwenda hapo hapo, mwaka huu tumeongeza Bilioni 200 kwenye malengo yetu Je, watazitoa wapi? Kwa sababu hatujachakata kuwaanzishia ili waweze kufanya uzalishaji mkubwa na tukusanye hivyo, vivyo hivyo kwenye uvuvi, vivyo hivyo kwenye mifugo, bado kile ambacho tumekitoa ni kidogo kwa hiyo tuangalie kile ambacho tunakiweka mahali kwa ajili ya kuzalisha, tukiweka kidogo tutapata kidogo na mwisho wa siku tuhakikishe kwamba *development budget* tunayoipeleka kule iende kama tulivyo *i-plan* mwaka kesho tutaanza kuulizana tulipanga iende asilimia 100 imekwenda asilimia 25 matokeo yake tutakuwa hatujafanya kazi kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sehemu ya pili ambayo nilitaka kuizungumzia eneo la madini, tunategemea madini yachangie tufike kwenye pato la Taifa asilimia 10, changamoto ambayo ninaiona sasa miundombinu tuliyonayo binafsi nimekuwa ninazungumzia barabara ya kutoka Geita kwenda Bukoli kupita Runguya kwenda Kahama, hii barabara inapita kwenye migodi, haipitiki sasa!

Kama haipitiki hiyo ndio hata makinikia yanayoulizwa humu ndani yanapita barabara hiyo, sasa tutakwendaje kufanya hii shughuli ambayo tunataka kufanya wakati miundombinu haipo? Lakini niseme...

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Magessa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

T A A R I F A

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nimpe taarifa mzungumzaji kwamba barabara hii inayotoka Geita - Bukoli, Bukoli - Kakola, Kakola-Kahama ni barabara ambayo kimsingi iliahidiwa kupewa kiasi cha dola milioni 40 na Mgodi wa Bulyanhulu, fedha hizo bado hazitolewa na Serikali sijui ni kwanini lakini pia barabara hii imekuwa ni adha toka makinikia yameanza kusafirishwa na magari haya yanayobeba makinikia yanatembea makundi kwa makundi gari zisizozidi 40 vumbi limekuwa ni kubwa sana, kwa ruhusa yako...

NAIBU SPIKA: Subiri kwanza unamuongezea mchango kwenye hoja ipi aliyokuwa anazungumza?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya barabara inayotoka Geita - Bukoli...

NAIBU SPIKA: Yeye alikuwa amemaliza kuzungumza hoja yake.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, alimaliza!

NAIBU SPIKA: Au wewe umeamua umalizie ili yeye asimalizie mchango wake?

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, alimaliza na nilitaka kumuongezea kwa sababu kwa ruhusa yako nimekuja na sampuli ya vumbi limo kwenye begi humu,

nilitaka uniruhusu niweze kumkabidhi ili aliachie humu vumbi aone namna gani wananchi wa Bulyanhulu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, kuna nyakati mtu anakuwa ana mtiririko fulani hivi wa mchango wake usimkatishe kabla hajaweka nukta, ukimkatisha maana yake kuna jambo labda anakosea unataka umrekebishe labda yeye kasema 10 kumbe ni tisa, sasa wewe unamkatisha ili wewe ndiyo useme vizuri jambo lake kabla Mbunge hajasema yeye hoja yake, yaani unakuwa kama unaonesha kwamba yeye hajaweza kumalizia hoja yake vizuri wewe ndiyo unataka umsaidie, sasa haikai vizuri kwa hiyo tusubiri awe anamaliza sentensi yake ndiyo wewe uingie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, mtu anayetaka kuchangia jamani sisi huwa tunawapa nafasi kama kwenye orodha haupo andika hapa mbele utapewa fursa ya kuchangia, ukimkatisha Mbunge mwenzio hizi zinakaa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kila tunachokizungumza humu ndani, sasa sisi wenyewe tuwekeane mazingira mazuri ya kuachiana nafasi za kuchangia kama hakuna jambo ambalo kweli unataka wewe kuchangia kwenye hiyo taarifa unayotaka kuitoa, maana nimeona wengi huwa unataka kuiseme barabara yako basi unasema hilo lilliloko huko na huku hivi hivi *ahaha!*

Mheshimiwa Magessa malizia mchango wako.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa hayo ambayo umeyasema. Niseme tu naendelea na hiyo barabara kwamba kumekuwa na mazungumzo ambayo umri wake ni zaidi ya miaka minne ya hiyo dola elfu 40 ambayo wadau kwa maana ya *Barrick* waliridhia baada ya mazungumzo barabara hiyo ianze kujengwa lakini nashangaa miaka minne Wizara ya Fedha, Wizara ya Madini wanazungumzia nini kwa miaka minne? Kwa hiyo kuna mahali fulani wananchi wanakaribia kupata

mafanikio lakini mazungumzo yanachukua muda mrefu sana, kwa hiyo barabara hii imekuwa sasa vumbi kama alivyokuwa anataka kuchangia ndugu yangu hapa, vumbi lake linatisha. Leo hii ukimkaribisha mgeni kutoka Geita ukamwambia njoo Dodoma unitembelee akifika hapa utafikiri umekutana na ninja alitaka kuvamia mahali kwa sababu pua zote zitakuwa zimejaa vumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme wazi kama maknikia yanapita hapo na dhahabu kuchenjua tunategemea ipite hapo nimshukuru nimpongeze sana Mheshimiwa Rais amefungua na amezindua kiwanda cha kusafisha dhahabu *refinery* pale Mwanza wamesema kuna sehemu itakuwa kwa ajili ya kukopesha wachimbaji wadogo, sasa hii dhahabu tutaitoaje huko Runguya tutaitoaje huko Msalala, tutaitoaje huko Geita ili iende Mwanza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama barabara tu inazungumziwa miaka minne na wadau wanataka kuweka fedha lakini haieleweki inaishia wapi, kwa hiyo niseme wazi ili tuendelee kuzalisha vizuri na dhahabu iendelee kwenda wamesema kuna kilo 400 kwa siku inatakiwa kilo 400 lakini baadaye inatakiwa kilo 900, kilo 400 ni karibu nusu tani, lakini kilo 900 ni karibu tani moja itapatikana wapi hii, lakini nijielekeze tena kwenye kod...

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye mjadala wa bajeti uliopo mbele yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa pumzi na uhai,

naomba aendelee kutulinda ili tuweze kuendelea kulitumikia Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji aliyemaliza kusema amezungumzia jambo la nchi yetu kuanzisha *refinery* ya kusafisha dhahabu hili ni jambo sana, nataka kuipongeza Serikali kwa hatua kubwa hii ambayo inaenda kuongeza thamani ya dhahabu yetu lakini tukipiga hatua zaidi kwa benki kuu kununua dhahabu ile maana yake tunaenda kuifanya sarafu yetu iwe na thamani zaidi, hongereni sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi kuna jambo aliliona, jambo ambalo limekuwa likipigiwa kelele kwa muda mrefu kuhusiana na kodi ya ongezeko la thamani kwenye sekta hiyo, ametoa maelekezo kwamba kodi ile isiwe kikwazo cha sisii kuweza kupata manufaa zaidi kutokana na sekta hii ya madini. Hapa ndipo ninapotaka kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita tulifanya mabadiliko makubwa sana ya kuruhusu wachimbaji wadogo kuingia kwenye sekta hii, tuliondoa kodi zilizokuwa na kero na hali ile ikachangia wachimbaji wadogo wa Kitananzania kuingia kwa nguvu kubwa kwenye uchimbaji, hali ambayo imeifanya sekta ya madini kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wetu. Lakini ninapata hofu kwa *measures* za kikodi zinazopendekezwa na hofu kwamba tunaweze kufifisha jitihada hizi ambazo tumekwishazifanya na zimeleta manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendelezo yaliyopo hapa yanaenda kubadilisha kumtambua mchimbaji mdogo ni nini, Sheria ya Madini inamtambua mchimbaji mdogo katika kiwango fulani kikubwa mapendekezo yanayokuja hapa yanaenda kumtambua mchimbaji mdogo Katika *level* ndogo sana, hii inaweza kuleta kikwazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yanayokuja yanaenda kupandisha kodi kutoka asilimia saba mpaka

kwenda asillimia 10, sina uhakika kama tumefanya utafiti wa kutosha kwa nchi zinazotuzunguka wao kodi yao iko vipi, hofu yangu hapa ni kwamba tunaweza kuweka kodi hii tukajikuta tunarejesha tatizo la utoroshaji wa madini kwenda nje. Hivyo ile tamaa yetu ya kuona viwanda hivi tulivyovianzisha vina pata malighafi tukajikuta tunajipiga risasi wenyewe kwenye mguu wetu kwa madini haya kusafirishwa kwenda nje; naiomba Serikali iliangularie vizuri suala hili. Nayasema haya kwa sababu wakati tukiongeza hivi tukumbuke kuwa zipo taasisi nyingine na zenyewe zinaweka tozo kwenye sekta hii hii. Leo hii tunapozungumza watu wa mabonde, Bonde la Ziwa Victoria na kwingineko wanamtoza shilingi milioni sita kwa mwaka mchimbaji mdogo. Kwa hiyo tuangalie jambo hili lisije likawa kikwazo kwenye ukuaji wa sekta yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye eneo la kilimo cha alizeti, naipongeza Serikali kwa jitihada hii. Sisi Mkoa wa Tanga tuliwekwa kwenye mazao saba ya kimkakati, kwa maana ya zao la mkonge, lakini Mkoa wa Tanga umebarikiwa, kwamba unapata mvua mara mbili kwa mwaka. Hivi kwa nini tuisitumie fursa hii ya upatikanaji wa mvua mara mbili kwa mwaka tukauingiza Mkoa wa Tanga kuwa mionganoni mwa mikoa inayolima zao la alizeti? Kwa sababu kilimo cha mkonge kinachukua miaka mitatu kuanza kuzalisha, sasa katika kipindi cha hapa katikati ardhi ile inaweza kutumika kuzalisha mazao ya mafuta haya. Kwa hiyo naiomba Serikali iangalie eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu huko nyuma mzee Kingunge marehemu alipokuja kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga alifanya uamuzi wa kuhakikisha mashamba yote ya mkonge yanatumika kulima kilimo cha mazao ya mahindi; na katika kipindi kile Mkoa wa Tanga uliongoza katika Taifa hili kwenye uzalishaji wa mahindi. Tukitumia mtazamo huu tunaweza kusaidia kukuza uzalishaji wa mazao ya mafuta katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu mapendelekezo ninayoyaona yanakuja hapa ya kikodi kwenye zao la mkonge. Nataka niipongeze Serikali kwamba

ilifanya kazi kubwa sana ya kufufua zao hilo la mkonge, hamasa kubwa iliingia na mifumo ya kikodi iliyokuwa imewekwa ilikuwa inamuhakikishia mkulima kuwa na bei inayotabirika na bei nzuri. Mapendekezo haya yanayokuja yanakwenda kuua hamasa ya kulima zao la mkonge yanakwenda kumsababishia mkulima mdogo aweze kupata bei ndogo na hivyo ulimaji au ufufuaji wa zao hili unakwenda kuanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie upya jambo hili eneo la *produce cess* na lile lingine hebu tuangalie vizuri. Yupo mtu tumempa jambo hilo atalizungumzia vizuri ndugu yangu Mnzava, lakini naomba sana Serikali mliangalie kwa umakini eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Serikali kwa kutanua wigo wa kodi. Ni jambo ambalo tumekuwa tukihangaika nalo kwa muda mrefu, nikupongeze Mheshimiwa Waziri umekuwa na ubunifu mkubwa sana, hongera sana. Lakini yapo maeneo mengine hebu tuyaangalie. Tunapofanya uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa sasa hivi kampuni zinazoagiza mafuta kutoka nje hazijasajiliwa hapa. Kwa hiyo kunakuwa na shida ya ushindani kati ya kampuni za wazawa zilizoko hapa na zile za kutoka nje. Za kutoka nje hazilipi *cooperate tax na service levy*. Hii inasababisha ushindani kati ya kampuni hizi za nje na hizi za ndani unakuwa si sahihi. Hebu tuangalie eneo hili tuweze kuona kama tunaweza kutumia mwanya huu kuweza kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Sanga atafatiwa na Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanzা nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nipende sana kumshukuru Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia kwa jinsi ambavyo anachapa kazi. Lakini Zaidi nimshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa bajeti ambayo kwa kweli mimi kama kijana najivunia na kama Mtanzania najivunia kwamba ni bajeti ambayo imeenda kuleta mabadiliko makubwa sana. Shukrani hizi nazitanguliza na *quote* moja kutoka kwa Rais Mstaafu wa Marekani Barack Obama, anasema; "*Change will not come if you wait for someone or other person. We are the ones we have been waiting for, we are the change that we seek.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niseme jambo moja, kwamba Mheshimiwa Waziri *you are the game changer*. Wewe ni *game changer* kwenye siasa ya Serikali yetu kwa sababu gani, bajeti hii inatubeba Wabunge wote katika majimbo yetu huko tunakoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tukilisubiria jambo kama hili, kuwa na bajeti ambayo ni *inclusive* kwa mawazo ya Wabunge, ya Mawaziri na wananchi. Ndiyo maana wakati wote Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwa anasoma bajeti hii hapa alisema nimeagizwa na mama tuzungumze na Waziri wa TAMISEMI, nimeagizwa na mama tuzungumze na Waziri wa Mambo ya Ndani, nimeagizwa na mama niongee na Waziri huyu; maana yake ni kwamba ni bajeti ambayo ni *inclusive* kuanzia Mawaziri hadi Wabunge. Hili ni jambo ambalo nasema wewe ni *game changer*. Kwa hiyo mimi nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasimama kwa mara nyingine tena nikishukuru. Mimi hili ni Bunge langu la kwanza la Bajeti, lakini nilishauri mambo karibia Matano kama siyo manne ndani ya Bunge hili na yote yamependekezwa kwenye bajeti hii na yanaenda kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nilishauri Serikali iondoe kodi kwenye nyasi bandia, Serikali imepokea na imeenda kulifanyia kazi. Nilishauri kwenye Bunge hili kwamba kwenye michezo ya *betting, betting companies*

zichangie michezo kwenye nchi hii, bajeti imelichukua imeingizwa humu ndani, asilimia tano za *betting companies* zitakuwa zinapelekwa kwenye michezo. Nilisimama kwenye Bunge hili nikashauri kuwa gharama za bodaboda ni nyingi, mama yetu amesikia kilio cha bodaboda zimeondolewa toka elfu 30 hadi elfu 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikasimama kwenye Bunge hili tena nikashauri viwanja vyote vya mpira kwenye nchi hii viwekwe nyasi bandia. Rais akiwa Mwanza juzi ameagiza Chama cha Mapinduzi kuanzia sasa kiruhusu mchakato wa kuweka nyasi bandia kwenye taifa hili. Kwa niaba ya wanamichezo wa taifa hili nimesimama kushukuru na kusema ahsante sana. Kwa sababu haya ambayo mmeyafanya hamyafanyi kwa maslahi ya Watoto wenu mnafanya kwa maslahi ya Watanzania wote. Wanamichezo walloko huko saa hizi wanasherehekea kuona kwamba sasa mpira wao utaenda kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, masuala ya *betting companies* sasa yataenda kuchangia michezo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitatumia dakika nyingi sana nikuombe jambo moja tu katika wakati wako na wakati mwininge hayo umetupokea. Suala lingine nilishauri Serikali iangalie namna ya kuunda ama kampuni au wakala wa kuruhusu vifaa vya michezo vipunguzwe kodi mashulen; mambo ya jezi na mipira, nilishauri hapa ndani ya Bunge. Na ninakusihi Mheshimiwa Waziri, ninakumbuka una ahadi kule Ruruma Sekondari, ninakumbuka una ahadi kule Kengege Sekondari. Kila Mbunge ameahidi vifaa vya michezo huko kwenye shule mbalimbali. Ukienda kwa Mheshimiwa Tulia, Mbeya Sekondari ameahidi vifaa vya michezo, ukienda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ameahidi vifaa vya michezo kule Iringa. Kila Waziri hapa ameahidi vifaa vya michezo shulen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione tija sasa kuwa na wakala maalum ambako sisi Wabunge tutaenda kununua vifaa vya michezo kwa punguzo ili nchi nzima watoto wetu

wasianze kushangaa kuona jezi wakienda kwenye UMITASHUMTA, jezi wakutane nazo tangu wakiwa shulenii. Kwa sababu kwa sasa kila Mbunge anatumia fedha zake nyinigiza mfukoni kuagiza vifaa vya michezo China ili aende aka-support michezo jimboni kwake. Tuliomba Serikali ihangaike. Kama tuna wakala wa mbegu kama tuna kampuni za ranchi za taifa kama tuna kampuni za ndege, kwanini tusiwe na wakala wa vifaa vya michezo shulenii ambaye atasimamiwa na Serikali? Na hivyo vifaa vitakuwa vimepunguzwa ruzuku au imeondolewa kodi ili sisi Wabunge iwe ahueni kwetu na watoto wetu waweze kupata vifaa vya michezo vingi na vya kutosheleza na hatimaye michezo ya nchi hii iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mambo mengi sana, na niwaombe watanzania kwa haya aliyojasema Mheshimiwa Waziri tuunge mkono bajeti. Hatuwezi kujenga nchi kwa kufurahia tu kodi kupunguzwa, tufurahie kujenga nchi yetu pia kwa kulipa kodi kwa wakati na kodi ambayo inastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niwaombe Watanzania kokote waliko ye yeyote anayekushauri uilalamikie bajeti hii anakupotosha, kwa sababu nchi itajengwa na wenye moyo na wenye moyo ni Watanzania wote. Kwa hiyo mimi niombe tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri, tuiunge mkono bajeti ya Serikali na tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu. Ameonesha njia na ameshirikisha mawazo ya Wabunge walio wengi. Wakati ni wa kwetu sisi Wabunge, tukitoka hapa twende majimbo ili tukai-support bajeti hii asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha za vijana mjini Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mama Samia wameupiga mwingi sana. Kwa sababu gani, leo hii hakuna bodaboda anapiga kelele kuhusu mambo ya bodaboda., hata *traffic* wenyewe wataacha kusumbua. Shilingi elfu 10 ni *reasonable*, kwa sababu kama basi lilikuwa linapakia watu 30, lilikuwa inapakia watu 60 analipa 30,000, boda boda anapakia mtu mmoja analipa 30,000, ile imetuonyesha kabisa sisi ni watu

wa aina gani. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri *you are the really game changer* na kwa hili Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mambo mengi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, atafatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ili na mimi nichangie bajeti yetu. Nami kama walivyosema Wabunge wenzangu mara kadhaa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote kwa kutuletea bajeti ya namna yake ambavyo kama Waheshimiwa Wabunge wameshasema mara kadhaa hapa mazuri ya bajeti hiyo nami nirudie yale ambayo wana Kilombero na wananchi wa Morogoro wanayashukuru na kuyapongeza. Mathalani suala la fedha za *TARURA*, milioni 500 kila Jimbo, Bima ya Afya kwa wote, mazingira mazuri ya biashara na kuwekeza katika kukuza thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni bajeti ya namna yake na Mheshimiwa Waziri kaka yetu Mwigulu anathibitisha ubora wa watu ambao wanapenda timu ya yanga. *Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na pongezi hizo nina mambo kama mawili ama matatu ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala zuri sana linalohusu posho kwa Waheshimiwa Madiwani tunalishukuru na tunalipongeza jambo hili. Lakini kama sisi tumesema Waheshimiwa Madiwani ni Wabunge wenzetu kule kwenye halmashauri, naishauri na kuiomba Serikali huko mbele tunakokwenda kuwe na utaratibu maalum wa vyombo vyaya usafiri kwa madiwani. Vyombo vyaya usafiri ambavyo vitawekewa utaratibu kama tulivyowekewa Wabunge mkopo wa magari tunaweza kufikiria pia Waheshimiwa

Madiwani wakawekewa mkopo kama wa lazima hivi usiokuwa na riba kubwa wa kupata walau pikipiki nzuri za kisasa za kuwasaidia Waheshimiwa Madiwani kufanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa Halmashauri imeondolewa mzigo wa posho sasa hivi mambo ya simu na nini kule kwenye halmashauri wanaweza wakayaangalia. Lakini pendekezo langu; Mheshimiwa Waziri ukweli ni kwamba kutokana na changamoto za baadhi ya majimbo Madiwani wakati mwingine wanateseka sana kwenye usafiri. Wasipopanda gari la Mbunge watadoea doea gari za halmashauri, lakini wakiwa na pikipiki zao zitawasaidia kufika kwenye vikao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mimi nina jambo mahsus i kwa Mheshimiwa Waziri, hasa la barabara yangu ya Ifakara Kidatu, na hapa nataka niseme kidogo, naona ukishikika kalamu Mheshimiwa Waziri, mimi nafarijika sana. Sisi tunajenga barabara kilometra 66.9 ya lami, mwaka wa nne tunajenga. Yaani kila siku nikisimama hapa nasema mpaka nimeenda nimekaa chini kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina changamoto nyingi, na hasa inauma kwa sababu unakuta wataalamu wa ujenzi wa barabara hii wanalalamika lakini wanakwambia Mbunge hii naongea mimi na wewe. Sasa barabara yetu Mheshimiwa Waziri imesainiwa na Wizara yako, na juzi tulikuwa na kikao na Wizara ya Fedha pale. Nataka kushukuru kwa dhati Katibu Mkuu wa Ujenzi na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kaka Emmanuel Tutuba kwa kweli ni msikivu, na kikao cha juzi kimeanza kuleta matumaini kwamba kuna changamoto kwa kweli watazitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kikao chetu cha mkoa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Morogoro katika mambo ambayo tuliambiwa tunatakiwa kupata elimu ya kuyasemea mojawapo ni barabara hii; na kwenye kikao kile wataalamu wa ujenzi bila kutaka kuwataja hapa walisema changamoto; kuwa ni mvutano wa Mhandisi mjenzi na mshauri. Na

wakasema kwamba mhandisi mshauri akimaliza muda wake aende, kwa sababu barabara ina fadhiliwa na *European Union* mkandarasi mshauri ameshachukua bilioni tisa mpaka sasa tunajenga kilometra 66.9 ameshachukua bilioni tisa mpaka sasa hivi barabara inasuasua. Mheshimiwa Waziri jambo hili liko kwako mkataba wa barabara ile ya ujenzi ya Ifakara Kidatu umesainiwa na Wizara ya Fedha. Sasa nimejaribu kumuelewesha Mheshimiwa Katibu Mkuu na nimeona *respond* yake kwamba atafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza na wewe European Union wameshaanza kusita kutoa fedha za mshauri, Serikali yako kwenye bajeti hii inatakiwa imlipe 1.4 Euro milioni karibu bilioni 4.6 za kumuongezea mkataba mkandarasi ambaye anamaliza mkataba wake Juni. Hii bilioni 4.6 wataalamu wale ambao wanatuambia Mheshimiwa Mbunge tuongee pembeni wanasema pesa hizi ni nyingi na huyu mshauri analipwa hela nyingi kuliko wakandarasi wote nchi hii kwanini? Kuna jambo gani nyuma ya pazia? Na hao wa ujenzi wanasema nusu ya fedha hizo aidha *TANROAD* inaweza kusimamia hiyo barabara au wakandarasi washauri wengine. Tuna miradi mikubwa hapa inataka akili nyingi kuliko kilometra 66 za barabara, kwa nini mkandarasi mshauri hapa alipwe fedha nyingi Zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa tuliamiwiwa hawa watu waligombana huko nje ya nchi kwenye mradi, ugomvi wao na mvutano wao kugombana wanauleta hapa, mpaka mambo mengine yanataka kwenda kwenye mahakama za kimataifa, mara huyu kamkataa huyu mara huyu kamkataa huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameingilia jambo hili, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alienda na ametoa maelekezo kwamba ili barabara ile ikamilike ambayo iko chini ya Waziri wa Fedha inatakiwa Mhandisi mshauri, Juni hii analize aondoke ili *TANROAD* wapewe nguvu wasimamie barabara hii na wakandarasi washauri wanaoona wanafaa ili tuweze kusongambele. Kwa hiyo Mheshimiwa nakuomba

chonde chonde, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesha *intervene* na wewe uki-*intervene* hapo tutamaliza jambo hili vizuri na barabara yetu itaenda mbele. Ni aibu sana, kilometra 66.9 ambazo fedha zipo kwenye Wizara yako mfadhili kalipa lakini mpaka leo tunasusua. Mfadhili ameshaonesha hataki kumlipa mkandarasi mshauri pesa tena kwa sababu amefika *maximum* ya malipo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa sababu wataalamu wetu wa ujenzi wanatuambia mambo haya tuyaseme na sisi wanasiasa hasa vijana kama Mungu akipenda *as a factor remain constant ceteris paribus we have nothing to lose because age is on our side*, Mungu akipenda. Kwa hiyo kutetea nchi hii tutaendelea kusema ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye kilimo; mimi la kwangu nataka kuungana na Mbunge wa Hai, kuhusu ushirika. Ushirika ni matatizo, matatizo kweli kweli. Na kama kweli tunataka kukuza kilimo chetu, na mimi nina *interest* na kilimo cha miwa kule, ni vizuri Wizara ya Kilimo ikatoa elimu ya kutosha kwa watu wa ushirika; hasa zile Bodi ili ziweze kuendeleza mazao ya ushirika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwambia hapa mfano wa jambo moja ambalo limefanywa na viongozi wangu wa ushirika kule, na migogoro hii Mheshimiwa Waziri anahangaika nayo kuitatua kila siku. Wanabandika taratibu za kutafuta zabuni zinafatua wanakuja wanatengua, mgogoro! Mgogoro! Mgogoro! Kama alivyosema Saashisha, kwamba Bodi hizi za ushirika lazima ziangaliwe vizuri. Kama zimebandika taratibu wanataka wazabuni wenyе sifa hizi wamepatikana wasitengue zile barua zao, kwa sababu wanavyotengua barua wanampa leo huyu inaleta mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nataka kutumia nafasi hii kuwasih sana wakulima wangu wa miwa hasa wa Sanje ambao wanani pigia simu kila wakati wanataka Mkutano Mkuu ili waamue jambo hili liishe; na naomba sana wavute Subira na Mungu atatusaidia tutamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kusisitiza kwamba namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama kweli wanataka kupandisha thamani ya mazao yetu kama walivyoahidi katika bajeti basi wasimamie vizuri ushirika, na nimemuomba Mheshimiwa Waziri awaruhusu hawa wakulima wa miwa wafanye mkutano wao mkuu waamue juu ya jambo hili. Ninhambukuru Dkt. Ndiyege ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Ushirika, amelifanya kazi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda sasa, kama kweli tunataka Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia iendelee kufanya vizuri sisi pamoja na wote wanaomshauri ni vizuri tukasisitiza kuhusu mambo ambayo Mheshimiwa Rais aliyafanya akiwa Makamu wa Rais na Hayati Dkt John Pombe Magufuli yakaendelezwa na yakasimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda sasa, kama kweli tunataka Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia iendelee kufanya vizuri sisi pamoja na wote wanaomshauri ni vizuri tukasisitiza kuhusu mambo ambayo Mheshimiwa Rais aliyafanya akiwa Makamu wa Rais na Hayati Dkt John Pombe Magufuli yakaendelezwa na yakasimamiwa, kwa sababu Watanzania wanaona na wanasikia. Ni hatari sana sasa hivi ukisikia kwamba kuna mkulima wa gunia moja analazimishwa kutozwa ushuru, maana yake Serikali iliyopita ilikuwa inasisitizwa ukiwa na chini ya tani moja vusha vusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekwenda kule Morogoro, nimekuta wakulima wanalamika wanasesma mbona sasa hivi tunatozwa na tulikuwa hatutozwi. Kwa hiyo, mtu yoyote anataka kukwamisha Serikali hii ni yule anayetaka kutengua mazuri ambayo Mheshimiwa Samia aliyafanya akiwa na hayati Dkt. Magufuli ambayo sasa hivi anayaendeleza na kurekebisha upungufu au kuuondoa, mathalani hiyo ya Machinga kuguswaguswa, mazao chini ya tani moja watu kuanza kutozwa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, Serikali yetu kurudi katika mikopo, lazima tuombe Mungu kwamba

mikopo hii ambayo nchi yetu itachukua, iwe ni mikopo mizuri, yenye masharti mazuri. Hayati Dkt. Magufuli alisikika mara kadhaa akisema, tahadhari za nchi ya Afrika kuhusu mikopo hii. Kwa hiyo, mambo haya yote yakisimamiwa vizuri itaonekana kwa kweli tunasonga mbele na tunaenda mbele pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye miradi ya maji na Wizara ya Maji. Ni wazi kuwa kuna Wabunge tulikutana hapa kama 28, tukakutana na Waziri wa Maji ambaye anafanya kazi nzuri, tukazungumzia Miradi ya Miji 28 na kwamba miradi ile ni muhimu na kwa sababu ilikuwa ni mkopo kutoka *Exim Bank* ya India process zilikuwa zinaendelea. Sasa kaka yetu mara nyngi anafuatilia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Dorothy George Kilave, ajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hii bajeti muhimu. Nianzie pale walipoishia wenzangu kumpongeza hasa hasa, Mheshimiwa Rais wetu mpPENDWA kwa jinsi alivyokuwa mbunifu na bajeti yake hii ambayo ni ya kwanza katika utawala wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hii bajeti imetushangaza wengi katika ubunifu ambao wameuonyesha, lakini pia najua pamoja na yeye na timu yake, timu ya Makamu wa Rais Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpPENDWA wetu, naye kuna mchango katika bajeti hii, lakini kuna Wizara ya Fedha pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Fedha pamoja na Serikali nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe pia kwenye bajeti hii mchango wako ni mkubwa mno. Nilikuwa najaribu kufanya analysis ya bajeti hii, zaidi ya asilimia 70 ya michango ya Wabunge, nimeangalia kwenye *Hansard* katika miaka 15 iliyopita, ile michango mizuri yote ya Wabunge imechukuliwa na Serikali safari hii. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho kinaonyesha namna gani sisi kama Wabunge ni muhimu katika utayarishaji wa bajeti. Kwa hiyo lile jukumu letu la msingi la utayarishaji wa bajeti, nafikiri kwa safari hii limefanyika vizuri sana. Kwa hiyo pongezi kwa Bunge lako vile vile pamoja na Wabunge wote kwa bajeti hii nzuri. Nashukuru sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hivyo, nikiangalia bajeti hii imezingatia tija kwenye kilimo, imezingatia ushindani kwenye masoko yetu. Vile vile, ukiangalia ni kiasi gani ambapo karibu majimbo yote yameweza kunufaika kwa milioni mia tano ambazo amezitoa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuziboresha barabara zetu za vijijini, lakini tumeshangazwa vile vile na nyongeza ya milioni 600 kwa ajili ya shule zetu za sekondari katika kata ambazo hazina shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza zaidi hasa kwenye bajeti hii ambayo imeonyesha vile vile kuwa kutakuwa na barabara yetu ya *TANZAM*, kipande kile cha Igawa mpaka Tunduma ambayo imezingatia vile vile kuwa na njia nne katika kipande cha Uyole mpaka uwanja wetu wa ndege wa Songwe, nafikiri hiyo ni hatua muhimu sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ku-*consider* hiyo lakini nashukuru kwa ujenzi vile vile wa barabara ya Isyonje kwenda mpaka Kikondo Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru vile vile kwa Barabara ya Mbalizi kwenda Makongorosi. Pia nashukuru kwa kuwemo kwenye bajeti Barabara ya Mbalizi Shigamba ambayo hii ina matawi yake ya kwenda Isongole mpakani na Malawi. Kwa kweli nashukuru sana. Vile vile nashukuru kwa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoiangalia hii bajeti imelenga kwenye kilimo, lakini imelenga zaidi kwenye maandishi. Ukiangalia bajeti hii, hakuna mahali utaona kuna uwekezaji kwenye kilimo, hakuna. Kama kuna uwekezaji ni kidogo mno, wala hata huwezi kuuona, lakini nimeshangazwa badala ya uwekezaji, nimeona bajeti inaonyesha ongezeko la kodi kwa wakulima, ongezeko la kodi ya asilimia mbili kwa kilimo chetu ambacho hakina tija.

Kwa kweli Mheshimiwa Waziri aende akaliangalie hilo, pamoja kwenye hotuba yake ya Kiswahili ameonyesha kwamba hiyo kodi haitamgusa mkulima mdogo. Hii kodi hajibagua, kwenye sheria ambayo imeandikwa Kiingereza hii kodi ni kwa mkulima ye yeyote, hata mtu anayekwenda kuuza kuku, anaenda kuuza mayai kwenye hoteli itabidi akatwe hiyo kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia dhima ya kwetu ni kumjenga mkulima, kuwawezesha wananchi wetu ambaao ni wengi. Sasa ukianzisha hii kodi ina maana hao wakulima kwa kiasi kikubwa unawaongezea mzigo, kwa vile mfanyabiashara ye ye atataka faida, lakini mzigo wa hii kodi utaenda kwa mkulima. Mkulima wa Tanzania leo hii ukimlinganisha na mkulima wa nchi jirani yetu hata kwa kiasi tu cha mahindi, mkulima wa mahindi anazalisha mahindi kwa gharama ya zaidi ya 300,000, lakini mapato yake ya mahindi ni 100,000 na tena hayo mahindi akiyauza *NFRA*. Sasa huyo mkulima unamtoza kodi kuto kana na nini na hii kodi ni ya mapato, mtu apate faida, huyu mkulima hana faida, kwa nini umtoze hii kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu uchumi wetu tuna ongelea uchumi shindani, inabidi tujilinganishe na wenzetu. Kwenye kahawa, uzalishaji wa Tanzania kwa mti mmoja ni gram 350 lakini mzalishaji wa jirani yetu Kenya kwa kahawa ya arabika ni karibu gram 400, mzalishaji wa Brazil ni gram zaidi ya 1,200. Sasa wote tunaingia sokoni, tufanye nini ili tumsaidie mkulima wetu aweze kuingia kwenye ushindani kwa vile bei haichagui kwamba hii ni kahawa ya Tanzania, Kenya au Brazil.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nategemea Mheshimiwa Waziri atakapokwenda kuiangalia hiyo bajeti tumsaidie viyi mkulima. Ili uzalishe vizuri unahitaji mbolea. Kwa hiyo tupeleke fedha isiyopungua bilioni 40 kuwasaidia wakulima kwenye ruzuku ya pembejeo, lakini pia tupeleke pesa kwa ajili ya utafiti ili wakulima wetu waweze kuzalisha kwa tija. Kwa hiyo, bado kuna haja ya kuongeza bajeti ya kilimo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la utafiti, nitatoa mfano mdogo tu. Tuna kilimo cha pareto ambayo inatumika kwa ajili ya kuhifadhi mazao. Pale kwenye halmashauri ya kwangu, wakulima wameshaanza kutumia maua ya pareto kwa ajili ya kuhifadhi mazao na imeonyesha kuwa inatumika vizuri zaidi, ina hifadhi kuliko viatilifu vingine. Kwa hiyo ningeomba fedha zipelekwe kwenye Taasisi yetu ya Utafiti ili pareto iinglie sasa hivi kwenye uzalishaji wa viatilifu kwa ajili ya kuhifadhi mazao yetu na kupunguza *post harvest losses*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia leo kwenye taarifa ya habari kuhusu ushindani na majirani zetu, ushindani na nchi Jirani, wameanzisha sasa hivi sheria ya kuzuia malori ya Tanzania kuingia na kusafirisha mizigo kwenye nchi zao. Sasa tusipojitatihidi katika hilo tutajikuta Tanzania tumekuwa kisiwa, bandari yetu itatumika viyi kama hawa wasafirishaji watazuiwa na ukichukulia kwamba hata uboreshaji wa reli yetu nao vile vile una changamoto ambazo zinatokana na majirani hao hao. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie ni namna gani tuboreshe ushindani katika suala la usafirishaji, likiwemo la kuboresha bandari; la kuboresha reli yetu ya TAZARA, lakini vilevile tuangalie kupeleka meli kwenye Ziwa letu la Tanganyika ili zisafirishe mizigo kwenda Zaire.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli pendekezo langu kubwa ambalo nalionia katika bajeti hii, iende ikae chini iangalie ni namna gani ya kumsaidia mkulima. Leo hii mkulima hasaidiwi kwa aina yoyote na hiyo kodi ya asilimia mbili, naomba iondolewe ilikuwepo kwa NFRA, inawezekana

labda ni kwa ajili ya kuisaidia *NFRA*. Naiomba hata kule *NFRA* na kuondoke ili mkulima aweze kupata bei nzuri na hiyo sio kwa ajili ya mahindi tu, lakini hii asilimia mbili ni kwa mazao yote, kwa hiyo utakuwa ni mzigo mkubwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nashukuru sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga atafuatiwa na Mheshimiwa Dorothy George Kilave na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea ajiandae.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Serikali. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kunijalia afya njema, nimeweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeisikia bajeti ilivoletwa na Mheshimiwa Waziri, yapo maeneo ambayo niseme yamefanya vizuri, lakini yapo maeneo ambayo yana changamoto na inabidi zifanyiwe marekebisho kutokana na mapendekezo ya Wabunge na michango ya Wabunge inayoendelea katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye suala zima la wafanyabiashara na *TRA*, hii imekuwa ni changamoto kubwa sana na ya muda mrefu, kwa wafanyabiashara kugongana na watendaji wa *TRA*, lakini naamini baada ya kauli ya mama, lakini pia katika bajeti hii inaonyesha sasa wafanyabiashara wanakwenda kufanyabiashara zao kwa utulivu, kwa amani na kwa salama zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nyuma ilikuwa mfanyabishara ana wasiwasi na mteja akiingia dukani anajua huyu sijui katumwa, huyu sijui namna gani, lakini mwisho wa siku sasa wafanyabiashara wamekuwa na amani na biashara zinaenda kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii pia imezungumzia maslahi ya wafanyakazi. Kimekuwa ni kilio kikubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunage wengi wanaposimama kuhusiana na maslahi ya wafanyakazi. Jambo hili limeonekana na niseme tu bado kuna vitu vidogo ambavyo vikifanyiwa marekebisho naamini kabisa wafanyakazi wetu nao sasa watafanya kazi kwa amani na mambo yao yataenda vizuri kama ambavyo wamekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Ubunge lakini pia mimi ni mwanamichezo. Niseme tu kwamba Serikali imeondoa kodi kwenye hizi nyasi bandia, lakini kwenye hili naomba niambie Serikali isiondoe kodi hizi kwenye majiji peke yake kwa sababu ukiangalia majiji yako sita tu na majiji mawili tayari yanavyo viwanja vyenye nyasi bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hili nashauri kwamba, iwe ni kwa nchi nzima kwa sababu mimi natokea Mkoa wa Tabora. Pale katika Mkoa wetu wa Tabora tuna kiwanja chetu cha Ali Hassan Mwinyi, kiwanja kile ni kikubwa, kiwanja kizuri, lakini kimetelekezwa, kimeachwa kwa muda mrefu sana. Ni imani yangu hizi nyasi bandia zikiletwa, angalau na sisi pale Tabora sasa tutaweza kucheza michezo mizuri hata hii michezo ya ligi kuu itakuwa inaletwa katika uwanja wetu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe tu na nishauri kwa Serikali, utaratibu wa vibali basi wawape BMT ili waweze ku-*control/uagizaji* wa nyasi hizi hili kusiwe na vurugu ya hapa na pale ya wafanyakabiashara kutaka kuweka mambo yao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuishauri Serikali, hizi fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika maeneo yetu tungeomba sana zisiwe kwenye makaratsi. Fedha hizi ziende ziende zikafanye kazi ambazo zimekusudiwa. Leo mimi hapa ninavyozungumza katika Mkoa wetu wa Tabora tumeletewa maji ya Ziwa Victoria. Maji yamefika lakini bado hayajasambazwa kwa wananchi, kwa hiyo niombe sana fedha hizi zipelekwe ili ile

miradi ambayo inahudumia wananchi wengi iweze kufanyika, baada ya bajeti hii watu waweze kupata ile huduma ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama ambavyo tumeshauri kwenye bajeti za Wizara mbalimbali kuna masuala ya zahanati, Vituo vya Afya, hospitali za wilaya kwenye wilaya ambazo hatuna hospitali za wilaya, tungeomba sana fedha hizi ziende na zikawe kipaumbele ili wananchi wetu waweze kupata huduma bora kama ambavyo mama amepanga na anataka huduma hizi zifanyike hasa huko chini zikiwepo huduma za afya, elimu na maji. Kwa hiyo naomba sana fedha hizi zisiwe kwenye makaratasi za kufurahisha watu lakini ziende sasa zikafanye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la ushirikishwaji wa Wabunge wa Viti Maalum katika fedha zinazopelekwa za miradi ya maendeleo kwenye maeneo yetu. Wabunge wa Viti Maalum tumekuwa vinara wakubwa wa kueleza changamoto zinazotukabili katika mikoa yetu na maeneo yetu. Kama unavyofahamu sisi Wabunge wa Viti Maalum tunatumikia mikoa sio majimbo peke yake na tunapozungumza hapa tunazungumzia mikoa yetu na sio majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo changamoto zinazoletwa katika Bunge zinapokelewa, zinachukuliwa, katika utekelezaji wake Wabunge wa Viti Maalum tunawekwa pemberi. Juzi zimepelekwa shilingi milioni 500 kwenye kila jimbo, Wabunge wa viti maalum hatujashirikishwa. Juzi nimemsikia wifi yangu Ummy Mwalimu akizungumzia kuhusiana na fedha zitakazokwenda kujenga mashule, katika majimbo. Mheshimiwa Ummy amesema kwamba watacaa na Wabunge wa Majimbo ili waweze kuona ni kata zifi ambazo zitakwenda kupeleka hizo shule.

Sisi wanawake wa Viti Maalum tumeshiriki kwa namna moja ama nyininge kuzungumzia changamoto zilizopo za mashule, tunaomba tushirikishwa na sisi hili tuweze kusema kwamba wapi shule hizi ziweze kupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wangu una majimbo 12 Wabunge wa viti maalum tupo watatu inashindikana nini kutuingiza kwenye hizo fedha hili na sisi tuweze kushiriki katika fedha hizi za maendeleo ambazo tunazipigania hapa Bungeni. Jambo hili kwa kweli linaumiza na niseme tu linaonyesha kwamba kama Wabunge wa Viti Maalum hatuna chochote ambacho tunatakiwa kukipata. Wabunge wa majimbo wana fedha za majimbo wanapata, wanafanya kazi, Wabunge wa majimbo miradi ya maendeleo inayokwenda wanapewa inakwenda kufanya kazi, sisi Wabunge wa Viti Maalum tunatumia fedha zetu wenyewe kufanya majukumu yetu na kutekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinapofika kipindi cha kampeni, Wabunge hawa wa majimbo wanatutegemea sana sisi Wabunge wa Viti Maalum tuwasaidie kwenye kampeni ndio wanashinda majimbo hayo. Wasituogope tunakwenda kufanya kazi pamoja ili tuweze kuleta maendeleo katika maeneo yetu. Naiomba sana Serikali, sisi ni Wabunge, tunaomba itushirikishe na sisi tunahitaji kufanya maendeleo katika maeneo tunayotoka na ndio maana tumekuwa tukichangia sana kuhakikisha kwamba maeneo yetu, barabara, miundombinu ya hospitali, shule na kila kitu tunaizungumzia hapa. Kwa hiyo ningeomba sana tushirikishwe, fedha za maendeleo zinapokwenda na sisi tuwe ni sehemu ya fedha hizo kwa sababu tunaziombea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nikizungumzia sana kuhusiana na sekta ya viwanda kipindi cha bajeti za nyuma. Niseme tu kwamba, bado tuna changamoto kubwa sana katika sekta hii. Bado ni baadhi ya viwanda vichache tu ambavyo vinaweza kutoa kodi kubwa kwa Serikali tofauti na ambavyo tunaambiwa viwanda vilivyo vingi. Kwa hiyo ningeomba Serikali na kuishauri kuangalia namna bora ya kuwezesha viwanda hivi ili viweze kuwa na tija katika Taifa letu kwa kuongeza kipato cha Taifa letu kwa maana ya kuongeza pia kodi za makusanyo ya kila mwaka katika nchi yetu. Naomba sana sekta hii ya viwanda iangaliwe vizuri, kwani ni sekta kubwa ambayo inaweza ikawa na mchango mkubwa sana katika pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo suala zima la sekta ya utalii. Zipo changamoto kidogo katika sekta hii. Ni sekta ambayo Serikali inategemea kuleta kodi na kipato kwa Serikali, lakini ina changamoto kubwa sana katika maeneo mbalimbali ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto za miundombinu katika baadhi ya hifadhi zetu. Hiyo inapelekea kukwamisha watalii wengi kuweza kufika katika maeneo yetu. Bado tuna changamoto pia ya kuona ni namna gani tunavyoweza kuboresha maeneo yetu ya utalii kwa ujumla yaweze kuendana na hali halisi ambavyo watu wanaaisikia Tanzania na utalii jinsi ilivyo. Kwa hiyo, naomba sana katika bajeti hii tuweze kuboresha kwenye sekta hii ya utalii ili basi sekta hii iweze kuongeza pato zaidi ambalo limekuwa likipatikana kwani sekta hii inategemewa sana na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wa majimbo nadhani mmesikia mchango muhimu sana huo wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga. Nafikiri nasi wanawake, viongozi wetu wako hapo, ni vizuri tukutane huko, mengine tuongee kule, tushauriane huko. Kama ni Halmashauri ile ambayo unashiriki wewe kama Diwani au vipi. Kwa sababu sasa kama majimbo yako 10, hizo sehemu 10 maana yake kata ziko zaidi. Sasa wewe Mbunge mmoja wa Viti Maalum mkoa mzima, Wabunge wako 10, sasa wote mtawezajae kushiriki?

Kwa hiyo, hayo yote lazima tuwe tumekaa pamoja ili iturahisishie kuona namna ya kushirikiana kwa karibu. Kwa sababu la sivo tutakuwa na mivutano kila wakati. Nami ningetamani sana kila Mbunge ajione ni Mbunge kamili kwa sababu wote tuna kiapo kimoja.

Kwa hiyo, ni muhimu haya mambo tujadiliane kwa mapana ili tuone namna ya kwenda nayo.

Mheshimiwa Dorothy George Kilave atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi ajiandae.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona nami niweze kuchangia machache niliyokuwa nayo. Vilevile namshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, aliyenipezesha kusimama mahali hapa ili niweze kuongea. Zaidi naomba sana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa kazi nzuri anayoifanya na hata sisi wanawake tunajivunia kuwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme nawapongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa jinsi ambavyo wameweza kuleta bajeti ambayo naamini na wenzangu wanaamini hivyo kwamba ni bajeti yenye matumaini kwa nchi yetu. Hivyo basi, napenda kuwapongeza sana na niamini kwamba kile walichokuwa wamekiandika, basi wataenda kukitendea haki ili nchi nzima tuweze kufurahia matunda ya bajeti ya mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisiwe nyuma sana, mimi kama mimi nilikuwa nazoea tu kusikia bajeti hii kuisoma au kuangalia katika runinga, lakini napenda pia nijipongeze kwamba ni mmojawapo sasa katika kuhakikisha kwamba bajeti hii inapita vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana niweze kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, mama ambaye amekuwa msikivu, nasi kama Wabunge hapa tulikuwa na vilio vingi ambavyo tumevisema, lakini amekuwa makini na kuvisikiliza hata kuifanya Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba yale tuliyoyasema yanakwenda kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa kilio kikubwa kwanza tulicholia kwa ajili ya barabara zetu za TARURA. Ameweza kutoa fedha shilingi milioni 500 katika kata zetu, nasi kama Wabunge ambao tunakwenda

kuziangalia fedha hizi kwa makini, tuweze kupitisha barabara hasa ambazo zina vilio vikubwa vijiji pamoa na mijini kwetu, sisi tunaita barabara za ndani. Mfano kama kwangu, naweza kusema kwamba barabara zile za Tandika hakika ni muhimu sana kwani tunaita Kariakoo ndogo kule kwetu Temeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba tunamshukuru sana kwa fedha hizi. Siyo hilo tu, nampongeza kwa fedha ambazo naamini zinakuja, fedha zile za mashule kwa kujenga Shule za Sekondari katika kata ambazo zina mahitaji makubwa ya shule. Sitasita kuendelea kumpongeza mama yetu Rais kwa jinsi ambavyo hata juzi uwanja wa Mwanza kule ameongea mengi sana. Mama nakupongeza sana kwa sababu kwa hakika umetunyanya sana wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kuipongeza sana Serikali sikuvi kwa kusikia hasa vijana wetu ambao wamekopeshwa bodaboda, wengine wamekuwa wakifanya kazi zile za watu wenye bodaboda, hata hizi faini zimeweza kushushwa sasa na badala ya kuwa shilingi 30,000/=, imekuwa ni shilingi 10,000/=.

(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu ndugu zangu, Wabunge wenzangu, nimetumwa na Jimbo langu la Temeke niwashukuru sana Wabunge wote waliolila kilio hiki na hata sasa vijana wale wanasma watafanya kazi kwa bidii na siyo tu kwamba watafanya bila makosa, lakini watatii sheria bila shuruti. Nawashukuru sana Wabunge wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi ambayo wenzangu wameyaongea hapa, mimi leo nilisimama ili niweze kushukuru na kusema kwamba ahadi hizi zote zilizoweza kuwekwa hapa kwa niaba ya wananchi kupitia Wizara ya Fedha ya kwamba tunatamani kama alivyosema mwezangu hapa yasiwe katika maandishi. Sisi kama Wana-Temeke pia wananchi wote sasa hivi tumekaa macho, tunaangalia kwa macho, inawezekana mimi na wenzangu tunayasoma hapa na kuona kwamba yako kwenye

maandishi, lakini wananchi wetu wako macho sasa kuangalia hivi fedha ambazo tunasema tumekwenda kuzitoa kwenye *petrol, diesel* pamoja na mafuta ya taa kwamba ni shilingi 100 inaongezeka, nasi tunaziomba ziende kwenye barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana sasa Wizara ya Fedha mziangalie hizi fedha na mtakapozileta hakika zije katika yale ambayo yanategemea kufanyika pamoja na hizi fedha, zisiwe tu katika maandishi lakini sisi tuko tunatoa macho sasa tuweze kuona barabara zetu kwenye elimu, afya hata dawa zinaweza kupatikana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu kwamba Wizara ya Fedha nisikilizeni, mtakapokuja kutoa hotuba yenu ya mwisho hapa mtuambie mmeweka mkakati gani wa hizzi fedha zinazokusanya hilli zitumike kwa mahitaji yanayotakiwa hasa katika majimbo yetu na hasa katika barabara pamoja na mambo mengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba naishukuru Serikali yangu sikivu na ninaamini ya kwamba yote waliyoyasema yatakwenda kutimia na Mungu awabarika sana. Ahsanteni. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi na Mheshimiwa Abdalah Dadi Chikota ajiandae.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii nzuri ya bajeti. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kutuletea bajeti nzuri. Nampongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara. Ni bajeti ambayo ina matumaini kwa wananchi, bajeti ambayo imesikiliza mawazo asilimia 80 ya Wabunge na inaonyesha kwamba ile moja ya kazi ya Wabunge kuishauri Serikali, basi hapa katika bajeti hii inaonekana Serikali imesikiliza mawazo ya Wabunge nao wameenda kuyafanya kazi na wametuletea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kuchangia moja kwa moja kwenye upande wa afya. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kutuletea bajeti ya shilingi bilioni 265.8 kwa ajili ya afya, dawa vifaatiba na kumalizia miundombinu iliyojengwa na wananchi kwa nguvu zao wenyewe ikiwepo zahanati 8,004, pamoja na Vituo vya Afya 1,500. Namwomba Waziri wa Fedha, bajeti hii kwa upande wangu naiona bado ni ndogo kwa afya, lakini pamoja na udogo wake tuweze kuipokea hivyo ilivyo ila iende ikatekeleze kama inavyosomeka hapa, kama mpango ulivyo. Hii bajeti iende kama ilivyo, itekelezeke kule, tuisaidie *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kabisa ni jambo ambalo liko wazi kwamba *MSD* inafanya kazi katika hali ya uhafifu. Tunajua kabisa ina madeni nje na ndani ya nchi, lakini kama bajeti hii ambayo inaonekana hapa itapelekwa fedha hizi kwa ajili ya kuwezesha dawa na vifaatiba kama ambavyo imeelezewa, tunaona kabisa changamoto ya ukosefu wa dawa na vifaatiba itaenda kupungua. Kama Wabunge wengine ambavyo wameweza kusema na kumsifia Waziri wa Fedha, atakuwa ni Waziri wa kiwango cha juu kwa bajeti hii iliyokuja hapa. Naomba niseme, atakuwa ni Waziri wa Fedha wa kiwango cha juu sana kama bajeti hii itatekelezeka kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo atakuwa ameweza kututolea changamoto kubwa tunayopata akina mama na watoto mahospitalini kwa ukosefu wa dawa; na hasa kina mama zile changamoto za kupoteza uhai wakati wa kujifungua ambapo hata Mheshimiwa Rais wakati wa hotuba yake aliongea akasema katika moja ya vita atakayoenda kuipiga ni kuhakikisha vifo vya mama mjamzito wakati wa kujifunga vinaisha. Sasa vitaisha kama bajeti hii itatekelezeka kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri wa Fedha, bajeti hii ipeleke pesa zinakohitajika. Kama ni *MSD* tuisaidie iweze kuhudumia wananchi, waweze kupata dawa na vifaatiba kama inavyotakikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala zima la Bima ya Afya. Ilani ya Chama cha Mapinduzi

tuliyoinadi mwaka 2020, tuliwaomba wananchi kwamba wachague chama chetu, tutakuja na Bima ya Afya kwa kila mwananchi. Bajeti hii imeeleza na inaonyesha kwamba kwa mchakato wa mwazoni tunahitaji shilingi bilioni 145 kwa mwanzo wa fedha. Hata hivyo, naiomba Wizara, nilikuwa natamani Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*finalize* aweze kutuelezea, hii pesa ambayo ameona kwamba ni shilingi bilioni 145: Je, ni pesa ambayo imekaa kwa bima ya mfumo upi? Ni Bima ya *NHIF* au ni *CHF*?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotegemea ni wananchi wapate bima yenye tija, isiwe bima ile ambayo mgonjwa anaenda kutibiwa hospitali ya Serikali tu, hana *option* ya kwenda kwenye *private hospital*. Hii itatusaidia kuweka mahusiano mazuri kati ya Serikali pamoja na *private sector*. Ile sera yetu ya *PPP*itaweza ku-*apply* vizuri zaidi maana mgonjwa au mtu anayehitaji matibabu atakuwa na *option* ya kwenda sehemu yoyote aidha ni *private* au aende Serikalini na kote atapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Waziri wa Fedha, huu mchakato wa shilingi bilioni 145 wa Bima ya Afya uwe ni wa bima ambayo ni kama ya *NHIF* ambapo mgonjwa anaenda sehemu yoyote anapata ile huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nimeona hapa, inaonyesha bajeti yam waka 2034/2035 ndiyo tutakuwa tumeweza kumaliza suala hili zima la Bima ya Afya kwa kila mwananchi. Kwa hiyo, nikiangalia hapa naona kama tuna miaka 14 ya kuweza kukamilisha hili. Natambua kabisa *universal health coverage* siyo suala dogo la miaka miwili mitatu minne, iwe imeisha.

Naomba Waziri wa Fedha arudishe nyuma kidogo kwa sababu mwaka 2020 tumewaomba wananchi kwamba tutawaleta Bima ya Afya; mwaka 2025 tena tutaenda kuwaambia tena tunawaleta Bima ya Afya, wakati huo bado tuko kwenye *process*. Kuna wengine wamepata kuna wengine awajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana, tena mpaka 2030 bado tutakuja kuwaambia wananchi tunawaleteeni Bima ya Afya kwa kila mwananchi. Bado naona ni muda mrefu sana, naomba tu apunguze. Japokuwa ni jambo kubwa, sawa, lakini hebu irudi nyuma kidogo tusiwe tuna muda mrefu wa kupeleka hii Bima ya Afya kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la kilimo. Natambua tuna benki ya kilimo, tuna *Tanzania Investimate Bank* ambazo zina riba kubwa. Nampongeza Mheshimiwa Rais ameweza kuona riba hizi ambazo ni kubwa na zinawakandamiza wananchi ambao wanashindwa kuweka maendeleo zaidi. Namwomba Waziri tuwe na mfuko wa kuchochaea maendeleo ya kilimo na viwanda kwa sababu tunaelewa tuna Sera ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita ya Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hizi sera tukiwa na mfuko wa kuchochaea maendeleo, tunaona kabisa ni namna gani wananchi wataenda kukopa pesa kwa riba nafuu kwenye mifuko ya kuchochaea maendeleo. Wakati huo huo, tunajua kabisa kilimo kinatupatia asilimia ya 65 ya ajira, asilimia 66 tunapata malighafi, asilimia 100 chakula tunachotumia sisi Watanzania kinatokana na kilimo.

(Hapa kengele ya kwanza illilia)

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, sorry ni kengele ya kwanza au ya pilii?

NAIBU SPIKA: Ya kwanza.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 100 tunapata chakula kwa Watanzania na vilevile asilimia 30 ni kwa ajili ya kuingiza pesa za kigeni.

Mheshimiwa Nailbu Spika, vile vile kwenye viwanda tunakuza thamani ya malighafi ya bidhaa zetu, tunaongeza ajira, tunakuza wigo wa kuongeza kodi. Kwa hiyo, tuliangalie

eneo hili la kilimo na viwanda, ni namna gani tutachochaea ili wananchi waweze kupata mikopo ya bei nafuu, huku tukiwa tumewaambia vijana wajajiri? Anajajiri vipi kama bado hawezি kujisimamia mwenyewe na akienda kwenye benki za kilimo riba ni kubwa ambayo mama amesema itakuja kupunguzwa? Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha aliangalie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Wizara na bajeti nzuri ambayo imesikiliza mawazo ya Wabunge wote. Wabunge walismama katika Wizara ya TAMISEMI ilipokuwa inawasilisha bajeti yake, wakawa wanatetea sana suala la Madiwani. Limechukuliwa vizuri sana, wameleta hapa ufumbuzi kuhusu posho za Madiwani. Mama amelipokea, amelielewa na atatekeleza kwa mujibu wa taarifa hii ya bajeti iliyosomwa. Ameelekeza kwamba Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI wataenda wakakae.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe tu Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI wanapokuja kukaa pamoja kuangalia Madiwani hawa wanaangaliwaje, waweze kuangalia na lile jambo ambalo kuna Madiwani wanalipwa, ni posho tu inalipwa lakini hawawekewi nauli. Unakuta kuna mtu anatoka kwenye kata yake mpaka anakoenda kwenye Halmshauri ambapo kikao kipo ni kilometra 30, lakini mtu anayetoka kilometra 60 atapewa nauli, sawa; atapewa na pesa ya kulala sawa; sasa huyu mtu ambaye hata kama atatembea kilometra tano, analipwa nini? Waweze kukaa wawapatie pesa hizo za nauli hawa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwa hali ilivyo sasa hivi, watu kutembea kwa muda hata wa nusu saa ni kama unapoteza muda. Mambo ni mengi. Kwa hiyo, tujaribu kuwa tunarudisha nauli za hawa Madiwani ambao wanatoka kilometra 20 kilometra tano waweze kurudishiwa. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI ambao wameagizwa na mama yetu kipenzi, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakakae pamoja, waweze kuangalia suala hilo la nauli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma ajiandae.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nami napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa kutupatia na kufanya kazi kubwa sana ili kuikamilisha hii bajeti ambayo tunajadili kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile muda siyo rafiki napenda kuingia moja kwa moja katika mchango wangu. Napenda kuzungumzia mambo mawili; la kwanza ni uchumi kwa ujumla wake na la pili suala la ubunifu na ajira, kwa sababu sehemu nyingi wenzangu ambao wamenitangulia wamezigusia na kwa kweli sina haja ya kuyarudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na janga kubwa la Uviko 19 liliokabidili dunia nzima Tanzania imebahatika; na siyo bahati, kwa mkakati na kwa mpango mzuri tumejaaliwa uchumi wetu kukua kwa asilimia 4.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nchi ambazo zinatuzunguka Kusini mwa Jangwa la Sahara nchi zote kwa wastani chumi zao zimepungua, zimekuwa hasi, zimepungua kwa asilimia 1.9. Na kwa ulimwengu kwa ujumla wake chumi zimepungua kwa asilimia 3.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika kabisa, na iko bayana kabisa, kuna jambo ambalo sisi tumeweza kulifanya vizuri katika Janga hili la UVIKO-19 na ikatuwezesha uchumi wetu kukua kulinganisha na chumi nyingine zote za ulimwenguni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimechukua fursa ya kutazama makampuni yetu makubwa yameendeleaje katika kipindi hiki. Nimechagua kampuni zifuatazo; *TBL*, *TCC*, Vodacom, Tigo na *Puma Energy*, kwa makusudi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiziangalia hizo kampuni, ndizo kampuni ambazo zinatupa kodi kwa wingi; *TBL*, *TCC*, Vodacom na Tigo pamoja na Puma. Kuangalia taswira ya kibashara inakwendaje. Ukiangalia kampuni zote hizo tano, hasa hizo nne za mwanzo, zote mapato yao yamepungua kwa kipindi cha miaka miwili mpaka mitatu sasa na kipindi cha mwaka uliopita mapato (*revenue*) yamepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vodacom *quarter* ya mwisho imepata hasara. Sasa ukiangalia huu uchumi umekuwa katika sekta gani, wakati ukiangalia makampuni haya makubwa mengi yameathirika. Sekta zilizotuwesha uchumi wetu sisi kukua ni ujenzi, madini, mawasiliano, uchukuzi, kilimo na viwanda. Ujenzi asilimia 13, madini asilimia tisa; hayo ndio maeneo ambayo yamekuza uchumi wetu. Eneo la *hospitality*; mahoteli, migahawa na utalii, yamepungua kwa asilimia karibu 14. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiipitia ripoti ya *BoT* ya Desemba, 2020, inaonesha bayana kwamba eneo kubwa la ukuzi wa uchumi ni ujenzi, asilimia 42.6 na kilimo, asilimia 24.6. Theluthi mbili ya uchumi wetu umeshikwa katika hayo maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimetoa haya kama muhtasari. Ili kuitathmini bajeti lazima tuelewe uchumi wetu uko wapi na unakwendaje na bajeti yetu iendane na hali halisi ya huu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 42.6 katika ujenzi imekuwa kwa sababu ya ile miradi ya kimkakati. Fedha nyinyi zimepelekwa kwenye *SGR*, fedha nyinyi zimepelekwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, fedha nyinyi zitapelekwa

kwenye bomba la mafuta la kutoka Uganda. Kwa takribani miaka mitano mpaka kumi sekta hiyo itaendelea kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pato kubwa, asilimia 24.6, katika kilimo ndiyo imetoka hapo. Lakini ukiiangalia bajeti inachangia chini ya asilimia moja. Chini ya asilimia moja inakwenda sehemu ambayo inatupa robo ya pato letu la nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa Waziri wa Fedha ni kwamba bajeti zijazo lazima tuongeze uwekezaji katika sekta hii ili izidi kustawi na izidi kutupa tija. Kama chini ya asilimia moja inatupa robo basi tukiweka asilimia kumi, kama *Maputo Protocol*, hakika uchumi wetu na bajeti yetu na mapato yetu yatakuwa makubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu ubunifu na ajira nilisema ninataka kugusia. Tatizo la ajira Tanzania ni kubwa. Asilimia 70 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 35. Tulisikilize vizuri; asilimia 70 wana umri wa chini ya miaka 35. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani sisi Wabunge kwa *demography* hiyo hatuwawakilishi wananchi wetu, sisi ni wazee wote kwa takwimu na kwa mfano wa hiyo *demography*. Maana yake wachache sana hapa wako chini ya miaka 35, lakini asilimia 70 ndio hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo inaonekana dhahiri kwamba ajira itakuwa changamoto na itakuwa agenda yetu kubwa sana. Tunafanyaje kukabili tatizo la ajira? Maeneo ni haya mawili; la kwanza, kwa Tanzania ni kilimo, la pili ni ubunifu ambao upo kwenye teknolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo sasa ndiyo ninataka nipagusie zaidi. Mwaka 2005 wanafunzi wa *Nairobi University*, Kitivo cha *Computer Science* walibuni *solution* ambayo hii leo ni *mobile money*; mwaka 2005. Ukiangalia uchumi, siyo tu wa Tanzania, wa Afrika Mashariki yote, umetokana kwa

sehemu kubwa na mchango huo. Ukiangalia sasa hivi katika mawasiliano *mobile money* inachangia fedha nyingi sana katika kodi zetu, Afrika Mashariki yote na Tanzania yenyewe. Hilo limetokana na ubunifu wa wanafunzi vijana. Na haikuwa bahati mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hichi *TCRA* ilikuwa inaongozwa na Profesa Mkoma na *BoT*Gavana alikuwa Prof. Ndulu. Hawa maprofesa wawili walikuwa na imani ya kukuza vipaji na ubunifu kabla ya kuongeza mfumo wa kupata fedha Kiserikali. Waliuacha huu ukastawi halafu ndiyo wakawekea mfumo wa *regulation*. Haikuwa bahati mbaya, imefanywa kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika sekta hiyo ni kwamba lazima turuhusu ubunifu ustawi na tuulee. Tusifanye kama yule bata anayezaa yai la dhahabu kila siku tukamkaba yule mpaka lile yai asilizae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hiyo – kama angalizo – kwa Tanzania ukilinganisha na wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndiyo sekta ambayo ina kodi kubwa. Ukilinganisha na Uganda, kodi yake ni ndogo, ukilinganisha na Kenya, kodi yake ni ndogo, Tanzania kodi yake ni kubwa. Na kwa safari hii tunaelewa kwa nini imebidi kuiongeza, lakini hilo ni angalizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ubunifu lazima ilelewe istawi ndiyo tuweze kupata tija. Sasa eneo kubwa ambalo sisi tunategemea kuwapa ajira vijana wetu ni maeneo mawili kwa bahati mbaya bajeti hii haiyapi *support* ya hali ya juu; kilimo na sekta ya ubunifu. Sekta zote hizo zipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Kama tutaiwekea kipaumbele na tutafanya mazingira ya ustawi ili ikue itupe tija zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika kwa hayo machache, ninapenda kuunga mkono hoja na ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mheshimiwa Zuena Bushiri ajilande.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, niwapongeze wasaidizi wake; Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango na Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Na tumeona jinsi anavyoshughulika kwenye sekta mbalimbali; kilimo, elimu, madini na shughuli zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake, Mheshimiwa *Eng.* Masauni, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Watu hawa wamedhihirisha wazi kwamba ni wasikivu, na ni watu ambao wanafikika na wanapokea ushauri ambao wanapewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwapongeze watendaji wa Wizara hii, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu. Lakini vilevile kipekee, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe kwa kuja na ushauri na maoni ambayo yatasaidia katika uboreshaji wa bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kujelekeza kwenye usimamizi, ufuutiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwanza nianze kuipongeza Wizara kwa kasi kubwa ya kupeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii imejidhihirisha wazi kwa sababu zimepelekwa fedha, milioni 500, kwa ajili ya *TARURA*. Lakini vilevile kuna ongezeko kubwa la fedha ambazo zitakwenda baadaye kwenye *TARURA*. Kuna fedha za ukarabati na fedha za maboma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba hizi fedha sasa ni nyangi, na kusimamia miradi hii kutoka Dodoma hatuwezi kufanikiwa. Ushauri wangu ni kwamba tuimarishe sekretarieti za mikoa. Nimpongeze dada yangu, Mheshimiwa Ummy, kwa wazo la kuimarisha sekretarieti za mikoa. Ni wazi kwamba tukiimarisha sekretarieti za mikoa watafanya ufuatiliaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na miradi yetu itatekelezwa kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ikiwezekana marekebisho ya sheria yafanywe; ile Sheria yetu ya Tawala za Mikoa (*Regional Administration Act*) Na. 19 ya mwaka 1997, sheria zile za Serikali za Mitaa na Sheria ya Utumishi. Kwa sababu kwa sasa hivi Katibu Tawala wa Mkoa ni mamlaka ya nidhamu kwa watendaji waliopo kwenye *regional secretariat*, anapokwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa hawezi kumgusa mtendaji yeoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza tukarekebisha sheria hizo ili kuhakikisha tuna usimamizi imara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kusababisha usimamizi imara katika miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili unahusu mradi wa Liganga na Mchuchuma. Nitumie nafasi hii kumpongeza Rais kwa maelekezo yake aliyotoa hivi karibuni akiwa ziarani Mwanza. Rais ameelekeza mambo makubwa mawili; kwanza kupunguza urasimu, na pili, kuondoa vikwazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba ninukuu; “*Tumeimba toka nikiwa Waziri, mpaka leo nimefika hapa nilipo Mchuchuma na Liganga haijatoa matunda.*” (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa maelekezo haya. Mradi huu ni mkubwa na ni kichocheo cha maendeleo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya kusini. Mradi huu ukitekelezwa utaongeza kasi ya mahitaji ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha SGR kutoka Mtwara kwenda Mbambabay. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, ile dhana sasa ya *Mtwara Corridoe* itaonekana. Na utaongeza matumizi ya Bandari ya Mtwara; hapa imeonekana kwamba Bandari ya Mtwara sasa hivi matumizi yake ni machache, lakini Bandari ya Mtwara umefanyika uwekezaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, una bilioni 157 zimewekezwa pale; una mitambo ya kisasa; vilevile sasa hivi inaweza kuhudumia *metric tons* milioni moja, lakini mizigo pale ni michache. Mradi wa Liganga na Mchuchuma ukianza kutekelezwa basi Bandari yetu ya Mtwara itatumika ipasavyo na hivyo kuongeza uchumi wa wana Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kodi ya *VAT*na ushuru wa bidhaa wa vifungashio na mashine za kufungashia korosho na karanga. Sekta ya ubanguaji wa korosho bado ni changa, inahitaji kuendelezw. Na kuna changamoto nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunabangua asilimia 20 tu ya korosho ambayo tunazalisha, tunauza korosho ghafi asilimia 80. Maana yake ni nini; tunapeleka ajira kwa wenzetu. Kama tukibangua korosho kwa asilimia kubwa ina maana tunazalisha ajira, lakini tunaongeza thamani ya korosho yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na kushushwa kodi katika maeneo mbalimbali, kuna sehemu ndugu yangu, Waziri wa Fedha, naomba uiangalie tena. Kuna mashine za kufungashia korosho ambayo ni *HS Code* 8422300; kuna vifungashio *SH Code* 3923210; hivi mmevisahau na matokeo yake wabanguaji wadogo wanapata vifungashio kwa shilingi 3,000 mpaka 3,500. Tukitoa *VAT* kuna uwezekano kabisa wabanguaji wadogo watanunua vifungashio hivi kwa shilingi 600. Na hivyo itaongeza uwezo wetu wa kubangua kwa makundi ya vijana na akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana kwamba *VAT*iondolewe katika maeneo hayo ili kukuza sekta

yetu ya ubanguaji na hatimaye tuuze nje korosho zilizobanguliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *export levy* kwenye korosho. Ni matarajio yangu kwamba wakati wa majumuisho Waziri wa Fedha na Mipango atakuja kutuambia kwamba nini kitafanyika katika *export levy*. Na hapa lengo kubwa ni kuchukua sehemu ya *export levy* kwenye korosho tupeleke kwenye sekta ya korosho. Tutoe motisha kwa wabanguaji, lakini vilevile itafute pembejeo kwa wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ni kengele ya kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haya maeneo mawili; *Incentive* kwa wabanguaji na upatikanaji wa pembejeo za kutosha, utasaidia kusukuma au kuendeleza sekta ya korosho ambayo sasa hivi kwa miaka minne uzalishaji unaendelea kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema pale awali, vilevile ubanguaji wetu tunabangua asilimia 20 tu ya kile ambacho tunazalisha. Kwa hiyo namuomba Waziri wa Fedha wakati anafanya majumuisho aliangalie hili na atueleze waziwazi kwamba sehemu ya *export levy* itapelekwa kwenye sekta ya korosho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu yangu ya mwisho ni suala na Madiwani na Udiwani. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumza vizuri kabisa, kwamba Madiwani ni Wabunge katika kata zetu. Madiwani wanafanya kazi nyingi, wana changamoto nyingi na wanafanya kazi zetu nyingi wakati sisi Wabunge hatupo majimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Serikali kwa kuamua kulipa posho kutoka Hazina. Lakini bado kuna kazi ya kufanya hebu tukiangalie kile anachokipata Diwani. Kama kweli ni Mbunge wa kata tumuongezee maslahi yake, tuongeze posho yake ili aweze kutekeleza majukumu yake

vizuri, ili aweze kufanya kazi yake vizuri. Asiwe omboomba kwa wakuu wa idara, asiwe mnyonge kwa mkurugenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukiwa na Madiwani dhaifu kutakuwa na halmashauri dhaifu, tukiwa na Madiwani imara tutakuwa na halmashauri imara. Kwa hiyo, naomba, uamuzi wa kupia posho zao kutoka Hazina ni mzuri lakini twende mbele zaidi tuangalie kile kinachotoka Hazina ni shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wengi baada ya kuingia kwenye Udiwani wamepata mikopo kama tulivyoofanya sisi Wabunge. Kwa hiyo, Madiwani sasa hivi wanapata kitu kidogo sana. naomba turekebishe ili na wao ukifika mwisho wa mwezi wawe na *appetite* ya kuangalia kwamba nini kilichopo kwenye akaunti zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo tutawahamasisha Madiwani, watakuwa madhubuti, wataweza kuwa na ujasiri wa kuwahoji watendaji na kumsimamia mkurugenzi. Lakini tukiwa na Madiwani ambao vipato vyao ni vidogo, hawana kipato cha kutosha, watakuwa dhaifu na hivyo wao watakuwa kazi yao ni kuitikia kile ambacho kimewasilishwa na wakurugenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais tunasema ameanza vizuri mno. Huku mtaani kauli ni kwamba Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi, kule kwetu tunasema Mheshimiwa Rais ameanza na

mguu wa kutoka na mguu wa kutoka Mtume ameuombea. Mambo mengi ya awali kabisa ambayo Mheshimiwa Rais ameanza kuyafanya yanatupa imani kwamba nchi ipo kwenye mikono salama na sasa Mama ndiyo ameshika usukani na tunako elekea kunatupa matumaini makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, milioni 500 kwa kila Jimbo kwa ajili ya *TARURA* zimefika hata Wilayani Muheza na Mimi na *Engineer* wangu wa *TARURA Engineer* Kahoza pale tumeshajadiliana ziende zikatengeneze barabara zipi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupandishwa madaraja kwa wafanyakazi na ahadi ya ongezeko la mishahara mwakani najua wafanyakazi wanalisubiri hili sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Kaka yangu *Comrade* Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri Injinjina Hamad Masauni, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao kwenye Wizara ya Fedha kwa bajeti hii, bajeti iliyonyooka, bajeti yenye matumaini makubwa na ambayo inaonyesha kwamba Wizara ya Fedha na nchi kwa ujumla ipo pia kwenye mikono salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli *Comrade* Mwigulu ningependa kulisema hili huku namuangalia usoni huku mtaani tunasema hana baya, anafanya vitu vyote, majukumu yote anayoyafanya kwa usahihi mkubwa, shida yake inakuja tu anapoanza mambo yake ya Yanga. Yaani najua amejizuia kwelikweli kutoweka japo Bilioni Tano kwenye hii bajeti kwa ajili ya kuisaidia Yanga kuwa bingwa mwakani, lakini ndiyo hivyo tusingekubali. Nimpe pongezi sana *Comrade* Mwigulu na naamini kwamba hata namna zake za ukusanyaji wa mapato ambazo amezipanga unaona kabisa bajeti yetu safari hii inaenda kutekeleza kwa zaidi ya asilimia 67.9, ambapo bajeti iliyopita ilitekeleza kwa vile inaonyesha kwamba kasungura kake katakua kakubwa safari hii. Nimpongeze kwa mara nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache tu ya kuweka kwenye bajeti hii kwa vile kama nilivyosema bajeti imetimia kusema ukweli, lakini ningeweza kuongezea hakuna ziada mbovu waswahili wanasema na la kwangu ninalotaka kuliweka ni kuhusiana na mifuko yetu ya uvezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tovuti ya uvezeshaji tunayo mifuko 45 ya uvezeshaji. Hakuna namna tukawa na mifuko 45 na majukumu yake yasiingiliane kwa namna moja ama nyiningine. Kuna mifuko ambayo kazi zake zitakuwa zinagongana na kwa namna hiyo inaipunguzia ufanisi na inatupunguzia pia uwezo wa kui-*monitor* kwa kadri ambavyo tulitakiwa tufanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba kuna mchakato wa kuunganisha baadhi ya mifuko maoni yangu ni kwamba mchakato huu uongezewe nguvu na ufanywe kwa makusudi makubwa kabisa mifuko mingi zaidi iunganishwe ili mradi tuwe na mifuko michache ambayo tunaweza kuvisimamia, pia ambayo tutahakikisha kwamba ufanisi wake unakuwa wa kiwango cha juu kama lengo la kuanzishwa kwake liliyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mifuko hii 45 hatuna hata mfuko mmoja wa ubia *venture fund* ambacho kimsingi tuna mifuko ya dhamana kwanza hakuna taarifa za kutosha kuhusu uwepo wake, takwimu zinaonyesha kwamba ni asilimia 30 tu ya wananchi wanaufahamu kuhusu mingi ya mifuko hii kati ya mifuko hii 45. Kwa hivyo, haifanyi kazi yake na kuna mifuko ambayo inafikisha mpaka mwaka mzima hajjaweka fedha popote na inachofanya ni kuweka fedha benki ili ku-*play safe* isipate hasara, sasa hili siyo lengo hasa la kuanzishwa kwake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna biashara nyingi huku kwenye *field* uraiani ambazo kimsingi zinachohitaji siyo tu kupewa mikopo na ikusanywe baadaye, lakini kinachotakiwa hasa ni uvezeshwaji wa moja kwa moja. Biashara nyingi zinafanywa na wajasiriamali ambao hawana kweli ufahamu wa kutosha kuhusiana na biashara na tunaishia tu kwenye

kukopesha vijana kwa kutumia mifuko ya Halmashauri, lakini wanafanya miradi ya boda boda na miradi ya kuku na unapata malalamiko mengi kuhusiana na ufanisi wa mifuko hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijawahi kukaa siku tatu kwenye Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Muheza na nisikutane na malalamiko, mawili ndiyo yanakuja sana *either kwamba mifuko hii haijawafikia watu wengi wanakuja watu wengi ambao wametekekeleza vigezo vyote* lakini wanashindwa kupata mkopo kwa sababu sasa ukiwa na milioni 200 ambazo unatakiwa kuwakopesha makundi yote haya matatu unawakopesha vijana wangapi katika wananchi takribani 300,000 wa Wilaya nzima ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusiana na wanaopata mikopo hii lakini wanashindwa kuirejesha na hii inatokana na uwezo mdogo wa namna ya kuwekeza kwa hiyo unakutana na kwamba...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ni ya kwanza?

NAIBU SPIKA: Ni kengele ya kwanza.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, unakutana na suala kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri anamshtaki raia kijana kutoka Wilayani kwako kwa vile wameshindwa kufanya marejesho sasa unakaa katikati unataka marejesho yafanyike ili watu wengine zaidi wafaidike na mikopo hii, lakini juu ya yote hutaki mwananchi wako apelekwe mahakamani kwa kukosa kurejesha mikopo. Kwa hiyo, unakuta upo mahali kama mwanasiaya, kama mtumishi wa wananchi ngoma yako inakuwa ngumu, kwa vile lengo la mikopo hii ikafanye kazi iliyokusudiwa, lakini irejeshwe, lakini kwa sababu hatuna upeo wa kutosha kuhusiana na biashara tunazotaka kuzifanya inaishia kupotea hewani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita nilimsikia ndugu yangu Waziri Patrobass Katambi anasema Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa imetoa shilingi bilioni 4.9 na kat i ya hizo zillizorejeshwa ni shilingi milioni 700 peke yake, bilioni 4.2 imepotea hewani, hakulisema lakini nina wasiwasi hata yeye anaamini hiyo hela haitarudi na kazi ya Serikali ni kuhudumia wananchi wake, sasa utashindana na wananchi kwenda nao mahakamani kila wakati mpaka lini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba sasa ni wakati wa kuzihusisha taasisi binafsi za fedha zitusaidie kufanya jukumu hili badala ya kuwakopesha tu na kukusanya mikopo hii kwa wananchi sasa tunachotakiwa kwenda kufanya ni kuwashirikisha kwa kuwa na ubia kat i ya Serikali, taasisi binafsi za fedha na wananchi hawa wajasiriamali ili kuhakikisha kwamba mikopo hii, haiwi ni mikopo lakini inakuwa ni uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ny ingi kwa mfano za Katani kule Kigombe, Ngomeni, Pande, Darajani, Wilayani Muheza hata ukiziambia zirudishwe baada ya mwaka mmoja zinakuwa bado hazijakomaa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katani inaanza kuvunwa baada ya miaka mitatu unampa mtu mkopo ambao anatakiwa kurudisha baada ya miezi kadhaa anazipata wapi, inabidi atoe kat i ya hizo hizo kuanza kufanya marejesho. Kwa hiyo tukiwa na *venture fund* zitasaidia kwa sababu tunachoenda kufanya sasa inakuwa ni kuwekeza kwa pamoja kat i ya Serikali, taasisi hizi binafsi za fedha na wajasiriamali wale wadogo na marejesho yake yanaenda kupanua zaidi mifuko yetu hii na itasaidia watu wengi zaidi kuliko ambavyo inafanya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halitoki tu hewani lip o katika *SME Policy* ya nchi yetu ya mwaka 2003 na nchi ambayo inafanya vizuri mifuko hii kwa ubia ni Ghana na Ghana walipata sera hii kutoka kwetu, sasa sisi tulian dika lakini hatujawahi kuifanyia kazi wenzenet wameichukua na inafanya kazi sawa sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naomba niseme kwamba naunga mkono hotuba ya bajeti ya Waziri Mwigulu na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuwena Bushiri tutamalizia na Mheshimiwa Kasalali Mageni.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuibadilisha historia ya Tanzania kwa kuwa Rais wa kwanza Mwanamke katika nchi yetu, pia nimpongeze Mama yetu kwa kutuletea bajeti ya kihistoria, bajeti ya mwanamke katika Taifa letu la Tanzania. Kule Kilimanjaro wanasema bajeti hii ina mshiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mawaziri, nimpongeze Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na Watendaji wake wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi nianze kuchangia katika Sekta ya Nishati. Nimpongeze Rais wetu kwa kusikiliza kilio cha Watanzania wengi ambao Wawakilishi wao ambao ni Wabunge wakaja kulia kilio hiki katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu suala la zima la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kutoa tozo la nguzo la umeme kuanzia shilingi 327,000 hadi 27,000, Tanzania bila giza inawezekana. Wote tunaelewa kwamba umeme ndiyo chachu ya maendeleo, Tanzania bila umeme hakuna Tanzania ya Viwanda, vijana wetu wengi wamefanya kazi nyingi sana katika nchi hii lakini mara nyingi sana wamekuwa wakimbia mijini kwenda kutafuta ajira. Baada ya Sera ya umeme vijiji vijana wengi wamepata ajira

katika vijiji, wamejajiri na hata wengine wameajiri wenzao tuipongeze Serikali katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunao wanawake wengi ambao wanajishirikisha katika biashara za mama lishe, wanawake hawa nao wamefaidi umeme vijijini kwa kuwa wameweza kutengeneza mazingira ya kuboresha biashara zao kama vile kutengeneza juisi na hata kuwa na friji kwa ajili ya kuhifadhi vyakula vyao. Niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipongeza Serikali kupitia nishati nije suala zima la Madiwani. Wote tunatambua kwamba Madiwani wana kazi nyingi sana katika Kata zao nani wawakilishi wetu ambao wanafanya kazi nyingi sana katika maeneo yao. Niipongeze Serikali kupitia Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha Madiwani ambao sasa fedha zao zitakuwa zinatoka Serikali Kuu badala ya Halmashauri zao. Hii itawaletea nguvu sana kwa kuwa watakuwa wanapata fedha zao kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi niiombe Serikali yangu siku tunatambua kazi nyingi wanazozifanya Madiwani katika maeneo yao ikitokea misiba wataombwa majeneza, ikitokea shughuli wataombwa hiki na kile, kukiwa na wagonjwa wataombwa usafiri ni hela hizi hizi, posho hii hii ambayo ndiyo wanayoitumia. Niiombe Serikali yako sikuwa iwaongezee posho Madiwani hawa, naungana na wenzangu wote waliochangia hili kwamba ni vizuri Serikali ikawatazama sasa na wao waweze kuongezewa posho ili angalau waweze kuendesha shughuli zao vizuri na kwa amani katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije suala la *TARURA*, niipongeze Serikali Wabunge wengi sana hasa wa Majimbo wamekuwa wakilia kilio cha *TARURA* humu ndani tukiwepo na sisi wanawake wa Viti Maalum. Wengi wameongea mengi kuhusu suala la barabara, bila barabara hakuna maendeleo, wakulima kilimo kinahitaji barabara, wananchi wenyewe tunahitaji barabara, wameongea wengi wakasema kwamba

hata akina mama wengine wakati wakijifungua wanajifungulia njiani kwa sababu ya barabara zetu kuwa mbovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa mwanamke siku zote mwanamke huwa anaangalia mtoto analia nini, mama ameweza kuangalia nini watanzania wanacholilia akajaribu kuleta bajeti hii katika Bunge hili ambalo kila Mbunge amefurahia bajeti hii na kwa kupitia Bunge hili Watanzania wengi kila mtu amefarijiha na bajeti hii. Niseme kwamba tozo kwa ajili ya barabara ya *TARURA* ambayo zaidi ya shilingi milioni 222 zikipatikana nakutekeleza malengo kama iliyokusudiwa naamini kwamba 2021/2022 ifikapo mwishoni tutakuwa barabara zetu zote zinapitika kipindi chote cha mwaka. Niombe Serikali ipeleke pesa hizi zikafanye kazi iliyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi niunge mkono hoja. Nasema ahsante sana kwa bajeti hii nzuri. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika bajeti yetu nzuri ya Serikali ambayo kwa kweli ni bajeti imeakisi mahitaji halisi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza sana naomba nianze kwa kuunga mkono bajeti hii nzuri inayotia matumaini. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, kaka yangu Mheshimiwa *Engineer Masauni*, lakini na Katibu Mkuu kaka yangu Tutuba kwa kazi nzuri mliyofanya ya kutuandalia kitu ambacho hata tukikipeleka *site* kinakubalika. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana, sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu

Hassan. Tumetoka Mwanza Wabunge wa Mwanza tulikuwa na ziara na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais na sisi tulikuwa tuna jambo letu Mwanza, amefanya kazi kubwa nadhani watu wote mmeiona. Ameionesha dunia kwamba Tanzania kazi inaendelea, ametia saini ujenzi wa meli tano mpya hii ni historia kubwa kwenye maendeleo ya nchi yetu, kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii yapo mambo ambayo nafikiria niishauri na mimi kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Suala la kwanza niipongeze Serikali kwa juhudilizozifanya katika kuimarisha utendaji kwenye Serikali za Mitaa juhudilizozifanya katika kuimarisha utendaji kwenye Serikali za Mitaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali hiyo haijawaangalia Madiwani tu imewaangalia na Watendaji ikawawekea posho za kuwaongeza morali kufanya kazi ni jambo jema sana linahitaji pongezi, lakini na mimi ninayo maboresho ambayo nataka nishauri. Madiwani tumeamua kuwalipa kutoka Serikali Kuu, mimi pia nimewahi kuwa Diwani wa Kata, kazi za Diwani wakati mwingine kwenye Kata zinakuwa ni kazi za moja kwa moja za kushughulika na wapiga kura kwa sababu ndiyo mtu anayeishi nao muda wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu ya CCM itoke kwenye kuhakikisha Madiwani inawalipa posho kutoka Serikali Kuu lakini na posho hizi ziongezwe zifanane na majukumu ya Madiwani. Madiwani bado wanachokichukua ni kidogo kulingana na majukumu yao, tumeongeza kwa Watendaji tukasahau Madiwani, kuwalipa kutoka Serikali Kuu ni hatua mojawapo nzuri, lakini ni lazima tuwaongeze kipato chao ili wakasimamie vizuri shughuli za maendeleo. Nikuambie kumuongeza posho Diwani ni kuiongeza posho jamii anayotoka Diwani, kwa sababu yeye ndiye anayeshughulika na shughuli za kwenye lile eneo muda wote,

kwa hiyo hilo naomba niishauri Serikali iliangalie kwa jicho la pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetoka kwenye Jimbo la Sumve, Jimbo la Sumve ni jimbo la wakulima na wafugaji, nilizungumza hapa kuhusu mazao ya chakula kama choroko na dengu kuwekwa kwenye stakabadhi ghalani, kitie kilelekeza wakati wa kujadili Wizara ya Kilimo, kwamba Wizara ya Kilimo sasa kutokana na yale waliyoyakubali kwamba wanayaondoa choroko na dengu na ufuta kwenye stakabadhi ghalani waandike barua kwenda chini kuelekeza walilokuwa wamewaandikia barua kuyaweka mazao hayo kuyatoa, lakini mpaka sasa hiyo waraka haujaandikwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huko bado kuna usumbufu wa stakabadhi ghalani ninaomba sasa Serikali kwa sababu tunataka bajeti yetu hii iakisi mahitaji ya wananchi iende ikaondoe migogoro na vikwazo vyta ukusanyaji wa kodi kwa sababu moja ya kitu ambacho kilipoteza mapato ya Halmashauri ikiwepo Halmashauri ya Kwimba ni kuyaweka mazao haya kwenye stakabadhi ghalani. Jambo hili lichukuliwe kipaumbe ili barua ile itoke iende ikabadilishe hili jambo ili tuweze kukusanya mapato tuweze kutekeleza hii mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali sana imeleta pesa kwenye TARURA sasa hivi matatizo hayajaisha lakini walau yamepungua, hata sisi kwenye Jimbo la Sumve kuna barabara ambazo zilikuwa hazipitiki sasa kupitia hii milioni 500 tuliyopewa tumeanza kuzitengeneza zinapitika sasa hii ni jambo jema lakini ili tuongeze mapato lazima vikwazo hivi tuvishughulikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la watu wa Sumve nimekuwa nikilisema kila mara na nilipata matumaini makubwa Mheshimiwa Rais akiwa Mwanza alielekeza kwamba Serikali sasa inapanga kuijenga kwa lami barabara yetu inayotokea Magu kupitia Bukwimba, Ngudu mpaka Hungumarwa kwa kiwango cha lami. Nilipata matumaini

makubwa sana na wakati tunajadili bajeti ya Wizara ya Ujenzi na wenyewe walikuwa wamesha tupangia pesa na kusema wanaanza kujenga kilometra 10, sasa jambo hili naomba nisisitize kupitia mchango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi hii tumekuwa tukiaahidiwa muda mrefu na imekuwepo hii *vote* muda mrefu, sasa nadhani kupitia bajeti hii imefika sasa wakati huu mpango ambaao tumekuwa tukipangiwa kwa muda mrefu sasa na sisi watu wa Kwigwa tuonewe huruma tujengewe barabara yetu hii kwa kiwango cha lami kwa mujibu wa ahadi iliyotolewa ili na sisi tufanane na maeneo mengine. Kwa sababu katika bajeti nzuri kama hii, itakuwa si vema kama bajeti hii itaisha itafika kikomo hatujapata jambo hili nasi walau tuweze kusimama kifua mbele tukisema bajeti ya 2021/2022 ilituangalia kwa jicho la tatu watu wa Sumve tukapatia barabara hii. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni kengele ya ngapi?...

NAIBU SPIKA: Muda wetu umeisha Mheshimiwa malizia.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu umeisha. Nakushukuru sana kama nilivyo sema tangu awali naunga mkono hoja na naomba yale yaliyoahidiwa kwenye bajeti hii yakatekelezwe nasi tutakuwa pamoja na ninyi kwenye kutenda kazi. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna matangazo mawili hapa kabla ya matangazo, Waheshimiwa Wabunge ambaao tutaanza nao mchana Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Athuman

Almas Maige, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, wengine tutaendelea kuwataja kadri tutakavyoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la Wageni sijui kama wapo ama wameshatoka. Wageni wanne wa Katibu wa Bunge, haya siwaoni.

Pia, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Waziri wa Maliasili na Utalii ameandaa ofa maalum ya kutembelea hifadhi ya Ngorongoro kuanzia tarehe 30 Juni mpaka tarehe 02 Julai, 2021.

Waheshimiwa Wabunge wenyе nia ya kutembelea hifadhi ya Ngorongoro mnakaribishwa kutembelea hifadhi hiyo kwa gharama ndogo kabisa ya 450,000 ambayo itajumuisha tozo ya klingilio hifadhlini, usafiri wa basi kutoka Dodoma hadi Karatu na kurudi, malazi ya siku mbili, hoteli ya nyota nne, usafiri wa magari ya utalii na chakula. (*Makof*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili ni punguzo maalum kwa ajili yetu sasa ukikosa nafasi hii sasa sijui utakuwa unataka Wizara ya Maliasili ikufanyeje ili ukashiriki utalii wa ndani. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge tujipange kwenda huko ili tuweze kwenda kusema vizuri kwa wapiga kura wetu ili na wao washikiri utalii wa ndani na ni jambo ambalo tunapaswa kuendelea kuhamasishana sisi, lakini pia wananchi tunao wawakilisha.

Kwa hiyo, mnakaribishwa Waheshimiwa Wabunge kuijandikisha kwenye lile jengo la utawala ile sehemu ya mapokezi, kwa hiyo, mkienda pale Waheshimiwa Wabunge mtapokelewa mtaandikishwa na siku ya tarehe 30 mchana baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge basi safari hiyo itaanza hapo, halafu watakaoenda huko ama niseme tutakaoenda mimi mwenyewe nipo najishawishi japokuwa nishaenda huko ni kuzuri sana Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo tujitahidi twende maana hizi ni gharama za chini kabisa. (*Makof*)

Baada ya kusema hayo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 Jioni leo.

(Saa 07.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Mhe. George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Athuman Almasi Maige ajiandae.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kazi nyingi ambazo anaendelea kuzifanya katika nchi yetu lakini pia hata utengamano wa taifa, kuna utulivu wa kutosha. Naompongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya bajeti nzuri ambayo imetayarishwa na Wizara yake, Naibu Waziri pamoja na timu yake yote. Kwa kweli bajeti hii kila Mtanzania, kwa sisi tunaotoka huko nje kila mtu anaisifia. Imegusa karibu kila

maeneo na matarajio ya watu; kwa hiyo watu wana matarajio makubwa sana na bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba, kutengeneza bajeti nzuri ni jambo moja lakini kutekeleza bajeti hii ni jambo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu kwamba bajeti hii itatekelezwa kwa ukamilifu wake. Isipotekelezwa katika ukamilifu wake maana yake pongezi zote hizi zitakuwa za bure. Kwa hiyo nakusih i sana Mheshimiwa Waziri, bajeti hii ikitekelezwa vizuri Watanzania wanakwenda kukomboka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia habari ya barabara za vijiji (*TARURA*). Ninaipongeza Serikali kwa kuamuzi wa kutoza tozo la shilingi 100 kwa ajili ya kuchangia mfuko wa *TARURA*. Nchi hii inashida kubwa sana, barabara za vijiji zina urefu wa kilomita zaidi ya 108,000; lakini katika hotuba yako umesema ni kilometa 2,250 tu ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami, kwa hiyo utaona kuna tofauti kubwa sana. Na mimi naamini kuongezeka kwa bajeti hii kutaongeza mtandao wa barabara za kiwango cha lami katika Mfuko huu wa *TARURA*; kwa hiyo nakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyangi hizi za vijiji zimedumaza uchumi wetu kwa sababu kule ambako zinakwenda ndiko kwenye uzalishaji wa kilimo. Na utaona kwamba hakuna mahusiano kati ya barabara na maeneo yanayozalisha mazao ya kilimo na maeneo yenye viwanda vyta kuchakata mazao ya kilimo. Kwa hiyo mazao mengi yanaozea porini kwa sababu hakuna barabara ya kupeleka mazao kwenye maeneo ya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana barabara hizi fedha zitoke barabara zitengenezwe ili wananchi wanapofanya shughuli za kilimo na mazao yakipatikana yasafirishwe mara moja kwenda kwenye maeneo ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwenye upande wa kilimo. Tunaamini kabisa kama asilimia 65 ya uchumi wetu unategemea kilimo. Ningeshauri sana Serikali tujikite kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kinaweza kutukomboa kwa sababu kama unafanya kilimo cha umwagiliaji unawenza kuvuna mara mbili au mara tatu kwa mwaka; Badala ya kutegemea kilimo cha mvua ambacho mnategemea kuvuna mara moja na huna uhakika kwa sababu mvua inaweza kuwa nyingi, kuna maeneo mengine mvua inakuwa hakuna. Kwa hiyo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ni lazima Serikali itenye maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na hapo ndipo kufanyike kilimo cha kutosha. Kwa hiyo naomba sana Serikali kupitia bajeti ya kilimo Wizara ya Kilimo basi tushughulike sana na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, papo maeneo mengi yenye maji ya kutosha. Tulikuwa tunapita juzi kutoka Singida, kuna mabwawa yamezagaa huko njiani lakini maeneo yanayozunguka mabwawa hakuna hata mchicha, hakuna mtu anashughulika hata na mchicha tu pale. Sasa ni lazima tubadilishe *mindset* ya watu wetu, yale maji ya kwenye mabwawa yanayozagaa hovyo katika nchi yetu tuyatumie *effectively*. Kama ni elimu basi itolewe kupitia Wizara yetu ya Kilimo, watu wayatumie vizuri yale maji. Lakini matokeo yake yale maji mpaka yatakauka, yatatumiwa na Wanyama, hakuna mtu anayeshughulika hata kulima mboga maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo uchumi wetu hauwezi kuendelea kwa sababu hata maji yale machache tunayoyaona barabarani hayatumiki vizuri. Kwa hiyo naomba sana elimu itolewe ili wale watu wanaoishi katika maeneo yanayozunguka maeneo ya maji basi wafanya kilimo cha umwagiliaji. Lakini pia kwenye kilimo bado haitoshi kama hatutakuwa na mbegu bora. Shida kubwa ya nchi yetu hatuna mbegu za kutosha ambazo ni mbegu bora. Naomba tujikite sana kwenye utafiti, wataalam wetu watafiti sana habari za mbegu. Tunatakiwa kuwa na mbegu bora ili tuweze kupata kilimo chenye tija. Tunaweza

kuwa na maji, tunaweza kuwa miundombinu mizuri ya umwagiliaji lakini kama tuna mbegu ambazo hazina tija tutaendelea kupiga *mark time* hatutapata mazao ya kutosha kwa ajili maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mbegu ni jambo ambalo Serikali lazima litoe kipaumbele. Mbegu inayopatikana sasa haitoshi, na hata hiyo kidogo inayopatikana inauzwa kwa bei ya juu sana ambayo watu wetu asilimia 90 hawawezi ku-*afford* kabisa. Kwa hiyo ni lazima tutafute mbegu za kutosha, mbegu bora, na ikiwezekana Serikali itoe *subsidy* ili watu wazipate katika bei ambayo wanaweza ku-*afford*, na hasa watu wetu ambao wako kwenye maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali kwa ajili ya kuwakumbuka Waheshimiwa Madiwani. Sisi wote tunatoka kwenye halmashauri zetu, tunaona namna Madiwani wanavyohangaika. Wakiitwa kwenye vikao mbalimbali wanageuka kuwa ombaomba kwa sababu hawana fedha za kusafiria kwenda wilayani. Kwa hiyo lazima either wamuombe Mbunge au nani, hii kitu inawadhalilisha Madiwani. Madiwani ni watu waliochaguliwa kama sisi na wananchi, hivyo lazima Serikali ione umuhimu wa Waheshimiwa Madiwani. Na sisi Wabunge mara nydingi tunawatumia Madiwani kutusaidia kupita kwenye chaguzi zetu, kwa hiyo tuna kila sababu ya kuwatetea. Namimi nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya uamuzi wake wa kuamua kwamba sasa walipwe kuitia Mfuko Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua zipo halmashauri ambazo zipo hoi kabisa katika nchi hii, na hazina vyanzo vya mapato vya kutosha. Kwa hiyo kila siku Waheshimiwa Madiwani wanakwenda vikao wanakopwa. Wengine wanamaliza muda wao wanakuwa hawajalipwa posho nydingi tu, na mpaka leo wanadai kwenye halmashauri. Lakini si kwa sababu labda ya ujeuri Mkurugenzi, kwa sababu halmashauri hazina vyanzo vya kutosha. Kwa hiyo jambo hilo naomba lizingatiwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia upande wa afya, kuna maboma ya Vituo vya Afya, Zahanati ambayo yamekaa zaidi ya miaka mitano mpaka 15. Wakati umefika sasa Serikali iende ikamalizie haya maboma. Tuna maboma ya zahanati zaidi ya 8,000, maboma ya vituo vya afya zaidi ya 1,500 katika nchi hii. Haya yote yangekuwa yanafanya kazi huduma za afya ingeboreka Zaidi, lakini yote yapo na haya yamejengwa kwa nguvu za wananchi. Wamefika mahali wameshindwa, sasa Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuboresha ama kumalizia haya majengo ili huduma za afya kwa wananchi ziweze kuwa za uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, nataka nizungumzie eneo la Bodi ya Mikopo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, amezungumza vizuri sana, akasema mikopo wanayopewa wanafunzi si hisani, ni fedha ambayo baadaye wanatakiwa kuirudisha, na zipo taratibu za kuzirudisha fedha hizo, kwa hiyo siyo hisani. Hata hivyo idadi wanaonufaika na mfuko huu bado ni ndogo sana, idadi ya wanaobaki wanaoachwa bila ya kupewa mikopo na wakiwa na sifa ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana Bodi ya Mikopo ijaribu kupanua wigo. Mheshimiwa Waziri amezungumza habari ya kuwaongezea bajeti Bodi ya Mikopo, hii itasaida vijana wetu wengi kujiunga na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, utaratibu wa kuwatambua wanufaika bado mimi nauona una kasoro kubwa sana. Wapo vijana wengi ambaao kweli wanahitaji na wanasifa za kupewa mikopo hiyo, lakini kwa sababu mbalimbali hawapewi mikopo. Kwa hiyo bajeti ikiongezeka kwa vyo vyote vile vijana wengi watapata mikopo na wataweza kujiunga na Elimu ya Juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipongeze uamuzi wa bodaboda. Watu wengi wanaoishi mjini wanafanya biashara za bodaboda; na vijana wengi ndio wanaohusika. Anakuwa aidha amepewa bodaboda na mtu au yeye

mwenyewe kajikusulu kanunua bodaboda. Na kwa sababu ya wingi wa bodaboda uliopo, biashara ya bodaboda bado hailipi sana. Kwa hiyo ilipokuwa inafikia hatua ya kumtoza faini ya Shilingi 30,000 kwa kosa la barabarani, sawa sawa na mtu aliyekosea anayeendesha lori haikuwa sawa kabisa. kwa hiyo nataka nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hilo na kuwapunguzia adhabu ili angalau tujaribu kuwasaidia waweze kujikwamua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almasi Maige, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya mwaka 2021/2022, bajeti ambayo ina mpango wa namna gani tunakwenda kukusanya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni ya kwanza katika Mpango wa Miaka Mitano tuliojiwekeea, ni bajeti ya kwanza ya Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa Awamu ya Sita yenye maelekezo mengi, yenye matumaini makubwa kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inakwenda kujibu kero na vilio vya Watanzania wa aina mbalimbali. Kwa mfano inakwenda kuweka matumaini makubwa kwa watumishi kwa sababu tunaona kuna mpango wa kuwapandisha vyeo watumishi wapato 92,619 pamoja na kwenda kupunguza makali ya Maisha kwa sababu inakwenda kupunguza kodi kutoka asilimia tisa mpaka asilimia nane. Tunamshukuru sana mama, hongera sana. Pia itajenga mazingira mazuri kwa watendaji wa vijiji na makatibu tarafa kwa jinsi ambavyo itawarahisishia kazi zao, kwamba

sasa wanakwenda kuwekewa laki moja ili iweze kuwarahisisha katika utendaji wao wa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuwapa nguvu na *confidence* viongozi wetu wa siasa, Madiwani kwa kuwa sasa wanaweza wakasimamia miradi ya halmashauri bila kubabaishwa, bila ya kuwanyenyekoa wakurugenzi wala wataalam. Wataweza kusimamia miradi ya Wakurugenzi kwa kuwawekea posho zao moja kwa moja kwenye akaunti inayotoka Hazina, hongera sana Mama. Lakini pia inampango mzima wa kuweza kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji waje wawekeze. Pia utaratibu mzuri kwa wafanya biashara kuweze kulipa kodi kwa hiyari yao wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa Watanzania walio wengi matumaini ni makubwa kwa sababu bajeti hili imewaonesha jinsi ya kwenda kuboresha huduma za jamii. Kwa mfano itaendelea kutoa elimu bure kuanzia *form one* mpaka *form four*. Tunapongeza sana, lakini mpango mzima wa kwenda kukamilisha vijiji ambavyo havijapata umeme katika mpango huu vijiji vyote Tanzania vinakwenda kupata umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni kichocheo cha maendeleo, nimpango mzuri sana. Tunajua umeme umepunguzwa *Rural-Urban Immigration* ambapo vijana walikuwa hawapenda kukaa vijiji. kwamba ni afadhali acae Machinga Mjini kutokana na kukosa umeme, kwamba anaona ametengwa na dunia anashindwa kuingia *internet*. Lakini vile vile imeweza kuchochea viwanda vidogo vidogo kama saluni huko vijijini, viwanda vyta ma-*grill*/pamoja na pia kuwasaidia kina mama amba walikuwa wanakwenda mbali kwa ajili ya kwenda kusaga mahidi wakifuata umeme mijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna mpango mzima wa kuboresha barabara, hasa hizi za *TARURA* pamoja na *feeder roads*; ni kichocheo kizuri sana miundombinu ya barabara. Hata hizi pembejeo tunazo sema zinafika kijijini

kwa bei kubwa sana kutokana na miundombinu ya barabara ambapo ni mbovu. Kwa mfano Serikali inatoa bei elekezi kwa ajili ya mbolea, lakini mbolea mpaka ifike kijijini bei yake imekuwa mara dufu kutokana na matatizo ya barabara. kwa hiyo kuna umuhimu sana wa kuimarisha barabara, *feeder roads* pamoja barabara hizi za *TARURA*. naomppongeza sana Mama yetu kwa kutoa *top up* licha ya bajeti ya *TARURA* lakini sasa imeongezwa milioni 500 kwa ajili ya kwenda kuboresha barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, ili kuweza kufikia ndoto hii sasa ya kutoa huduma bora kwa Watanzania pamoja na makundi mengine ni lazima sasa tuweke mkakati wa kupata mapato; kwa sababu bajeti yetu ni *cash budget we expenditure* kila ambacho tunaki-collect.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomppongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa jinsi ambavyo amekuja na vyanzo mbalimbali vyta kukusanya mapato. Kuna vyanzo vyta zamani vinaendelea lakini pia nimeona vyanzo vipyta. Vyanzo vingine kama jinsi utakapopata *property tax*, kodi ya majengo watu wamechangia najua ni msikivu atakwenda kuboresha kwa namna gani anakwenda kukusanya mapato hayo ambayo hayana kero kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ameweka vipaumbele, kwamba namna hii ya kwenda kukusanya mapato kipaumbele cha kwanza ni mapato yetu ya ndani na yanayotokana na kodi, tozo na ushuru, na sehemu nyiningine ni mkopo wenye masharti nafuu na misaada. Sasa, kama kipaumbele cha kuendesha miradi yetu ni mapato ya ndani kwa hiyo sisi hatuna budi kuwekeza katika sekta hizi za kiuchumi, ikiwepo kilimo, mifugo, maliasili na madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipongeza sana Serikali kwa sababu hata bajeti, kwa mfano nikichukulia mfano wa kilimo; tumeongeza bajeti ya kilimo kwa asilimia 22 lakini bado bajeti hii inaonekana haitoshi kwa sababu ukiangalia kwenye *gross budget*, bajeti yote ya Nchi nzima bado kilimo inakwenda kwenye asilimia 0.8 kwamba iko chini

ya asilimia moja. Tunavyoweza kuboresha kilimo; kwa sababu tatizo kubwa kwenye kilimo ni uzalishaji mdogo. Kwa mfano tungeweza kuboresha uzalishaji katika kilimo, faida moja wapo tunayopata ni uhakika wa chakula. Tunapokuwa na uhakika wa chakula basi tunakwenda kumudu *inflation*, na vile vile tunakwenda kufanya *serving*, kwamba sasa vyakula ambavyo tulikuwa tunategemea kuagiza kutoka nje ikiwemo mafuta, watu wengi wamechangia, ngano na sukari. Tunatumia hizi fedha kupeleka kwenye miradi ya vitu vingine; kwa hiyo ni faida kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunajua kwamba kilimo kinatoa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu. Kwenye viwanda tutapata ajira, tutakusanya kodi, tutakwenda kuongeza mnyororo wa thamani na hivyo tutapata fedha. Kwa hiyo hatuna budi kuwekeza katika sekta hizo ikiwemo kilimo pamoja na sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mazao ya kilimo yanakuwa hayajafikia malengo kwa sababu, kwanza kuna upungufu mkubwa wa huduma za ugani. Tumeona kwamba sera ya nchi ilikuwa kila ni kijiji kupata Afisa Ugani mmoja wa kilimo na mmoja wa mifugo. Lakini tukiangalia kuna upungufu mkubwa sana kwa maafisa kilimo, tuna maafisa kilimo takriban 6,700 ilhali wanaotakiwa ni 21,288. Hii inaonesha kwamba *ratio* ya Afisa Kilimo mmoja ni kuwahudua wakulima 600. Hatuwezi kufanya maajabu au mapinduzi makubwa kwenye kilimo kama tupo hivi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, japo naipongeza sana Wizara kwa sababu pia imetenga fedha kwa ajili kuboresha huduma ya ugani, imeweke bilioni 11.5 kwa ajili ya kununua pikipiki 1,500 kwa ajili pia ya kuwapa maafisa kilimo *extension kit* pamoja na *soil test kit* lakini bado hizi 1,500 hata si robo bado vitendea kazi vinatakiwa kwa maafisa ugani. Mimi nilikuwa naomba kama kuna uwezekano kitengo hiki kiongezewe bajeti kutoka kokote itakavyopatikana ili Watanzania walio wengi ambaao ni wakulima waweze kufikiwa na huduma za ugani. Lakini vile vile Maafisa Ugani

waajiriwe. Kuna halmashauri nyingine hali yao ni mbaya sana kwa ajili ya upungufu wa huduma hizi za ugani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na tatizo la pembejeo, mimi naisifu sana Serikali kwa sababu imeongeza bajeti ya kituo cha utafiti ili waje na mbegu bora ambazo zitakuja kuzalishwa na ASA, hata ASA imeongezewa bajeti. Bajeti ya utafiti imeongezwa kutoka bilioni 7.5 hadi bilioni 9.9. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Utafiti vina kazi nyingi tunahitaji utafiti kwenye kilimo. Kwa mfano licha ya mbegu pia wanatakiwa kutufanya utafiti wa *agroecological zone*, tujue ni mazao yapi yanatakiwa kuzalishwa wapi, tunatakiwa kufahamu hali ya rutuba ya udongo. Wakati mwingine tunamshauri mkulima apande na *dup*, nani anayefahamu kwamba pale kulikuwa shida ya *phosphorus*, ndio maana mkulima anaingia gharama kubwa, anatumia hiyo *dup* lakini *at the end of the day* bado matokeo ni madogo. Kwa hiyo tunahitaji utafiti tusibahatishe hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imeongeza maradufu bajeti ya Wakala wa Kuzalisha Mbegu (ASA), kutoka bilioni 5.4 hadi bilioni 10.5. Tunaiomba ASA sasa isimamiwe, izalishe ile mbegu inayohitajika.

Kuna mbegu kwa mfano za alizeti, mkulima atahangaika atavuna alizeti, lakini gunia zima la alizeti akienda kukamua anaenda kupata lita ishirini, ndoo moja. Kwa hiyo tunahitaji wazalishe mbegu chotara ambazo kweli zinakwenda kukidhi. Mtu anavyotoa jasho kwamba anaenda kufanya kile kilicho bora, pamoja na mbegu ya ngano nashairi, mbegu ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Watanzania wengi kwa mfano Kanda ya Kusini kule wanatumia mbegu za mahindi za Zambia, ambazo ni za Kampuni za SEEDCO na Mosanto pamoja na watu wa Kanda ya Kaskazini...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshalia Mheshimiwa.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga hoja mkono. (*Makof*)

MHE. NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed ajiandae.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa kuchangia bajeti hii ya mwaka 2021/2022. Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kukamata usukani wa nchi yetu na kututembeza mpaka hapa tulipofika, nchi imetulia na nchi imekuwa na maelewano mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri wa fedha na mipango, ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara hii kwa kuleta bajeti nzuri ambayo imekuwa ni ya kupigwa mfano, kwa sababu hii ni bajeti ya kwanza kwa Mheshimiwa Rais Samia, lakini watu wameikubali. Mimi ni mmoja wa watu wanaounga mkono bajeti hii, na nina ushahidi wa kutosha kwamba bajeti hii imekuwa na kiasi kikubwa sana cha mambo ambayo Wabunge waliyomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na ukweli kwamba bajeti hii itamalizia miradi ambayo ilikuwa ya kimkakati kama reli ya *SGR*, mradi wa umeme kule Mto Rufiji na mradi wa *REA* wa kupeleka umeme vijiji vyote. Vile vile bajeti hii imetafuta fedha kwa ajili ya *TARURA* ambazo Wabunge tumekuwa tunalia humu kwamba *TARURA* iwezeshwe na tumetafuta fedha kwenye vyanzo vya uhakika ambavyo tutawapa *TARURA* ifanye kazi ya kutengeneza barabara kwenye vijiji ambavyo hakuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia miradi mbalimbali ya kufua umeme, ambao umeme huo utatumika kwenye Mradi wa *REA*. Sasa hivi Mradi wa *REA* hata ukikamilika umeme utakatika kwa sababu uliopo sasa hivi hautoshi, pia miradi mbalimbali ya maji itakamilika. Kuhusu afya bajeti hii imelenga kumalizia majengo na kupeleka vifaa tiba kwenye majengo ya hospitali ambayo sasa yapo, lakini hayana vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za majimbo. Hii ni bajeti ya kwanza ambayo imetupa hela mkononi Wabunge. Kwanza milioni 500 za kujengea barabara, vile vile milioni 600 za kujengea shule katika kata ambazo hakuna shule. Hapa nina maboresho kidogo, fedha hizi milioni 600 kuna majimbo mengine tayari yana shule na watapata hizo hela na kuna majimbo mengine yana kata zaidi ya tano katika kata 20 hazina shule, inakuwa tabu sana. Kwa mfano, jimboni kwangu nina kata mbili, hazina shule za sekondari. Hata hivyo, wenyewe tumeaanza kufurukuta, tumejenga kwa kutumia Mfuko wa Jimbo na michango ya wananchi.

Kwa hiyo ningeomba kabisa mimi hizi hela milioni 600 nizigawe milioni 300 kila kata na tunaweza kumalizia shule ya sekondanri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine ambalo bajeti hii imeligusa, nalo ni kuwagusa waajiri na wafanya kazi. Katika nyanja hiyo, bajeti hii Serikali imependekeza kupunguza *PAYE* kutoka asilimia tisa mpaka nane. Kwa hili tunaipongeza sana Serikali yetu. Pia Serikali imependekeza kwamba waajiri wenyewe wafanyakazi mmoja mpaka wanne sasa wasilipe tena *SDL* kama ilivyokuwa zamani, tumesogezza ile idadi ya chini ya wafanyakazi kuwa 10. Sasa hii imesaидia sana na waajiri wengi watalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna huu Mfuko wa Matibabu au Malipo kwa Wafanyakazi Wanaoumia Kazini, yaani *Workers Compensation Fund*, tumekubaliana kwamba na bajeti imeonyesha kwamba sasa waajiri wa sekta binafsi walikuwa wanalipa asilimia moja watalipa asilimia 0.6. Sisi tuna maoni kwamba ingefaa hizi asilimia 0.5 kwa ajili ya

wafanyakazi wa Serikali au *public*, iwe sawa na kwa ajili ya wafanyakazi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kabisa nina maoni machache, kuboresha tu bajeti hii ambayo nimeisifia kwa ajili ya watu wote. Maoni yangu kwanza. Ni kweli kabisa naamini kwamba *VETA* ingefanya kazi vizuri sana kama ingekuwa chini ya Wizara ya Kazi chini ya Waziri Mkuu, kwa sababu *VETA* maana yake ni kuhudumia watumishi kwa wafanyakazi wa waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza sasa Serikali ijiingize kabisa kabisa kwa ajili ya *blue prints*, tutekeleze mpango wa *blue prints* ambao ungerahisisha kufanya kazi kwa kufanya biashara yaani *easy doing business* hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu tozo za wafanyakazi nimeisemea, kuhusu tozo ya *SDL*. leo tumesimama katika asilimia nne ya mshahara wa mfanyakazi, nchi zote za Afrika Mashariki na *SADC* tozo hii ni ndogo sana. Kwa hiyo hii inatuongezea kuwa na gharama za ufanyaji biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niongelee posho ya Madiwani ambayo Serikali inalipa, itawalipia moja kwa moja Madiwani wetu badala ya kulipwa na Halmashauri. Hii imeleta na imeibua wazo la utawala bora, maana wanaesema mtu anayemlipa mpuliza zumari, anachagua na wimbo wake. Sasa hii watalipwa Madiwani hao kwa hiyo watasimamia Halmashauri zetu vizuri. Naipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matatizo madogo jumboni, lakini sugu kabisa ni vituo vya afya. Jimbo zima lina kata 19, lina kituo kimoja tu cha afya. Nimelisema sana hili mpaka naona aibu kulirudia rudia, kama Waziri wa Afya yupo, Waziri wa TAMISEMI yupo, watusaidie kumalizia majengo kwenye kata ambazo nimezitaja; Shitage, Mabama, Ilolanguru na Usagari ambako tunajenga wenyewe kwa hela

zetu za Mfuko wa Jimbo na nguvu za wananchi. Tuna shida kweli ya hospitali, tungependa sana kama Serikali itaingilia katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naendelea na pongezi kwa Wizara ya Maji, imefanya kazi nzuri sana ya kugawa maji jimboni kwangu na nchi nzima. Hata juzi tumekwenda kufungua mradi huko Misungwi na Mheshimiwa Rais. Wizara hii imefanya kazi nzuri sana nawapongeza sana Mheshimiwa Aweso na timu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala muhimu sana la kilimo. Kilimo ndio uti wa mgongo katika nchi hii, lakini kilimo hakithaminiwi na Serikali kabisa. Wamesema Wabunge wengi hapa kwamba tunapata bajeti nzima ya Serikali kilimo kinachangia asilimia 27. Matokeo yake Serikali inawekeza 0.8 ya bajeti kwenye kilimo na tumesahau kitu kimoja kikubwa sana, nchi hii itatokea vita au ugomvi mkubwa sana kwa sababu Serikali hajjaweka ardhi ya kilimo kama ambavyo tumeweka ardhi ya wanyama yaani hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akishawekwa mwekezaji hapa anataka ekari 200 ziko wapi, hakuna. Anataka hekari 500, hakuna, anataka hekari 10,000 aweze kuweka shamba kubwa na uzalishaji wa tija, hakuna. Matokeo yake wananyang'anywa watu wenye mashamba yao kama vile sijui wamenyang'anywa na matumbo, kwa sababu hawa watu wenye mashamba yao watakula wapi, walikuwa wanalima, inachukuliwa ardhi anapewa mwekezaji. Iko haja ya Serikali sasa kuweka ardhi ya kilimo, *demarcated* kabisa kwamba ardhi ya kilimo ni hii, kama ambavyo tumeweka ardhi ya wanyama ni hii, itatusaidia sana kuondoa migogoro huko mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala hili la kutegemea kudra za Mwenyezi Mungu limepitwa na wakati. Tunangoja mvua zinyeshe ndipo tuvune, kama hazikunyesha hatuvuni na hatuna simu sisi na Mwenyezi Mungu kwamba tuletee maji, tuletee mvua mwaka huu, hatujui, hata Waziri wa kilimo leo hajui kama kesho mvua itanyesha, imekuwa tu utabiri wa hali

ya hewa ambao wanaona mawingu na kadhalika, hakina uwezekano wa kutoboa sisi kilimo bila ya kuwa na kilimo cha umwagiliaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, Serikali ibadilike itoke nje ya *box*, ising'ang'anie kusukuma wakulima na pembejeo tu kwenye maji ambayo hawayajui yako wapi, wakati kila mwaka mvua inanyesha maji mengi yanapita kwenye madaraja na tunakazana kujenga madaraja tu ili maji yapite, tuzuie sasa hayo maji tufanye umwagiliaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia bajeti hii. Naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili nichangie bajeti iliyopo mbele yetu. Nikushukuru wewe na pia nielekeze shukrani zangu za dhati au pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote waliomo kwenye Wizara hii, kwa kweli kazi wanayofanya mwaka huu imeonekana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati ziende kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya aliyoweza kujibu hoja za wananchi mbalimbali kupitia kwa Wabunge wetu kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini watu wanaisifia hii bajeti, kwamba kama kumbukumbu zetu zipo vizuri huko nyuma bajeti kuu ilianza kusomwa kabla ya bajeti za kisekta, lakini Serikali ya Chama Mapinduzi ilikuja kubadilisha ule utaratibu, ili kukidhi matakwa haya ambayo yamekuja na bajeti hii, kwamba bajeti za kisekta yale tulioyachangia yote

ndio yamekusanywa, yameingizwa kwenye bajeti hii. Tunawapongeza sana, tunawapongeza kwamba bajeti imekwenda kujibu hoja za Wabunge na kujibu hoja za Wabunge maana yake ni kwenda kujibu hoja za wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi kwenye bajeti hii tunakwenda kujibu masuala ya afya, elimu, maji, umeme na mambo kama hayo. Kuna jambo moja naomba niliongeze kwenye bajeti hii limesahaulika. Tunalo jambo linalozungumzwa kwa jumla ya uhifadhi wa wanyamapori, lakini hapa tumesahau jambo moja kwamba wananchi wale wanaozungukwa na hifadhi za wanyamapori, wanayaonaje matunda ya moja kwa moja kwa kuwepo kwao kwenye hifadhi. Maana leo tunaweza kuzungumza kwamba hifadhi ina faida kwa inaongeza watalii, na mambo mengine kama hayo ya kuinua uchumi, lakini hayo ni mambo ya mbali sana ambayo yanahitaji elimu kubwa kuyaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali waende waimarishe *WMAs*, hapo ndipo wamesahau kwa sababu zile *WMAs*, wananchi wanahifadhi kwa *WMAs* ni kwamba wanapopata mapato yao wanajenga shule, madarasa, vyoo. Kwa hiyo wananchi wale wanaozungukwa na hifadhi wanapata ile *pinch* ya moja kwa moja kwamba kumbe kutokana na hawa wanyama tunapata faida hizi, kuliko hizo ambazo tunatakiwa Wabunge twende tukajieleza, Waziri aje aeleze. Hivyo, kama Serikali wangeimarisha *WMAs* kwenye maeneo yetu, wananchi wangeweza kupata faida ya moja kwa moja kwa wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye *WMAs* naiomba sana Serikali, kumekuwa na kigugumizi kikubwa sana hata pale ambapo vitalu vyta *WMAs* wakapata wawekezaji, bado yale mafao yao yanakuja kwa kuchelewa sana. Kwa hiyo sasa tunapokwenda kuzunguka kule, wananchi wetu wanapohama mashambani kurudi baada ya kukosa mazao yao, kuliwa na tembo na wanyama wengine wanakosa nini cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana sana, naiomba Serikali, iimarishe WMAs, na kuimarisha WMAs maana yake nini? Kuwasaidia hata kuwatafuta wawekezaji kwenye vile vitalu, vile vile kuvitangaza, unawaachia WMAs watangaze vile vitalu vyao, uwezo wao wa kutangaza ni mdogo sana. Naiomba Serikali kupitia Maliasili waendelee na wao kuitangaza vile vivutio, ambavyo kwenye vile vitalu vinanyomilikiwa na WMAs.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ambalo naweza kuishauri Serikali katika kuboresha hii bajeti yetu. Jana nimeuliza swalii hapa kuhusiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa barabara mbalimbali nchini. Zipo barabara zimefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 2012, mpaka leo tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga. Mfano mmojawapo, kuna barabara yetu ya Nachingwea-Masasi, barabara ya Nachingwea – Liwale, barabara ambazo zimefanyiwa upembuzi yakinifu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini basi Serikali isifikirie sasa isitishe kwanza kuendelea kufanya upembuzi yakinifu ili barabara zile ambazo tayari zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, iweze kupata fedha kwa ajili ya kuzijenga. Jambo hili Serikali imelifanya, mwaka huu imepunguza kujenga vituo vya afya, imepunguza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa sababu gani, wapate fedha za kupata vifaa za kumalizia zile hospitali. Naomba na huku kwenye upembuzi yakinifu wafanyeni hivyo, kwamba wajiridhishe barabara ngapi tumeshazifanyia upembuzi yakinifu, zinahitaji fedha ngapi kuzijenga, basi wakasitisha, wakaacha kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndio mambo niliona kwamba nije kuwashauri kwa maana kwamba, niwashauri ili waone kwamba wanaweza kupoteza fedha nyngi sana za Serikali. Kwa mfano, nafahamu barabara ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2012, tutakapokwenda kujenga mwaka 2025 hatutajenga kwa *data* zile za mwaka 2012. Kitakachofanyika ni *building and*

design, tunapoteza nyingi. Kwa hiyo nashauri jambo hilo dogo sana walifanye kama ambavyo wamefanya katika sekta zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naisifu sana Serikali, tulichangia hapa kutafuta fedha za *TARURA*, kutafuta fedha za maji vijijiini, jambo hili wamekuja nalo vizuri sana, wamekuja kutwambia wameongeza Sh.100 kwenye mafuta; wameongeza tozo kwenye miamala ya simu, jambo zuri, lakini vile vile kwenye *line* ya simu ni jambo zuri. Hizo fedha mpaka leo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hebu ziwe *ring fence* tuzione, kwa sababu zile zilivyo wazi wazi hivi, hazieleweki, haiwezi kuwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu zile Sh.100 tuzione moja kwa moja kwamba zile fedha zinakwenda *TARURA* na hata pale unapoweka mafuta zinaonekana kabisa kwamba imekatwa shilingi kadhaa zimekwenda *TARURA* kama zilivyo kwenye *REA*. Leo ukinunua mafuta kwenye *REA* unaona kabisa kama kuna shilingi kadhaa imeenda *REA*. Unapofanya muamala kwa simu unaona kabisa kuna shilingi kadhaa zimeenda kwenye *REA*, tunataka tuone fedha ya mafuta inakwenda moja kwa moja *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile na zile za kwenye miamala ya simu, tunapofanya miamala ya simu, tuone kwamba hii shilingi kumi imekwenda moja kwa moja kwenye maji vijijiini (*RUWASA*)....

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Hapo ndiyo tutakuwa tumeona vizuri, hiyo ndiyo *ring fence* ambayo nashauri iwekwe, kwa sababu inaweza kutokea....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka kuna taarifa.

Mheshimiwa Maganga naamini unachotaka kusema ni taarifa hasa. Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baba yangu anachangia vizuri sana yaani pesa zikifanyiwa vizuri hesabu za mafuta pamoja na kwenye simu zikaenda mahali husika, Taifa hili tutakuwa hatuna shida tena ya barabara. Ahsante sana, nilikuwa nataka nimpe taarifa hiyo tu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. NAIBU SPIKA: Sasa, Mheshimiwa Maganga rungu litakufuata muda siyo mrefu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zubeir Kuchauka, malizia mchango wako.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama nilivyosema, nilianza kwenye miamala ya simu iende *RUWASA* na hii ya laini iende maji vijijini, hapo tutakuwa tumefanikiwa, kwa maana kwamba hela ya mafuta inaenda *TARURA*, hela ya miamala inaenda *RUWASA*, na hela ya laini inakwenda maji mijini. Huo ndio mchango wangu kwenye bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, mimi ni mionganoni mwa Kanda ya Kusini, kwa hiyo kukaa bila ya kuizungumzia korosho nitakuwa sijafanya sawasawa. Nataka niambie Serikali, mazao yote hakuna zao lenye *export levy* isipokuwa korosho. Lazima tuijulize imetokana na nini hii *export levy* kwenye korosho. Hii imetokana na kikao cha wadau wa korosho. Walipokaa wadau wa korosho wakasema sisi hili zao za korosho lisiendelee kudumaa tufanye nini? Tukaweka fedha kwenye *export levy* ili ziweze kurejea kwenye korosho, lakini Serikali baada ya kuona zile fedha ni nyngi na ni tamu wakazihamisha zote wamebebeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwenye kikao cha wadau wa korosho cha mwaka 2020 tumetoa kwa mkulima shilingi 25/= kwenye kila kilo kwa ajili ya kupeleka Naliendele kwenye Chuo cha Utafiti. Tumetoa shilingi 25/= kwenye kila kilo, tumepeleka kwenye Bodi ya Korosho ili Bodi ya Korosho iweze kusimamia zao la korosho. Sasa Muone hii mizigo yote inarudi kwa mkulima. Tunaomba *Export Levy* irudi kwenye zao

la korosho, hata kama siyo *hundred percent*, lakini mhakikishe angalau hata 50 au 60 zirudi kwenye korosho, vinginevyo zao hili linakwenda kupotea. Nawaomba sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho siyo kwa umuhimu, naomba kuishauri Serikali, tujiondoe kwenye kufanya biashara; tusimamie, tuimarishe Sekta Binafsi. Hatuwezi kuimarisha Sekta Binafsi kama na Serikali nayo itakuwa na taasisi zake zinatamani kufanya biashara. Taasisi zile ambazo zimepewa kusimamia sekta mbalimbali, zenyewe ziwe kama *regulator*. Siziwe na zenyewe zinafanya biashara, tunakwenda kuharibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano, kuna taasisi moja ya *TASAC*, kazi yao ilikuwa ni ku-*regulate* biashara pale bandari, lakini nao pamoja na kwamba tuliwaambia wapitische zile nyaraka za Serikali tu, leo hata ngano pale kwa Bakhresa wanachukua *TASAC*. Tunawashauri, tunaomba Serikali, kama tunataka kuimarisha uchumi wa nchi yetu, lazima watu binafsi tuwabebe. Sekta binafsi lazima tuibebe. Tutafute namna yoyote tunavyoweza, Sekta Binafsi ipate nafasi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana. Huo ndiyo ulikuwa mchango wangu kwa leo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Asya Mwadini Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi nami jioni hii ya leo niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nianze kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri aya ya 77 ukurasa wa 65 unaosema kuhusu Zanzibar. Kwa maneno

aliyoweka ya kunukuu, napendekeza kutekeleza utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na kodi na tozo za Muungano kwenye mapato yanayotokana na viza ili yawewe kutumika pale yanapokusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yanayotokana na tozo na viza za Zanzibar yaonekane kwenye bajeti upande wa Zanzibar kuidhinishwa na kutumika kwa upande wa Zanzibar. Hii kwa Wazanzibari imekuwa ni jambo jema sana na inakwenda kuendelea kutatua zile kero mbalimbali zinazogusa Muungano wetu. Naiomba Serikali, maana maneno siyo vitendo, kwa hiyo, linapozungumzwa, tunaomba sana liende kwenye utekelezaji. Tuone kama bajeti inaanza kutumika Julai, basi utekelezaji huu na makusanyo kuanzia Julai yaanze kutekelezwa na yakaweze kutumika kwa upande wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuisaidia Serikali ili tuweze kupata mapato, najikita katika Sekta ya Uvuvi. Sekta hii inachangia pato la Taifa asilimia 1.8, lakini mapato yanayotokana na mauzo mbalimbali ya bidhaa za uvuvi ni 3%. Kwa masikitiko makubwa sana, hii sekta ni kubwa na pana, lakini pato ambalo limetajwa hapa la asilimia 1.8 ni dogo kulinganisha na rasilimali zinazotokana na bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahari yetu Mungu ametujaalia neema kubwa sana kwa kweli, ina rasilimali nyingi sana za kutosha. Kama Serikali itajiwekeza zaidi, basi tuna uwezo wa kupata pato kubwa ndani ya Taifa letu na tutapunguza hata hizi kodi mbalimbali ambazo zinawagusa wananchi wanyonge wakipunguziwa mzigo huu, mapato yataongezeka kupitia sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia bajeti ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano iliyokwisha, Wizara hii ya Uvuvi imekuwa ikipatiwa asilimia 21 tu ya bajeti katika utekelezaji wake. Hii inaonekana wazi kwamba Serikali bado haijaamua kujivekeza vizuri katika Wizara hii, ikiwa miradi ya maendeleo inapewa asilimia 21 kwa miaka mitano,

tusitegemee kama kuna mabadiliko wala kupata mapato katika Sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika rasilimali ambazo zipo ndani bahari, nakumbuka nilizungumza suala zima la uhifadhi wa matumbawe kama kivutio na nikatoa mfano wa baadhi ya wageni ambao huwa wanatembelea na tunapata mapato mengi kama Serikali. Nje na matumbawe, kuna kilimo cha mwani. Cha kushangaza ni kwamba Serikali yetu bado haijatupa jicho na wala haioni kama kuna umuhimu wa kuwekeza zaidi kwenye kilimo cha mwani. Ni kilimo ambacho kinalimwa kwa muda wa wiki sita tu na watu wanavuna. Kwanza kilimo chake ni cha muda mfupi lakini tumepewa bahari ambayo ndiyo sehemu sahihi tuna uwezo wa kupanda mwani wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile faida ambayo inapatikana katika kilimo cha mwani kwanza tutatengeneza ajira pana, maana watu watajajiri kwenda baharini na tutakuwa na viwanda nje. Tunazungumza kila siku tunahitaji kuwa na Tanzania ya viwanda, lakini tutakuwa na viwanda ambavyo mwisho wa siku hatutakuwa na rasilimali kwenye hivyo viwanda ambavyo tunavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nje tu na ajira, mwani ni chakula. Tuna uwezo wa kutengeneza vitu mbalimbali ambavyo binadamu tunavitumia, ni vyakula vya kila siku. Vile vile, mwani hutumika kama vipodozi. Akina mama wengi wa Kitanzania tunatumia *cosmetics* kutoka nje ya nchi wakati tuna rasilimali zetu nyingi. Ukianza na huu mwani, tuna uwezo wa kutengeneza sabuni na vitu vingi tukavitumia wenyewe. Kwa hiyo, kuna haja Serikali nayo kutupa jicho kwenye kilimo hiki cha mwani ili tuweze kuokoa Taifa letu na kupata mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kilimo hiki cha mwani tukizungumza kwa dunia, tuchukue mfano nchi ya Indonesia ndiyo imekuwa ya kwanza ikilima mwani na ndiyo nchi ambayo inafanya vizuri kwenye Sekta hii ya Mwani. Mheshimiwa Rais alisema kwamba tuwe tunajaribu kuwaiga

watu wanaofanya vizuri, siyo dhambi. Kwa hiyo, nasi nadhani ni wakati wetu sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Indonesia walio wengi wametajirika kuititia kilimo cha mwani. Vile vile wana viwanda vingi vya kutengeneza dawa, vipodozi, wanatumia mwani kama chakula na bado maisha yao yamenyanyuka vizuri sana. Kwa hiyo, naishauri tu Serikali kwanza tuwekeze kwenye mwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali imeona labda imekuwa mzigo mzito au tunaona ni jambo ambalo haliwezekani, wawekezaji wako tayari na wanahitaji hii bahari. Wanaiangalia kwa jicho la huruma sana na wanaitamani kama leo waipate na waweze kuwekeza ili tuweze kutengeneza ajira pana kwa Taifa hili na ili tuweze kutengeneza pato la Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika Sekta ya Utalii. Sekta hii nayo imekuwa ni chachu ya uongezaji wa pato letu, tunaizungumza kila siku lakini ukiangalia sekta hii, utalii ambao umejikita zaidi ni utalii wa wanyamaporii maana tumekuwa hatu-focus kwenye utalii mwingine, yaani tumeganda tu kwenye wanyamaporii, sisi kila siku kazi yetu ni kutangaza, tuna Ngorongoro na sehemu nyingine. Sasa tunahitaji pia kupanua wigo zaidi. Vile vile, kama sisi hatuwezi wawekezaji wapo, wa ndani na wa nje wako tayari, wanahitaji hii nchi kwa ajili ya kuwekeza. Wao watatengeneza pesa lakini na sisi tutatengeneza mapato, ndiyo kinachotafutwa ili tuweze kuiokoa nchi yetu kwenye masuala mazima ambayo yanaleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukipitia ripoti ya *CAG*, naye alishauri kwamba utalii wa Tanzania, kuna haja sasa ya kwenda kuingiza katika utalii mwingine na kuanza kuutangaza. Tusing'ang'anie tu kwa wanyamaporii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri tena Serikali iweze kutengeneza mikakati iliyokuwa bora ili tuweze kusimamia Sekta hii vizuri sana. Halikadhalika unapopitia hii hotuba,

Mheshimiwa Waziri alisema kwamba watapunguza ada ya leseni za biashara za utalii kutoka Dola 2,000 hadi Dola 500. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza tu ada kwenye leseni bado hatujasaidia kwenye hii Sekta, kwa sababu tuna changamoto nyingi ambazo zinaikabili Sekta hii. Ukiangalia miundombinu yetu ni mibovu sana. Sehemu ambazo zina vivutio hazififikasi. Kwa hiyo, naishauri Serikali waanze kwanza kuboresha sehemu zenye vivutio vyatya utalii, watengeneze barabara, viwanja vyatya ndege ili watalii wawe wana uwezo wa kufika vizuri na kuweza kuingiza pato ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe kuna mazingira Rafiki; tupunguze sintofahamu kwa wawekezaji wetu, maana Uhamiaji anamganda mwekezaji; sijui Halmashauri anamganda mwekezaji na wengine wengi. Imekuwa *harassment* kubwa sana. Kwa hiyo, tupunguze hizo *harassment* kwa wawekezaji wetu ili nao waweze kuwekeza kwa kijiachia na kuweza kulisaidia Taifa hili kwa kuwapa ndugu zetu ajira na kulisaidia Taifa hili kwa kuweza kutuingizia mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Muhamari Shabani Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ajiandae.

MHE. MUHARAMI S. MKENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nishukuru kwa kupata nafasi hii kwa jioni hii ya leo kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2021/2022. Kwanza napenda nitoe pongezi za dhati kabisa zinazotoka ndani ya moyo wangu kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, jemedari wetu, Amiri Jeshi Mkuu wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kwa kipindi kifupi ambacho nipo ndani ya Bunge hili, mama huyu kiongozi wetu ametuheshimisha sana Wabunge kwa kutoa

pesa, takribani kwa muda mfupi, shilingi bilioni moja na pointi kadhaa katika majimbo yetu. Tunampongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa uwasilishaji wa bajeti yake ambayo haijapata kutokea. Miaka yote kabla sijawa Mbunge nilikuwa nasikiliza bajeti, lakini hii bajeti ambayo niko ndani ya Bunge ni bajeti ya aina yake. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na ninaamini kuwepo katika timu fulani yenyе rangi nzuri nzuri kumesababisha na mambo yake yawe mazuri ndani ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe mchango wangu kwanza katika Sekta ya Uvuvi. Serikali mwaka huu katika mipango yake imeamua kujenga Bandari ya Mbegani ya Uvuvi. Naipongeza sana Serikali kwa jambo hili. Bandari hii ya Uvuvi itakapojengwa italeta manufaa makubwa siyo kwa Wanabagamoyo peke yake, ni kwa Watanzania wote kwa sababu Mbegani miaka mingi inafahamika ni Chuo kikubwa sana cha Uvuvi na wanafunzi wengi kwa miaka ya nyuma walikuwa wanasoma pale katika kile Chuo cha Mbegani. Sasa hivi, kile chuo kiko katika hali ngumu kidogo. Katika ujenzi huu wa bandari ya uvuvi ambayo inatakiwa kujengwa, itaifufua sekta ya uvuvi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa kununua meli nne za uvuvi. Hizi meli pamoja na hii bandari vikienda sambamba, basi katika sekta ya uvuvi, Serikali itakusanya mapato mengi ya kutosha. Wenzetu wako mbali katika suala la uvuvi. Kwa mfano, wenzetu Wakanya wana bandari yao pale inaitwa *Liwatoni Fishing Port*. Ile bandari imejengwa mpya kabisa; na mwaka huu mpaka Juni 2021, wamesema wanaingiza wanafunzi 1,000 pale kwa ajili ya kujifunza masuala ya uvuvi ili ile bandari iweze kufanya kazi kiaina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, naiomba Serikali katika bandari hii ambayo inatarajia kujenga pale

Mbegani, kwanza waanze kutoa mafunzo kwa vijana ambao watakwenda kufanya uvuvi katika hiyo bandari. Halafu bandari itakapokwisha, kazi moja kwa moja inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka kuzungumzia katika sekta ya utalii. Siku moja nilichangia hapa katika mchango wangu kuhusu utalii wa ndani. Utalii wa ndani una pesa nyingi sana, lakini niliwashauri kitu kimoja, sasa hivi ifikie wakati tuanzishe utalii wa kutembea (*mobile*), kwa sababu Watanzania wengi sana hawana uwezo wa kwenda katika mbuga za wanyama. Tutashawishiwa sisi Wabunge twende Ngorongoro, twende Manyara na Mikumi lakini mtu wangu pale wa Bagamoyo au sehemu nyingine yoyote hawezi kuwa na kipato leo hii cha kwenda kutembea katika mbuga za wanyama za Mikumi, Ngorongoro au Manyara. Hapo itakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa sababu mabanda ya maliasili pale Saba Saba yanatembelewa na watu wengi sana katika kuona wanyama, waende kila mkoa wakafungue hizi *zoo* ndogo ndogo za kutilii watu. Wajenge mabanda, waweke simba, waweke swala, kila mnyama pale, watu wakienda wanalipa viingilio kwenda kuona wanyama. Wanafunzi, watu mbalimbali wakienda huko pesa itapatikana, tena kwa wingi sana, kuliko tukitegemea utalii wa ndani tuwashawishi watu waende Ngorongoro, Manyara na wapi. Watanzania walio wengi uwezo huo hawana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la biashara. Biashara ndiyo inayoleta kodi na kodi ndiyo inatusaidia katika kuendesha nchi yetu. Hata hivyo, kuna changamoto sana katika biashara na hasa katika sheria hizi za *TRA*, za Utaifishaji. Sheria za Utaifishaji ni changamoto kubwa sana. Hizi sheria naona kwa upande mmoja au mwингine zinatakiwa sasa zifanyiwe mpango zirekebishwe. Kwa sababu leo hii kwa mfano mtu ana gari yake amenunua, amemkabidhi dereva Fuso au *lory*, amekwenda kubeba mzigo huko, bahati mbaya huo mzigo ni wa magendo. Inafika gari inakamatwa,

inapelekwa katika sehemu labda TRA wanaikamata, wanataifisha mzigo, wanataifisha gari, pengine mwenyewe mwenye gari hahusiki. Hii inatia hasara sana kwa watu na watu wengi wanalamika mno, kwamba kosa kafanya dereva lakini gari linataifishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu hii sheria tuiangalie vizuri kwa kweli, inaumiza sana watu. Pale jimboni kwangu Bagamoyo kuna kijana mmoja ana Fuso zake mbili; madereva walikwenda wakapakia vitenge vya magendo, magari yakakamatwa, yakataifishwa. Kijana wa watu wamemrudisha nyuma. Alikuwa na Fuso mbili ambazo amezitafuta karibu miaka 20, ameanza tena sifuri. Yaani amechanganyika karibu anakuwa chizi. Jamani haya mambo mengine ya sheria tuyaangalie Mheshimiwa Waziri ili wafanyabiashara wetu waweze kufanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hizi sheria za kutaifisha tunazozitunga humu ndani, wawekezaji wa nje wakizisikia hawatakuwa na imani ya nchi yetu. Wataona kwamba Tanzania ukienda kuwekeza, kama wenyewe kwa wenyewe wanataifishana, mimi imgeni nikiwekeza mali yangu itakuwa salama? Kwa hiyo, nafikiri kwamba tubadilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa nataka kulizungumzia ni la sensa, sensa ni kitu muhimu sana. Kuna kitu ambacho nataka nimshauri Waziri, nchi zilizoendelea nyinginezo sasa hivi sensa yao, pamoja na kwamba, wanapanga kila baada ya miaka fulani wanafanya sensa, lakini wanafanya sensa ya ndani kwa kutumia watu wao. Na sisi Tanzania tuanze kufanya sensa ili tuwe na *projection* ya kujua maendeleo yetu yanakuaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, leo hii tunangojea kila baada ya miaka 10 au mingapi tufanye sensa, tunao watendaji wa vijiji, tunao watendaji wa kata, tuwatume kazi wapite vijijini kuangalia idadi ya watu wanaozaliwa ili Serikali iwe na *projection* vinginevyo tutakuwa

na ule mpango wa zimamoto, hatujui idadi ya watu, watoto wanaoenda sekondari wanaongezeka, tunajenga madarasa ya zimamoto. Lazima tuwe na mipango thabiti katika hii sensa, tuwatumie viongozi wetu wa vitongoji watuletee taarifa wazipeleke katika kata taarifa za watoto waliozaliwa nchini, wa vitongoji wapeleke kwenye kata, watu wa kata nao wapeleke wilayani, watu wa wilayani wapeleke mkoani. Mkoani wapeleke Taifani tupate mtiririko wa idadi ya watu wanaozaliwa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, tukitegemea taarifa za hospitali tupu, wengine wanajifungulia majumbani hatupati taarifa zao kwa hiyo, inakuwa kidogo kuna ugumu fulani. Niiombe Serikali hili suala la sensa wasingojee mpaka kipindi, walianze mapema kuangalia *projection* ya nchi inakwendaje katika uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo la kilimo, nataka kuzungumzia, kilimo cha umwagiliaji. Hiki kilimo cha umwagiliaji tukikifuatilia na tukikitilia mkazo Taifa litatoka kabisa katika maisha tuliyonayo sasa hivi kwa sababu, umwagiliaji ndio wenye tija. Tukitegemea mvua hizi za kunyesha tu za msimu wakulima wetu wengi sana huwa hawazalishi pale ambapo idadi yao au idadi ya mazao wanayohitaji kufikia lengo, lakini kilimo cha umwagiliaji kitatusababishia tufike katika *level* nzuri kabisa ya uzalishaji katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii. Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2021/2022 ambayo iliwasilishwa hap ana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kutujalia uzima na kuweza kukutana hapa. Lakini pili nichukue nafasi hii kwa dhati ya moyo wangu kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Jemadari wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuiongoza nchi vizuri kwa muda huu ambao tukonae na kwa namna ambavyo amekuwa akisikiliza maoni ya Wabunge. Miiongoni mwa sifa inayompamba kiongozi yejote ni kusikiliza watu wake; Mama yetu anatusikiliza na anawasikiliza wananchi na anatuongoza vizuri, tunampongeza sana na tunamtakia afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi ni huu ambao tumeuona tumeongea sana hapa wakati tunachangia bajeti za kisekta. Tulizungumza sana habari ya barabara zetu ziliziko vijijini na tukaeleza kiu yetu ya namna ambavyo tunatakiwa kutenga fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya kujenga barabara za vijijini. Kama haitoshi ameweza kutoa milioni 500 kwa kila jimbo na hivi tunavyoongea ma-*manager* wetu wa TARURA wanaendelea kufanya kazi ya kufanya maandalizi ya kujenga barabara hizi. Maana yake barabara za vijijini zikiwa salama maana yake huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo kusafirisha mazao zitaenda kufanikiwa katika vijiji yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada yamaneno hayo niseme nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Mchomba, kwa kuwasilisha vizuri bajeti hii ambayo tunaijadili. Kwa hakika bajeti hii imejikita katika kutatua kero za wananchi, bajeti hii imeonesha muelekeo wa Serikali kwa mwaka mmoja ujao; kwa kweli, nimpongeze yeeye pamoja na watendaji wake akiwemo Naibu Waziri pamoja na katibu mkuu kwa kazi nzuri ya kutuandalia bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nimeona maeneo mengi yamefanyiwa kazi, lakini ni vizuri nitoe ushauri wangu ili tuweze kubeba kwa pamoja bajeti hii ambayo inaenda kuboresha maisha ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwenye eneo la kilimo, wote wamezungumza hapa tumepongeza juhudini mbalimbali, lakini tumeangalia katika hili kwamba, bajeti ya Serikali inaeleza wazi kwamba, kilimo kinachangia fedha katika Serikali asilimia zaidi ya 26, lakini tunatenga fedha kidogo sana za maendeleo za kuhakikisha kwamba, tunapanga vizuri mipango ya kilimo cha nchi yetu, lakini wote tunajua kwamba, asilimia zaidi ya 65 ya wananchi wetu ndio wanafanya kilimo vijiji. Maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, shughuli kubwa inayofanywa na wananchi wetu wa Tanzania ni kilimo, lakini kilimo hiki kikitumika vizuri tukapata mazao ya kutosha tutaweza kupeleka malighafi nyingi kwenye viwanda. Maana yake tutakuwa na uwezo mkubwa wa kukuza viwanda na ambayo itatusaidia sana kuongeza pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu nilikuwa nataka niseme tu kwamba, pamoja na kuwa nchi yetu imeingia kwenye kipato cha katika kama tusipoangalia vizuri tatarudi tena nyuma, ombi langu ni kwamba, tuongeze nguvu sana kwenye kilimo cha nchi yetu. Wananchi wetu wasaidiwe walime kilimo cha kisasa. Ninajua juhudini zipo kubwa na kwenye hili nitaongelea zao la alizeti kwa asilimia kubwa kwa sababu, zao hili linalimwa sana katika mikoa 19 ya nchi yetu, pamoja na Mkoa wa Singida tunalima sana alizeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa. Tarehe 13 mwezi wa sita alitisha kikao cha wadau wa alizeti katika Mkoa wa Singida na alionesa wazi kwamba, Serikali imedhamiria kuwekeza sana, ili kuondokana na kuagiza mafuta nje ya nchi. Tunatumia fedha zaidi ya bilioni 400 kuagiza mafuta kila mwaka ili kufidia *gape lililopo* la mafuta katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nieleze kwamba, tumepata mwanga mzuri juzi tulivyokaa na wadau. Na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametumia muda wa saa nane

amekaa kwenye kitu anasikiliza maoni ya wadau, ikiwemo sisi Wabunge. Niombe sana eneo ambalo limeelezwa sana ni sehemu ya kupata pembejeo ikiwemo mbegu bora zenye kutoa tija. Niombe sana kuititia bajeti hii tuongeze fedha za mbegu bora, ili wananchi wetu waweze kulima alizeti itakayoleta mafuta mengi, uzalishaji mwingu na kusaidia viwanda vyetu viweze kuzalisha mafuta mwaka mzima. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea kwa sababu uzalishaji ni mdogo tumegundua kwamba, wanafanya miezi mitatu tu ya mwanzo, miezi iliyobakia yote hakuna uzalishaji wa mafuta kwa sababu, hakuna mbegu za mafuta za kukamua. Kwa hiyo, niombe sana kwenye eneo hili tumesema kwamba, tutahakikisha kwamba, miundombinu ya umwagiliaji tutaiongeza. Kwenye eneo hili ninaomba sana Serikali longeze nguvu kwani kilimo hiki kikiwepo kitasaidia sana uzalishaji wa kutosha bila kutegemea mvua. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwenye hili niseme kwenye eneo moja tumekuwa tukitengewa fedha, lakini hazitoki kwenye skimu ya umwagiliaji katika kata yangu moja inaitwa Mang'onyi. Skimu ya umwagiliaji hii ikikamilika itasaidia wakulima wengi kupata kilimo cha umwagiliaji na kuongeza tija katika kilimo chao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi tumeongelea habari ya upimaji wa udongo. Kuna maeneo mengi wakulima wanalima tu ilimradi wanalima, lakini hawajui ardhi yao ina uwezo gani wa kuzalisha mazao. Tumeomba sana watafiti wetu wafanye kazi hiyo kuhakikisha kwamba, ardhi ambayo tunalima inakuwa ni ardhi inayojulikana wazi; kama inahitaji mbolea ijulikane ni mbolea kiasi gani, ili wakulima wetu waweze kulima kwa uhakika. Na kwenye hili Waziri Mkuu ameelekeza kwamba, wenzetu wataalamu wa kilimo waweze kufanya kazi yao vizuri, washauri kwenye hal mashauri zetu ili tuweze kuhakikisha tunalima kilimo cha uhakika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kilimo hiki ni pamoja na kuhakikisha kwamba, tunaongeza kilimo cha chakula kwa maana ya mazao mbalimbali yanayotokea huku, ili tuwe na usalama wa chakula. Niseme tu, nieleze tu kwamba, pamoja na kwamba, tunaongelea kilimo, lakini nishukuru sana Mheshimiwa Rais ameonesha wazi kwamba, bajeti hii ni kweli ni bajeti ya kazi iendelee. Kwa sababu, miradi yote ya kimkakati amesema itaendelea na juzi akiwa Mwanza amezindua tena ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Mwanza kwenda Isaka maana yake sasa inakutana katikati iweze kukamilika ianze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeeleza waziwazi usafiri wa anga pamoja na ununuzi wa meli ambao amesaini juzi meli tano zinaenda kujengwa pamoja na uboreshaji wa bandari. Hili ni jambo jema kabisa, tuendelee kuiomba Wizara, tuendelee kutoa fedha ambazo zimetengwa ili miradi hii isikwame njiani ili tuweze kupata matokeo ambayo tunayatarajia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo hili nitaongelea kidogo kwenye eneo la wilaya yangu. Wilaya ya Ikungi tulikuwa na maombi ya muda mrefu, tunaomba tuwe na mradi wa kimkakati na sisi tuwe na stendi ya wilaya; hatuna stendi ya mabasi ambayo inaweza kukidhi haja iliyoko pale katika wilaya yetu. Lakini kwenye eneo hili pia nilikuwa naombaa tupate soko la kisasa katika eneo lile katika wilaya yetu, ili kuongeza mapato ya halmashauri ili yasaidiane na bajeti ya Serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi wetu katika vijiji vyetu pamoja na wilaya zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongelee jambo la tatu ni jambo la maslahi ya watumishi. Hili eneo niipongeze sana Serikali kwa kuamua sasa kwamba, wafanyakazi wapatoa 94,000 wanaenda kupandishwa madaraja na fedha zipo katika bajeti hii. ni jambo jema sana pamoja na kuwa tunasema waongezewa mshahara, lakini ukipandishwa daraja una uhakika na kulipwa mshahara katika daraja lako. Wengine wanajiendeleza katika elimu, lakini wanakuwa wanabaki hawapandishwi madaraja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara husika ihakikishe inasimamia vizuri wafanyakazi hawa wapate haki yao ya kuhakikisha wanapanda madaraja. Nimeona zimetengwa karibia bilioni 400 zinaenda kufanya kazi hii ni jambo jema sana tunamshukuru sana Rais, tunamshukuru sana Waziri kwa kuwasilisha jambo hili; lakini niendelee kuomba tuendelee kuendelea kuwaza kuongeza mapato, ili tuweze kuongeza mishahara ya watumishi ambayo kwa kweli, wameendelea kuomba kila mara na dhamira ya Mheshimiwa Rais tunaiona atawaongeza kama alivyosema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo hili tumeongelea pale Madiwani, Madiwani wanafanya kazi nzuri sana kule. Nipongeze kwamba, fedha zile ambazo walikuwa wanalipwa posho yao itaenda moja kwa moja kutoka kwenye Serikali kuu ni jambo Jema. Lakini niombe sana Mheshimiwa hii ilikuwa ni hiyo fedha wanalipwa huko nyuma kwa hiyo, wamekuwa na maombi ya kuda mrefu tunaomba posho ziongezwe za Madiwani ili wafanye kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika maeneo yetu. Sisi tukiwa huku wao wanafanya kazi vijiji kule kukaa karibu na wananchi katika kusimamia maendeleo, tukiwaongezea wataongeza motisha, wataongeza nguvu kubwa ya kusimamia maendeleo na fedha hizi tunazozipeleka kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tumeongelea habari ya suala la Madiwani, lakini kuna namna ambavyo tunadhani kule kwenye vijiji tuone namna ambavyo tutaongeza fedha kwa ajili ya kuwasaidia viongozi wetu wa vijiji ili waweze kufanya kazi kwa tija.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ninaunga mkono asilimia 100 bajeti hii. Nawatakia kila la heri, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence Saizi atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Mheshimiwa Omar Ali Omar ajiandae.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya kimkakati iliyowasilishwa mbele yetu. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi nzuri na bajeti nzuri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, nimpongeze Naibu wake Mheshimiwa Eng. Masauni, Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Emmanuel Tutuba na watumishi wote wa Wizara kwa kutuwasilishia bajeti nzuri ambayo kwa kweli ni bajeti ya kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ametuletea bajeti ambayo inaonesha matumaini makubwa maana aimejielekeza katika huduma za jamii ambazo zinagusa maisha ya wananchi moja kwa moja. Ni bajeti nzuri ambayo kwa kweli, imeleta matumaini, wana-Muhambwe wameleta shukrani nydingi sana na mimi naziwakilisha kwa heshima na unyenyekevu mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna maeneo ambayo naona yanaweza yakafanyiwa kazi zaidi ili tuweze kuongeza kipato maana ni ukweli usiopingika tunahitaji kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Nitachangia upande wa maliasili na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langa la Muhamwe linayo hofadhi ya Moyowosi, hifadhi hii ni hifadhi kubwa sana ambayo ina wanyama wote wakubwa watano, lakini pia ina wanyama ambao wanapotea kama vile statunga, lakini pia kuna ndege ambao ni adimu kama vile shubiri. Hifadhi hii inafanya utalii wa uwindaji tu, tunavyo vitalu sita, tumekodisha vitalu vinne, lakini viwili bado havijakodishwa. Hifadhi hii ina ardhi oevu, lakini pia ni ardhi yenye majimaji inachangia pato la Taifa sana kama tunavyo jua maliasili

inachangia takribani asilimia 17 ya pato la Taifa, lakini inachangia asilimia 25 ya pesa za kigeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi hii haijatumika inavyotakiwa kwa sababu ya miundombinu. Kama nilivyo sema hifadhi hii ina maji, barabara hazipitiki kabisa, hakuna vyombo vya usafiri katika hifadhi hii, hii inachangia kwamba, vile vitalu vingine visiweze kupata, lakini watu wasipende kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali zile hifadhi zinazofanya vizuri ina maana kuna nguvu iliwekwa ndio zikafanya vizuri, ili ukamue maziwa vizuri kwa ng'ombe lazima huyu ng'ombe umtunze. Naomba Serikali iangalie vizuri Hifadhi ya Moyowosi, bado ina vivutio vikubwa ituwezeshe kutuletea magari, ilituahidi kutuletea trekta na boti, ituletee illi na sisi pato likipanda katika halmashauri *automatically* wananchi mmoja-mmoja watafaidika maana watapata ajira mahali pale, pato litaongezeka, lakini na nchi itafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu hifadhi il eina mito mingi ambayo ina samaki bado inaweza ikatumika kwa kufanya uvuvi wa hapohapo, *spot fishing*, lakini pia tunaweza tukaweka utalii wa picha. Hii yote ni kujitahidi kuitumia hii hifadhi kwa kiasi kikubwa, ili tuweze kujiongezea pato. Tuilee hii hifadhi, mtusaidie tupate vyombo hivi vya usafiri, tuitangaze maana vitalu viwili kukaa bila wawekezaji hii ni hasara kwa halmashauri yetu ya Kibondo, lakini pia kwa nchi nzima; tunaomba tuitangaze Wizara itenye bajeti kabisa rasmi kwa ajili ya kutangaza hivi vivutio ili tuweze kuongeza kipato. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishukuru Serikali kwa sababu, inaendelea kuonesha jinsi gani inawekeza katika kupanua biashara za ujirani mwema. Jimbo langu la Muhambarwe limebahatika tuna ujirani mwema na Burundi. Tunaishukuru Serikali ilitujengea soko katika Kata ya Mkarazi hii ni kati ya Mabamba na Gisulu, Burundi, lakini bado hili soko halijatumika ipasavyo ndio yani kama kila siku kama linaanza, kwa nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna vitu muhimu. Hatuna *TRA* pale, hakuna polisi, hakuna mambo ya ndani, ina maana Warundi pia wanaona hofu kuja kufanya pale biashara. Soko hili likiwezeshwa tukaweka *One Stop Centre* pale ina maana biashara pale zitafanyika tutajongezea pato la Taifa, wananchi watafanya biashara zao pale, mazao yetu yataenda pale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kabisa Jimbo langu la Muhamwbe tunalima sana mihogo na wanunuzi wakubwa ni Warundi. Kwa hiyo, tukiweka soko zuri pale tukaliboresha hili soko la Mkarazi ambalo Serikali imeshaweka pesa, lakini haikuwekwa kwa utimilifu kwa sababu, haikukamilisha kuweka mambo muhimu ili biashara iweze kufanyika. Basi tunaamini ikifanya vizuri katika lile soko basi tutakuwa na biashara nzuri ya ujirani mwema na hivyo, kipato kitaongezeka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuboresha barabara maana mazao ili yaweze kufika pale Mkarazi lazima barabara ziwe nzuri. Barabara zile hazipitiki kabisa wakati wa mvua kwa hiyo, mazao yanaharibika shambani. Tuinaiomba Serikali itusaidie kwa sababu, halmashauri ikiongeza mapato basi pato la Taifa moja kwa moja litaongezeka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kuishukuru Serikali kwa jinsi inavyoona kuboresha miundombinu ya shule kwa ajili ya vijana hasa kwa kuongeza bajati kwenye vyuo vya ufundi stadi. Zipo *VETA* nchini, lakini kuna sehemu nyingine hatuna *VETA* ila tumebahatika kuwa na vyuo vya wananchi ambavyo vilianza miaka mingi sana, kama Jimbo langu la Muhamwbe chuo kimeanza mwaka 1975 kwa hiyo, kwa picha ya kawaida unaweza ukaona hiki chuo kiko katika hali gani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali ilituletea pesa milioni 500, tulifanya ukarabati kwa kiasi. Ili tuwasaidie vijana wa Jimbo la Muhamwbe tunaomba chuo hiki kiangaliwe vizuri kwanza wakati tukijipanga kwenda kwenye *VETA*. Tuongezewe pesa ili tukiboreshe zaidi, tuongeze

mabweni, tuongeze madarasa, tuongeze vifaa, ili vijana nao wa Muhamwe waweze kupata ujuzi mdogomdogo ili waweze kujajiri kwa ajili ya kufanya biashara, ili tuweze kuongeza kipato kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa tozo hizi ilizoleta tozo ya *line* za simu, tozo za miamala, tozo mbalimbali ambazo hizi zitatusaidia kupata kipato, tutaendelea kupata kipato kwa watu wengi kidogo kidogo kipato ambacho ni kodi ambayo si ya moja kwa moja kwa hiyo hii haimuumizi sana mwananchi, ombi langu kwa Serikali fedha hizi zikipatikana basi siende kule tulipozielekeza, hasa kwenye *TARURA* maana sisi wa vijiji hasa tunalilia kwanza barabara zipitike, barabara hazipitiki kabisa, vijiji haviunganishwi kama vijiji haviunganishwi Pato la Taifa litaongezeka vipi wakati watu hawawezi kuingiliana barabara ya kwenda kijiji kingine hakuna! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kusikitisha bajeti ya sisi tunaotoka tunaitwa pembezoni kama Jimbo langu la Muhamwe bajeti ya *TARURA* inapinguia kila mwaka tulianza na *one billion* 2017/2018, lakini 2021/2022 Milioni 800, nilidhani kwa kuwa ni pembezoni basi tutaongezewa ili na sisi tuwasiliane japo vijiji, lakini inaendelea kupungua kwa hiyo naishauri Serikali sisi wa pembezoni pia tuna uwezo wa kuchangia pato la Taifa kama mta- *invest* kwenye Wilaya zetu ili tuweze kufanya vizuri, tusitolee macho tu kule kulikofanya vizuri tuanzishe na huku ambako kunaweza kukafanya vizuri zaidi, japo ni pembezoni lakini bado kuna fursa nyingi ambazo hatujazitumia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali kwa miradi ya maji ambayo tumeona kabisa fedha hizi tutakwenda kuzipata na zitaisaidia miradi ya maji. Ushauri wangu kwa Serikali miradi ya maji jamani ni mingi hata jimboni kwangu ipo lakini Jimbo la Muhamwe ni Jimbo ambalo Kibondo Mjini nikikuonyesha maji yake ni aibu ni tope, japo ukiuliza unaambiwa kuna mradi wa kwanza wa pili na wa tatu, miradi ya maji ambayo haizai matunda sielewi utafiti haufanyiki tunapoanzisha mradi, sielewi usimamizi haufai sijui

vizuri naona wataalam wa maji watusaidie kwa nini tuna miradi lakini hii miradi tunaisoma kwenye makaratsi haitoi maji? kama Kata yangu ya Kibondo Mjini ni tatizo maji hakuna na yanayotoka ni tope. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi tunaishauri Serikali fedha hizi ambazo tutawakata walipa kodi kwenye *lane zao* za simu kwenye miamala zitumike inavyostahili miradi waione hii itawafanya wananchi waendelee kuwa na moyo na ari ya kutoa na hizi kodi hazitawaumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali pia kwa posho ya Madiwani, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye Mbunge wa Muhamwe, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajandale. (*Makof*)

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali chini ya uongozi wake Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuisimamia vizuri Serikali yetu kiasi kwamba imekuwa ikiendelea kutekeleza miradi ya kimkakati na miradi mikubwa kwa ufanisi mkubwa pia napenda kuwapongeza wasaidizi wake Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Baraza zima la Mawaziri, kwa namna ambavyo wanachapa kazi usiku na mchana kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imeonesha ukomavu, usikivu, unyenyekevu na hekima kubwa na busara kubwa kwa wananchi wake katika kuiendesha nchi yetu, naipongeza sana Serikali yetu. Suala la kutengwa kwa Milioni

500 kila Jimbo suala la kuwekwa tozo ya shilingi 100 kwenye mafuta ni mambo ambayo wananchi wengi yamewafariji sana na ni imani yangu kwamba sasa barabara nyingi zitawenza kuitika muda wote wa mwaka bila kuwa na kikwazo chochote, lakini vilevile kutenga Milioni 600 kwa ajili ya shule za Sekondari ni imani yangu kwamba sasa tunakwenda kutatua changamoto kubwa iliyokuwa inalikabili Taifa letu, changamoto ya mimba za utotonu, pamoja na utoro kwenye shule zetu kwa sababu hapo kabla watoto walikuwa wanasoma shule za mbali sana kwa sababu kwenye Kata zao kulikuwa hakuna shule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwangu Somanga kulikuwa hakuna shule kwa hiyo nina imani kwa kuititia hizi Milioni 600 basi tutapata suluhisho la matatizo na changamoto ambazo zilikuwepo, walikuwa wanasoma umbali wa Kilometra 15 kwenda kwenye Kata za Jirani. Nieleze tu taarifa ya masikitiko kwenye Jimbo langu la Kilwa Kaskazini siku ya tarehe moja ya mwezi huu wa Juni, kulitokea msiba wa mwananchi wangu anaitwa Walivyo Uwiro, katika Kijiji cha Kipindimbi, mkazi wa Kijiji ya Kipindimbi kata ya Njinjo, alifariki dunia kutohana na migogoro ya wakulima na wafugaji, ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na tukio hilo na matukio yanayoendelea ambayo kwa kweli hali ya usalama sio nzuri sana kule, kule katika kata za Miguruwe, za Kandawale, pamoja na kata hiyo ya Njinjo niliyoisema na Mitowe ningeomba tu Serikali sasa wakati tunaelekeea kutekeleza bajeti ya mwaka 2021/2022 iweze kurekebisha mambo fulani na kutuboreshea mambo fulani ili kuhakikisha kwamba matukio ya namna hii hayajitokezi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu tumekuwa na tunu zetu za Taifa ambazo ni amani, utulivu, na mshikamano katika Taifa letu ambazo ni msingi imara kwa maendeleo ya Taifa letu ambazo kwa sasa zinaonekana kule Jimboni kwangu katika baadhi ya kata zimeanza kupungua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kwa kushirikisha zile sekta ambazo zinahusika kwenye kilimo, ufügaji, pamoja na ardhi watusaidie kuharakisha kuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili kuhakikisha kwamba hii migogoro haiendelei tena. Lakini vile vile ningeomba Wizara ya Mifugo ijkite kwenye kuboresha mazingira bora ikiwemo ujenzi wa malambo, ili kuwafanya wale wafugaji ambao wamehamia katika maeneo yetu wasiwe wanahangaika hangaika sana na kuingia kwenye mashamba ya wananchi na hatimaye kuzua migogoro ya namna hii. Lakini vile vile Serikali kwa kushirikiana na vyombo vyake vyaa dola basi ijitahidi kufanya *operations* za mara kwa mara ili kuzuia wahamiaji ambao siyo rasmi ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo wanaosumbua na kuleta hii migogoro ambayo ipo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninaomba nijikite kwenye sekta ya uvuvi kuna mambo matatu hapa nitayazungumza, kwanza ninaomba Serikali kupitia Wizara ya uvuvi itusaidie kujenga masoko ya kisasa katika maeneo yetu, Pwani yetu ya Bahari ya Hindi ikiwemo Jimboni kwangu Kilwa Kaskazini ni maarufu sana kwenye uvuvi ukifika pale Somanga Samaki wanavuliwa sana, wengine wanasafirishwa hadi nje ya nchi wanapelekwa hadi Spain, Portugal pamoja na Italy na China Samaki aina ya robusta pamoja na *prawns* pweza wamekuwa maarufu sana kule Kilwa hasa pale Somanga na Kivinje, lakini hali ya masoko kwa kweli ni mbaya lakini wataalam pia wamekuwa wachache kwenye sekta hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mtaalam ambaye anatoa leseni ambaye yupo chini ya Wizara ya Uvumi ni mmoja tu kwa Pwani yote ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, kwa hiyo mtu akitaka kusafirisha bidhaa zake kama hao Samaki ambao wanauzwa hadi nje nchi wanahangaika sana wale wafanyabiashara. Vilevile ningeomba wavuvi waboreshewe miundombinu ya kuvulia Samaki, vifaa vyaa kisasa vipatikane lakini vilevile maelekezo kutoka kwa wataalam, wataalam wetu wawe karibu na wavuvi wetu ili

kuboresha kipato chao na kipato cha Taifa kwa ujumla.
(*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la utalii wa uvuvi pia kama alivyotangulia kuzungumza Mbunge mwenzangu aliyetangulia bahari ya Hindi ina visiwa vingi, Kilwa peke yake kuna Songosongo, kuna Simaya kuna Ukuza lakini vile vile kuna kisiwa cha Simaya, kwa hiyo niombe iweke mkazo Wizara yetu ya Utalii ikishirikiana na Wizara ya Uvuvi kwenye eneo hilo, hii tunaiita *sports fishing* iweze kufanyika nchi kama *Seychelles , Maldives na Mauritius na nchi ya Mexico na Latin America* zimekuwa zimepiga hatua kubwa sana zimekuwa zikiingiza fedha nyngi kila mwaka kupitia hii *sport fishing* au uvuvi wa utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niombe kuzungumzia mchezo wa mpira wa miguu, nimefarijika sana kusikia kwenye bajeti yetu kwamba kutakuwa na msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye kuingiza nyasi za bandia ambazo zitatumika kwenye viwanja vyetu, nimefarijika sana kusikia kwamba *TFF* itapewa jukumu la kusimamia, kwa sababu *TFF* ndiyo yenye jukumu la kusimamia mchezo wa mpira wa miguu katika nchi yetu na wanajua *standards* za vile viwanja zinavyotakiwa kuwa, aina ya nyasi bandia zinazotakiwa wanazijua kwa hiyo nafikiri ni jambo ambalo limekaa vizuri, isipokuwa ningeomba kushauri katika eneo moja kwa Serikali yetu niiombe isitoe ile *privilege* au ile *exemption* kwa Majiji peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu dhamira ni njema ya kukuza vipaji na kuendeleza vipaji vya vijana wetu, vipaji vimetapaka nchi nzima kwa hiyo niombe kwenye Majiji, kwenye Manispaa kwenye Halmashauri za Wilaya kote misamaha itolewe ili wenyewe uwezo wa kununua hizo nyasi waweze kupata huo msamaha wa kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kuizungumzia *TFF*, *TFN* taasisi ambayo siyo ya kibashara lakini katika manunuzi yake yote hata mapato ya mlangoni yalikuwa yakitozwa *VAT* asilimia 18, lakini kwenye mapato ya

mlangoni unakuta wanakata kwenye ile *gross figure, gross revenue* yale mapato ghafi kabla ule mgao wa vilabu na maeneo mengine haujatolewa unakuta wanakata ile asilimia 18, hii imeleta uchungu na inasumbua sana kwa vilabu vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilabu vyetu vingi ni vichanga vinacheza mpira wa ridhaa sio *profession football* kwa hiyo mwisho wa siku ukikata asilimia 18 ya VAT maana yake unakuwa unavididimiza na kuvifanya vilabu visiwe na mapato ya kutosha, kwa hiyo ningeomba hii ikiwezekana ifutwe na kwa kuzingatia kwamba kama nilivyosema mpira wetu hauendeshwi kibashara, *TFF* siyo taasisi ya kibashara ningeomba ifutiwe hii kodi ya VAT. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sasa hivi kuna mradi unaogharimu kama Bilioni 10 wa uendelezaji wa virtuo vya michezo kule Kigamboni - Dar es Salaam na Tanga tayari pale inaonekana 1.8 Bilioni ambazo zile fedha zimeletwa na *FIFA* tayari 1.8 Bilioni zitakwenda kwenye VAT kwa hiyo zitapinguza ufanisi kwenye ile miradi ambayo inakwenda kujenga vipaji na kukuza mpira wa nchi hii, ndiyo maana ninasisitiza Mheshimiwa Waziri wa Fedha tusaidie kwanza kuiondoa kwenye *legislation* ya VAT *TFF* ili hatimaye iweze kufanya mambo yenye tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Ali Omar atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

MHE. OMAR ALI OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii jioni hii kuweza kuchangia bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana wataala* aliyetuwezesha jioni hii

kutupa pumzi zake na nguvu zake tukaweza kubakia katika Bunge hili Tukufu, siyo kwa uwezo wetu siyo kwa ujanja wetu wala siyo rai isipokuwa ni uwezo wake ye ye mwenyewe. Katika mchango wangu kwanza nataka nitoe kauli ya ndugu yetu mtunzi maarufu wa Kiswahili Shaaban Robert aliposema kwamba jibu linaposadifu swal shaka huondoka, hii ina maana ya kwamba nampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujibu maswali ya Watanzania moja kwa moja kwa matendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa kweli hatuna budi tumpongeze sana na wala asichoke na asonge mbele kwani asie macho haambiwi tazama, katika mchango wangu pia nataka niweze kuangalia kwa ruhusa yako unipe nafasi ndogo niweze kutoa nukuu ya falsafa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa hili la Tanzania. Marehemu mwalimu alisema siku moja katika nukuu yake "Njia pekee ambayo uongozi unaweza kutunzwa kama uongozi wa watu ni pale ambapo viongozi wanapokuwa na sababu ya kuogopa hukumu kwa watu".

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana ya kwamba furaha ilitanda katika ukumbi huu wakati Waziri wetu Mama Ummy Waziri wa TAMISEMI alipozitaja Milioni 500 kwenda moja kwa moja kutatua tatizo la barabara zetu za vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli furaha ilitujaajaa katika nyonyo zetu na bado furaha ile tunaendelea kuwa nayo, lakini tulikuwa tunajiuliza sana sana maswali na ndiyo hapa majibu yalipokuja kwenye falsafa ya Mwalimu Nyerere kwamba Hukumu ya watu tunaiogopa, kwamba tunatakiwa tutende mema kwa watu ili kwamba hukumu hiyo isitujie kwetu sote, kutokana na hali hiyo basi tukawa tunajiuliza hizi milioni 500 kwa vile zinatoka Mfuko wa Hazina, na Mfuko wa Hazina ni wa Tanzania tukaona sasa furaha na sisi imeanza kutuingia, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana pamoja na Naibu Waziri kwamba hili litaweza kutatua tatizo la Wazanzibar kwa kiwango kikubwa kwenye barabara zetu ambazo na sisi zinakero kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Tumbatu barabara ni mbaya hazipitiki za vijijini, ukienda Mwera kwa Mheshimiwa Mwinyi nako ni vilevile ukija kwenye Jimbo langu mimi la Wete pia hukumu ni hiyo hiyo, ukienda kwenye Jimbo la Mfenesini nalo linalia, ukienda kwenye Majimbo mengine yote ya Zanzibar yanalia kilio hiki cha barabara ambazo hazipitiki. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakushukuru tena naendelea kukushukuru kwamba mfuko huu wa Hazina nao utakwenda kutibu lile donda tulilonalo kule Zanzibar, kwa heshima kubwa kabisa napenda kukushukuru sana pamoja na Naibu Waziri wako na Waziri wa TAMISEMI kwa kulitoa tangazo kwamba Majimbo yote kwa hiyo mimi ninaichukulia yote ni yote Tanzania ni moja itajibu maswali na swali hili litajibowi na Watanzania wote, hasa ukilinganisha mfuko ni wa Hazina na Hazina ni ya Watanzani wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mnamuona Mheshimiwa George Boniface Simbachawene amekaa kwenye kile kitikinaashirika kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Dodoma, kwa hivyo Mheshimiwa George Boniface Simbachawene atakaimu nafasi ya Mkuu wa shughuli za Serikali Bungeni mpaka Waziri Mkuu atakaporejea Dodoma. (*Makofi*)

Lakini pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula huyu ni mdau wa Korosho kutoka Kigoma anaitwa Fredrick Amos Kidudu, karibu sana. Waheshimiwa Wabunge Korosho zinalimwa hadi Kigoma, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo ajiandae. (*Makofi*)

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi ya kuwa mliongoni mwa wachangiaji wa siku ya leo. Awali ya yote niipongeze sana Serikali kwa kuleta bajeti ambayo ina matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais

kwa jitihada anazozifanya za kujengwa nchi yetu kwa vitendo, tumeshuhudia miradi mingi mikubwa ambayo anaizindua ikiwa ni muendelezo wa yale ambayo aliahidi kuwatumikia Watanzania hasa pale alipoahidi kwamba ataendeleza kazi zilizoachwa na mtangulizi wake, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ambayo imekuja ni bajeti ambayo inaweza ikatusaidia sana Watanzania. Hata hivyo tuna ushauri kwenye bajeti, yapo mambo ya msingi ambayo Serikali kupitia Wizara ya Fedha ni vyema ikayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia suala la kilimo. Watanzania wengi wanajihuisha sana na shughuli za kilimo ambazo ndizo zinawapatia kipato. Watanzania wengi wanajihuisha na shughuli za uvuvi na ufugaji. Sasa ukitaka kuutengeneza uchumi wa nchi lazima kwenye maeneo hayo ambayo yamewashika wananchi walio wengi mtenge fedha na muwezeshe kwa kiwango kikubwa. Na unapotenga fedha kwenye sehemu ya kilimo umewasaidia Watanzania wote. Kilimo kina mahitaji mengi kwanza kinahitaji uwezeshaji wa zana za kilimo, lakini pili kinahitaji mbegu za kisasa ambazo mkizisambaza wananchi watazalisha kwa tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado, lingine ambalo Serikali halifanyi kwenye sekta ya kilimo ni kutokutafuta masoko. Mazao yanapozalishwa wananchi wengi wanakosa masoko; na wanapokosa soko tunawajengea uwezo duni wakulima. Niiombe sana Serikali, katika mwaka huu wa fedha Wizara ijitahidi sana kuhakikisha mazao yale ya biashara na mazao ya chakula mmatenga fedha kwa ajili ya kutafuta masoko ambayo yatawasaidia wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kwenye kilimo hasa cha zao la mahindi jirani zetu wa Kenya ndio wanaozalisha mbegu wanatuletea sisi. Ni kitu cha ajabu, kwamba jirani anakuzalishia mbegu, unanunua na baadaye unaenda kumuuzia malighafi kutoka kwako. Ni vyema sasa Serikali itenye fedha kwa ajili ya kukuza vituo vya utafiti, na

wale wanaozalisha mbegu tuwapate kwa wingi kwenye maeneo haya ili yaweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linguine ambalo hatujalifanya kazi zaidi ni kwenye sekta ya uvuvi. Mwenyezi Mungu alitujalia tukawa na Bahari ya Hindi yenye eneo kubwa sana la uvuvi. Tunaipongeza Serikali kwamba ina dhamira sasa ya kununua meli za uvuvi kwa ajili ya bahari ya hindi. Sasa tunaomba na kwenye Maeneo ya Maziwa Makuu Ziwa, Tanganyika pamoja na Ziwa Victoria tupeleke meli ambazo zitaanza shughuli za uvuvi sambamba na kutafuta mazao ya uvuvi ambayo masoko yake yatakuwa na uhakika. Hili litasaidia sana kuongeza tija kwa wananchi na wavuvi wa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuja na hoja ya kuongeza tozo ya simu na kuongeza fedha kiasi kwa ajili ya mafuta ili ziweze kuja kutatua kero ya Watanzania walio wengi, hasa wenye barabara za vijijini na barabara za mijini. Wakala wa *TARURA* ilipoanzishwa Serikali illianzisha huu wakala tulikuwa hatujakuwa na maandalizi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* ilipoanza haikuwa na fedha iliyotengwa kutoka Hazina, ilitegemea Mfuko Mkuu wa Barabara ambao wao walikuwa wanapewa asilimia 30 na asilimia 70 wanapewa *TANROADS*; na kazi yake kubwa ilikuwa ni kufanya matengenezo ya barabara kwa zile barabara zilizojengwa. Kwa bahati mbaya sana *TARURA* ina kilometra zaidi ya 100,000 ambazo zinahitaji kuhudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa amekuja na pendeleko, na tumeangalia kwenye kitabu chake; Waheshimiwa Wabunge wengi walileta mapendeleko, niombe sasa fedha itakayotokana na ukusanyaji wa hiyo tozo tunaomba uziwekee mfuko maalumu kwa ajili ya kujenga barabara za mijini na vijijini, kuliko ilivyo sasa fedha hizo ambazo mmezitenga hazikuoneshwa kwamba zitalindwa vipi, huo mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kero ya Watanzania walio wengi wanaoishi mijini na vijijini ni barabara. Na Watanzania wakishajua kwamba hizi fedha tunazochangia zinaenda kutatua barabara za mijini na vijijini hata kulalamika hakutakuwepo. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri zitenge hizi fedha ili ziwe na mfuko maalum kama ulivyo Mfuko wa Barabara; itatusaidia sana kuwa na uhakika wa kutengeneza miundombinu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilikuwa napenda kuishauri Serikali ni kwenye sekta ya maliasili. Nchi yoyote ile ambayo ina watalii wengi iliwekeza fedha nyngi za kutangaza utalii. Zipo kampuni nyngi za wakala ya utalii ambazo ziko nje ya nchi. Sasa kwa nchi yetu bado hatujawekeza kwa kiwango kikubwa. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tutenge fedha za kutosha ili tuwezeshe mawakala wa kutangaza vituo vya utalii nje ya nchi. Hii itatusaidia sana kuwa na idadi kubwa ya watalii kuliko ilivyo sasa. Nchi yetu ina vivutio vingi lakini idadi ya watalii wanaokuja hapa nchini ni wachache sana. Naomba hili tukawekeze kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine, kwenye sekta hiyo ya maliasili, Serikali inapata mapato madogo sana kupitia misitu. Nchi nyngine kwa sasa zinanufaika sana kupitia misitu kuliko ilivyo sisi, tunategemea sana kuvuna misitu na kwenda kuuza magogo. Nikuombe Waziri mwenye dhamana mkishirikiana na Waziri wa Fedha, kipo chanzo ambacho mnawenza mkapata fedha nyngi sana wekeni mikataba na mashirika ya kimataifa kwa ajili ya kuvuna hewa ya ukaa. Eneo hili linatoa fedha nyngi mno. Mkisimamia uvunaji wa hewa ukaa sisi tuna misitu mingi ambayo inaweza ikatoa fedha itawanufaisha wanavijiji wanaolinda hiyo misitu, itanufaisha halmashauri na itanufaisha Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano, kwenye halmashauri yangu tumejipanga. Halmashauri ya Tanganyika miaka ijayo tunaweza tusitegemee kabisa Serikali Kuu kwa sababu tunaweza tukapata mapato kwa mwaka kati ya bilioni 30 kwa ajili ya utunzaji wa misitu. Sasa eneo hili

halijafanyiwa kazi kwa kina. Serikali imejielekeza zaidi kuvuna ile misitu, na mahala ambapo panavunwa misitu huwezi ukalipwa fedha kwa ajili ya hewa ya ukaa na mashirika ya kimataifa. Naomba hili mkae mliangalie kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaishauri Serikali ni kuwekeza kwenye teknolojia, hasa za mawasiliano. Ninaamini Serikali ikiwekeza hapo tunaweza tukapata ajira kwa vijana na tukapata mafundi vijana ambao watakuja kufanya shughuli nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika atafatiwa na Mheshimiwa Bahati Hamis Kombo, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii, ambayo ni bajeti ya kwanza ya awamu ya sita na vilevile ni bajeti ya kwanza katika mpango wa miaka mitano, wa 2021/2022 kwenda mpaka 2025/2026 ambayo dhima yake ni uchumi wa viwanda shindani na shirkishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linanigusa sana na nimeliongelea sana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake pamoja na Naibu Waziri na timu yake kwa kutupa bajeti hii ambayo kwa kweli imegusa mioyo ya Watanzania. Sisi Wabunge ni mashahidi, mengi yaliyosemwa katika bajeti hii ni yale ambayo sisi kama Wabunge tuliomba Serikali iyashughulikie. Kwa hiyo tunamshukuru sana, na kwa vile hii ni Bajeti ya Taifa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais jemedari wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa ndiye chachu kubwa ya bajeti hii, tunamshukuru sana. Mimi kibinafsii namshukuru kwanza kwa sababu ndani ya bajeti hii tunaona

dhamira ya dhati ya kuishirikisha sekta binafsi katika kuendesha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupende tusipende sekta binafsi ndio sekta ambayo tunaitegemea kwa kupata mapato makubwa ya nchi. Lakini si hilo tu, ndani ya bajeti hii tunaona wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Rais anatoa maono ya wazi na miongozo ya kuonesha kwamba miradi mbalimbali ambayo ilikuwa ni ya sekta binafsi ambayo imekwamba sasa ipate ufumbuzi na iweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwa kifupi kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kiukweli kabisa kwa kutoa muongozo kuhusiana na mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mradi huu umeongeleta kwa muda mrefu sana, na ulifikia mahali ukawa kama ni wimbo tu; unaimbwa unaisha. Lakini sasa tunaona dhamira ya dhati kabisa ya Mheshimiwa Rais, kwamba majadiliano yale ambayo yalikuwa yamekwama yaweza kuendelea na kukamilishwa; na kama hayawezekani basi tutafute *alternative* nytingine. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee sekta ya kilimo. Sekta hii ya kilimo wote tunafahamu kuwa ni sekta ambayo imetoa mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa nchi; asilimia 26 ya Pato Ghafi la Taifa linatokana na sekta hii ya kilimo. Asilimia 65 ya waajiriwa ambao wanatoka katika maeneo ya vijiji Watanzania wanatoka katika sekta hii ya kilimo. Lakini siyo hilo tu mchango wa sekta hii kwa upande wa kuleta pesa ya kigeni ni takriban asilimia 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza ni kwamba sekta hii inatia huruma. Kwa sababu pamoja na hizo namba tunazoziongea hapa uwekezaji kwenye sekta hii bado ni mdogo sana, na wengi wameliongea hilo. Tunaongelea chini ya asilimia 0.8 wengine wanasema asilimia 0.9 lakini ukweli ni kwamba ni mdogo mno; na udogo wa uwekezaji huo si kwa Serikali peke yake kupitia bajeti bali hata kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki zetu bado hazijachangamkia fursa kubwa ambazo zipo katika sekta hii kubwa ya kilimo. Ukiangalia mgawanyo wa fedha ambazo zimekwenda kwenye sekta binafsi kwa ajili ya kilimo inasikitisha kuona kwamba takriban asilimia 35.8 ya mikopo ya benki imekwenda kwenye mambo binafsi tu ya watu. Asilimia 15.7 imekwenda kwenye biashara za kawaida, asilimia 10 kwenye viwanda, lakini kilimo ni asilimia nane tu. Kwa hiyo tuna tatizo kubwa la uwekezaji kwenye sekta hii upande wa Serikali kupitia bajeti lakini vile vile kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa wote tuna kazi ya kufanya hapa, lakini la kwanza kabisa tuanze na maamuzi ya kibajeti. Naelewa hakuna kitu tunachoweza tukakifanya katika bajeti hii kwa sasa, lakini tunaiomba sana Serikali na tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri, wote tutambue kwamba lazima tuitendee haki Tanzania; na huwezi kuitendea haki Tanzania kama hautatoa pesa za kutosha kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka mitatu minne iliyopita sekta hii uwekezaji wake umeteremka. Lakini huko nyuma angalau tulifilia asilimia tano ya *total collection*. Lakini tukiweza angalau tukafika angalau tufikie hata asilimia sita, tukiweza kufikia asilimia saba ambayo ndiyo *declaration* ya Maputo nadhani tutakuwa tayari tunaenda katika mlolongo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitoe ushauri; tunahitaji kuvutia uwekezaji kwa namna ya pekee kwenye sekta hii ya kilimo, na ninavyoona tunahitaji kuwa na *special scheme* za sekta ya kilimo pamoja na vivutio katika sekta hii. Tunajua sekta hii iko katika maeneo ya vijijini huko mikoani. Wengine walisema na mimi nalisisitiza, kwamba iko haja ya kuwa na vivutio vya kikodi na vya kisera ambavyo vita-focus kwenye sekta ya kilimo na kwenye viwanda ambavyo vitakua na vitajengwa katika maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaloliona sasa hivi kiwanda kinachojengwa eneo la kilimo mikoani na kinachojengwa mikoa ambayo haina kilimo vinakuwa *treated* sawa; hatuwezi kufika katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi kuweka vivutio vya aina fulani katika bajeti hii kwa upande wa *cold rooms* na vifungashio. Lakini mimi nasema kwamba, pamoja na hilo tunawashukuru lakini bado tutatakiwa tuangalie wapi hasa panahitaji kuwekewa hivyo vivutio. Tuangalie mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo. Mimi nasema, vifungashio sawa, *cold rooms* sawa, lakini twende tukaangalie pale ambapo kunafanyika uzalishaji wa mazao yetu ya kilimo ndipo hasa tuweke hivyo vivutio. Tuangalie maeneo ambayo kama kuna viwanda vya madawa, tuangalie viwanda vya mbolea, tuangalie vilevile pale ambapo tunahitaji utaalami na utaalamu hatuwezi kuupata hapa basi tulegeze masharti ya vibali kwa watu ambao watakwendwa kufanya kazi kama wataalamu kwenye sekta ya kilimo. Tunahitaji kufanya kazi kimkakati ili tuweze kuifunua hii sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu zao la *avocado*, kwa kifupi tu. Nchi hii ina uwezo mkubwa sana wa kuongeza mapato makubwa sana kama tukiweza ku-focus kwenye zao la *avocado*. Zao hili linaweza kui-transform Tanzania. Ukichukua nchi kama ya Mexico ambayo eneo lake ni dogo, hata ukubwa wa mkoa wa Njombe Mexico ni ndogo lakini kwa mwaka 2018/2019 Mexico kwa *avocado* peke yake wameingiza *2.7 billion dollars*. Hayo ni mapato yanayofikia mapato yetu yote ya dhahabu. Kwa hiyo iko haja ya kuliangalia hili jambo kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa sasa watafiti wanasema katika miaka mitano ijayo Tanzania inaweza ikawa nchi ya uzalishaji mkubwa wa *avocado* kuliko hata Kenya. Lakini tuna kilio hapa ndani, kwamba *avocado* zetu sisi tunazi-*register* kama zinatoka Kenya, na kwa hiyo kuna upotevu wa mapato, lakini vilevile nchi yetu inakosa fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tatizo hilli litaendelea kama tusipoweka mikakati mahiri sasa hivi. Ukiangalia kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam ambayo ndiyo *port of exit* kubwa tunayoitegemea uwekezaji unaoendelea ni mkubwa lakini bado hauja *focus* kwenye *perishables*. Nchi hii inategemewa kuwa *projected* kuzalisha takriban laki sita za *avocado*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukilinganisha na Mombasa watu wanakwenda Mombasa kwa sababu *slot* za *cold rooms* Mombasa ziko 1800, unakwenda na *container* una *slot* unangojea meli Tanzania *TICTS* Pamoja na *TPA* zipo 120. Kwa hiyo hakuna uwezo wowote utakaotufanya sisi tuende kwenye huo ushindani na tukashinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuongea kidogo sekta ya Madini, ukiangalia utakuta kwamba tumelegalega na nchi yetu kwa kiasi kikubwa sana sekta ya utalii ime-*collapse*, lakini sekta ya Madini imeweza ku-*balance* na imenyanyua kwa kufanya shilingi yetu i-*stabilize* kwa sababu ya dhahabu. Tunamshukuru Mungu kwamba tunaiyo dhahabu, lakini kwa kiasi kikubwa dhahabu yote hiyo imetoka kwenye migodi kama miwili pamoja na wachimbaji wadogo wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba, tunatakiwa tuendelee kuvuta wawekezaji kwenye Sekta hii ya Madini ili tuweze kupata mapato makubwa. Pia tunatakiwa tu-*identify*, twende kwenye sekta nyingine au *sub-sector* nyingine ambazo ndiyo sasa hivi dunia inakwenda na huko tuna wawekezaji kuna maeneo kama ya *helium gas*, kuna maeneo kama ya *rare earth*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya tayari tuna wawekezaji, lakini wawekezaji hawa wanagombea mitaji na nchi nyingine na kama hatutafanya maamuzi haraka ina maana hiyo *opportunity* haitakuwepo na hatutaweza kukua na kupata mapato makubwa ambayo kama tungekuwa na migodi kila mahali inafanya kazi, kila mahali inazalisha, tungekuwa na uchumi mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, mambo mengi yamefanyika ya kikodi hapa ambayo yanataka kusimua uchumi, lakini tukiwa na utendaji na uzalishaji na migodi na huku wewe unalima uchumi huu siyo kwamba utasisimuka lakini utazimuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, ajiandae.

MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia kutupa uhai na uzima na tukaweza kufika hapa tukiwa katika hali ya salama na amani kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa ni Rais wetu na akiwa ni mwanamama. Niseme tu mwanamama huyu ni hodari mno na ni shujaa. Tunamuombea dua Mwenyezi Mungu amjalie azidi kuimarika zaidi. Mama yetu koleza majani ya chai na kazi iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee moja kwa moja katika bajeti yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Fedha kwa kutuletea bajeti hii ambayo imewagusa Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika upande wa *TASAF*, naipongeza Serikali yetu kwa kutenga tena bajeti ya kutuletea miradi hii ya *TASAF*. Kwa kweli miradi hii imesaidia sana kaya zetu maskini na tuna imani kwamba kwa bajeti hii itazidi kuimarika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa upande wa Zanzibar, ripoti imeonyesha kwamba Zanzibar imefanya vizuri. Naipongeza sana Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya vizuri katika kusimamia miradi hii ya TASAF, lakini pia pongezi zaidi ziende kwa wasimamizi wakuu walioweza kusimamia TASAF Zanzibar na tukaweza kufikia lengo kuu lilokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika mchango wangu wangu wa pilii kwa upande wa Jeshi letu la Polisi. Mheshimiwa Waziri hapa amegusia changamoto ya Jeshi la Polisi. Nimwambie tu Mheshimiwa Waziri waende wakaitatue changamoto hii kwani Jeshi letu la Polisi linafanya kazi nyingi usiku na mchana bila kujali mvua au juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha acae makini anisikilize katika jambo hili moja ambalo naomba kulichangia. Jeshi letu la Polisi, kuna fedha ambazo wanazikosa, hawa wenzetu baadhi yao natoa mfano; mwanajeshi huyu anapokea shilingi 565,000 anatakiwa apewe asilimia 15 ya mshahara wake ikiwa ni posho la pango. La kusikitisha mwanajeshi huyu anatakiwa apewe shilingi 84,750, lakini posho anayopewa ni shilingi 40,545. Mheshimiwa Waziri aende akakae na Waziri mwenzake ili waweze kuitatua changamoto hii Jeshi letu liweze kufanya kazi likiwa na ufanisi mzuri na hii haki yao ya posho waweze kuipata kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu sina la ziada ila nampongeza tena mama yetu Mama Samia, niwaambie Waheshimiwa Wabunge tunapompongeza mama tunamsahau baba, tumpongeze na baba yetu kwani yeye ndiye anayempa maliwazo mazuri na akaweza kutuongoza vizuri. Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati, jamani ametukumbusha jambo la msingi kabisa hapo.

Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, ajiandae.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Serikali. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kufikia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipende kuungana na Wabunge wenzangu hasa akinamama kwa jinsi ambavyo tumeona hizi siku 100 za Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, ambazo zimeonyesha kwamba nyota nzuri huonekana asubuhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alipotuita pale kwenye mkutano sisi akinamama kwa kweli alizungumza maneno ambayo yalitugusa akinamama wote kwa ujumla na pia Bunge waliona upweke walivyoona akinamama hatupo Bungeni. Kwa hiyo akajua kwamba akinamama ni watu muhimu katika jamii yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee mambo ya *TARURA*, kuongeza ile Sh.100 kwenye kila lita ya mafuta ni jambo nzuri, lakini kama fedha hii haitakuwa *ring fenced*, kama fedha hii haitatumika *specifically* kwa ajili ya kutengeneza barabara za vijijini na mijini iliyoko *under TARURA*, dhambi hii haitamwacha salama Waziri Mwigulu Nchomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua ni wazi kwamba kuongeza Sh.100 kwenye kila lita la mafuta itaongeza gharama za vitu mbalimbali ikiwepo usafiri wa malori ambayo yanabeba bidhaa mbalimbali kupeleka vijijini. Kwa hiyo, kama wananchi hawataona kwamba kweli zile barabara zimetengenezwa, watajua kwamba hapa Serikali ilikuwa inataka kuwatumia kwa kuwadanganya ili na sisi Wabunge *tui-support* hii *measure* iliyochukuliwa, halafu sijui hii lawama

kama haitafanya kazi ile fedha hiyo iliyotegemewa, Bunge hili tutaficha wapi sura zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nina wazo moja tu au nina weza kutoa maoni kidogo. *TARURA* wamekuwa hata vijijini wakitumia *contractors* au wakandarasi. Hawa wakandarasi wanakuja kutengeneza barabara hizi wakati wa kiangazi ambayo kwa kweli tunategemea iwe hivyo, lakini wanachofanya yale *magraderwanapitisha* mara moja, mtu ukipita unaona barabara inatengenezwa, baada ya miezi miwili mvua ikinyesha, barabara hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaotoka sehemu za milimani tumeona pesa nydingi zimetumika sana kwa *TARURA*, lakini mifereji haitengenezwi, zile sehemu korofi hazitengenezwi imara, matokeo yake baada ya muda mfupi tu mvua ikinyesha mara moja, mara mbili barabara hazipitiki, mabasi hayaendi, malori hayaendi, balaa kubwa kwa wananchi wakati fedha za mlipakodi zimetumika kwa ujanja, ujanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nishauri kwamba wakati nafanya *internship* kule ILO - Geneva nakumbuka kwamba kazi kubwa ambayo *ILO* alikuwa anasisitiza ni *labour intensive, activities* hizi zitumie *labourzaidi* kuliko *equipment* na kwamba *equipment* itumike pale ambapo panaonekana kuna hali ngumu ambayo haitaweza kutumia wananchi. Kwa mfano, wakati huko nyuma tulikuwa tunaona kwamba kulikuwa na hizi zinaitwa *PWD – Public Works Departments* vimewekwa vibanda kila sehemu za barabara zetu na wale wafanyakazi walikuwa wanapewa vifaa kwamba wao wana-*monitor*, wakiona kuna sehemu ina shida wana-*repair* mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashauri, Serikali yetu hii izungumze na *TARURA* wajiongeze, wafundishe wanavijiji wetu, vijana wetu, kule kwenye vijiji, kwenye kata jinsi ya *ku-repair* kufanya *periodical maintenance* ya hizi barabara, wawape vifaa kama machepeo, *wheelbarrows*, mafyekeo,

ambavyo wao baada ya *contractorkuondoka* wataendelea na ile *maintenance* ya zile barabara ili ziwe *sustainable*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kutumia ile kama wanavyotumia *force account*, kuwe na posho ya kuwalipa hawa vijana, kwanza wata-create *employment*; pili watahakikisha kwamba zile barabara zinapitika *throughout the year*. Halmashauri zetu kwa mfano halmashauri ya Wilaya ya Same hatuna hata *grader*, hatuna hata *equipment*, ukichukua *graderla* kutoka Moshi kupeleka kwenye vijiji vyetu unaambiwa ulipe kwanza milioni tatu la kuliondolea pale na kila siku unalipa laki tisa. Sasa hapo kwa fedha hizi ambazo naamini ni nyingi, naamini Serikali ikiwa na nia njema itaweba kusaidia Halmashauri zikapata hizi *equipment*, zikaongeza ma-engineer wa *TARURA* ambaao wataweza ku-monitor hizi *activities* ambazo zinafanywa na vijana wetu ambaao tutaweka hizi *building brigades* au *road brigades*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo nataka nizungumzie pia vikundi vya ujasiriamali, ile *ten percent* inayotengwa kwenye halmashauri. *Experience imenionyesha* kwamba akinamama licha ya jinsi ambavyo Rais wetu alizungumzia kuhusu hela ndogo inayotolewa kwenye hivi vikundi, lakini *once wakishapewa* zile fedha mgogoro unaanza pale, vikundi vinasambaratika, wanagawana zile fedha na kazi haifanyiki ile iliyotarajija. Fedha hizi zilikuwa zinatengwa ili ziwe *revolving fund*, ili ziwe zinarudishwa wengine wanapewa, lakini haionyeshi popote pale kwamba hizi fedha zimekuwa zikirudi na vikundi vingine kupewa fedha hizo hizo imekuwa kila mwaka Serikali inatoa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashauri kwamba fedha hizi badala ya kutolewa *cash*, kuna Maafisa Maendeleo ya Jamii, kwa nini wasitumie hizi fedha kununua *equipment* wakawapa vile vikundi, maana wao ndio wana-mobilize vile vikundi, wakawapa na kuwasimamia kuhakikisha wanafanya ile kazi waliyoitarajia. Kwa hiyo ningeomba kwamba Serikali iliangularie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia, napendekeza *TRA* fedha inayotengewa iwe ya kutosha ili iweze kuajiri wafanyakazi watakaoweza kukusanya kodi. Pia *CAG* nashauri kwamba apewe hela za kutosha, apewe ruhusa *I do know you call it ruhusa* ya kuajiri wafanyakazi, because ameongezewa kazi ya ku-audit miradi zaidi kwa ajili ya kuona kwamba fedha za umma zinatumika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka *CAG* kama alivyosema afanye *-real time auditing* aweze ku-*curb problems* za kupotea kwa fedha kabla hazijawa zimetumika vibaya, halafu ndiyo aje kukagua. Kwa hiyo tungesema kwamba *CAG* akipewa hizi fedha mapema anaweza kufatilia jinsi ambavyo bajeti hii itatumika. Tumeona huko nyuma kwa mfano kuna Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori ambao ulipata bilioni nne kwa ajili ya kufanya usanifu wa jingo. Tangu wamefanya usanifu huo ni miaka minane sasa lile jengo halijajengwa ambalo ni la Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori, bilioni nne zimepotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ndege ambayo imetengenezwa zimetumika karibu bilioni nne, lakini hiyo ndege haijawahi kunyanyuka chini, ni mbovu siku zote. Sasa tunachosema ni kwamba, laiti *CAG* angekuwa na fedha za kutosha akaajiri wafanyakazi wa kutosha, akawa anafanya *real time auditing* angeweza ku-*curb* hizi *proliferation* ya hizi fedha zinazopotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia nchi yetu iunde *think tank* la watu wenyewe busara, wenyewe hekima wa uchumi, wenyewe kujua mambo ya uchumi, ambao wanaweza kuishauri Serikali yetu jinsi ya kuweza kufanya ufuatiliaji wa yale ambayo yanawekwa kwenye bajeti na jinsi ambavyo fedha inatumika ili kusudi isiwe tunapanga hiki na kinachofanyika ni kingine. Naamini kwamba hii pia itafanya mambo ya *monitoring* na *evaluation* ili tujue kwamba kweli fedha ya umma inatumika jinsi ilivyopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika bajeti hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu anayetujalia uhai na anayezidi kulinda Taifa letu na ustawi wa wananchi wake. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya, nimshukuru sana Makamu wa Rais, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri wanazofanya. Hii imetuletea bajeti nzuri, bajeti ambayo imegusa kila eneo, kila kundi kwa kweli ni bajeti ambayo inaenda kuinua hali za Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu ujikite katika kilimo; kwa vile asilimia 65 ya Watanzania wanajihusisha na kilimo, lakini pia vijana wetu ambao hawana ajira wanaweza wakajiunga na kilimo. Vile vile Bunge lako Tukufu hili Bunge la Kumi na Mbili limebainisha kwamba linaenda kujikita zaidi katika kufanya mageuzi makubwa katika sekta hii ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika bajeti ukurasa wa tano, ukurasa wa 16 na wa 17 namna ambavyo Serikali inaenda kuboresha kilimo, namna Serikali inavyoenda kuleta tija na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, nilitarajia kuona kwamba Serikali inaweka fedha nydingi kama mtaji kuinua hii sekta; kwanza kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, lakini pili, kwa kutafuta masoko na kuboresha ya ndani na nje na kikanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kabla ya kuanza mtaji huu naona kuna tozo mbalimbali zimewekwa pale. Kwa mfano katika ukurasa wa 33 kuna tozo ya zuio, sasa pale imefafanuliwa vizuri kwamba tozo hii inaenda kutozwa kwa NFRA kama Wakala wa Ununuzi, lakini bahati mbaya

kinachotokea kule ni tofauti kabisa, ni wakulima ndio wanaotozwa tozo hii. Wakulima wale hawajafafanuliwa vizuri, tozo hii inatozwa wakati gani kwa sababu kuna ushuru wa halmashauri na wakulima wanatozwa njiani wanavyotoka shambani wakati wanarudisha mazao nyumbani, wanatozwa barabarani, lakini pia wakulima wanatozwa wanapopeleka gulioni wanatozwa mara ya pili na tatu wengine wanatozwa pale wanapouza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri aje na ufanuzi, kwamba muda sahihi wa kumtoza mkulima hasa mdogo ni wakati gani? Anaposafirisha au anapouza? Ni wakati gani atozwe na kwa kiasi gani? Tumeona nyuma huko, ilikuwa kawaida ni kwamba anayebeba chini ya tani moja hatozwi chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukurasa wa 33 imebainishwa kabisa, hii haitahusu wakulima wadogo wadogo magulioni, itahusu tu wakala wa ununuzi, lakini kinachotokea kule ni tofauti kabisa; wale wazabuni wanaotakiwa watoze njiani, hata wakiona gunia chini ya tani moja, wanatoza. Wanatoa visingizio mbalimbali; watasema umeweka mfuko haufai siyo wenyewe, watasema sijui sasa hivi tunatoza tu kwa vile umechelewa kurudi toka shambani, ili mradi wao wapate kodi kubwa. Wanapiga hesabu ya kutosha kupeleka Halmashauri na nyingine ibaki kwa ajili yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tungependa ufanuzi, tujuue hali halisi, inatakiwa itozwe kwa nani? Kama ni mkulima, basi ni wakati gani? Je, ni pale anapofanya biashara au wakati gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, changamoto nyingine kwa wakulima hawa ni mbolea. Mbolea ina ruzuku lakini kwa kweli ruzuku ile inafika mahali haiwezekani, bado ni bei kubwa sana. Nitoe mfano, mwaka jana 2020, Jimbo la Mbalali mbolea aina ya CAN imeadimika kabisa. Huwa bei ya kawaida uwa ni shilingi 45,000/=, imepanda mpaka shilingi 55,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kwa wakulima ni skimu zile. Kwa kweli skimu zilizo nyingi zina hali mbaya sana. Kwa hiyo, wakulima wanakosa pato kwa sababu skimu zile hazijakarabatiwa kwa muda mrefu. Kule Mbarali kuna skimu moja inaitwa Mwendamtitu, imekuwa ikijaa mchanga mara kwa mara. Halmashauri kupitia mapato ya ndani imejaribu kuzibua, imeshindikana na wale wameomba mkopo kutoka *TAB Bank* mpaka sasa hivi hawajapata mkopo wowote na baadhi yao hawajavuna kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni mtaji. Wakulima wadogo wale hawana mtaji wa kutosha. Mtaji kwa maana ya kwamba wanaenda benki wanaahidiwa kukopeshwa, lakini ukifika msimu kwamba wanaenda shambani, benki hawatoi mikopo kwa wakati na pengine hawatoi kabisa. Wamekuwa wakinilalamikia. Mwenyewe nimeenda benki kuulizia, mbona hamuwapi wakulima hawa mikopo na msimu unapita? Wananijibu kwamba mtandao haupatikani, waombaji ni wengi, tunaendelea kuchambua, tutawapa tutakapoona majina yao, lakini muda unazidi kwenda, wengi wamekosa mikopo, wachache wamebahatika kukopa na wengine wameenda kukopa kwa watu binafsi, kitu ambacho ni gharama kubwa, kwani riba ni kubwa mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wamehangai, wamepata mikopo, wamepata shida zote hizo, lakini masoko hakuna. Wamevuna mipunga, imejaa ndani na soko hakuna. Kwa mwaka uliopita Mbarali tumevuna tani 275,000 uzalishaji, lakini mahitaji yetu ni tani 125,000 tu. Kwa hiyo, tuna ziada ya tani 150,000; na hizo tani zimekutana na mavuno ya mwaka huu. Kwa hiyo, wamekopa, hawajauza, wamelipa ushuru, tozo mbalimbali, mpunga umekwama ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nije kwenye suala la masoko ya ndani. Naiomba Serikali iwave *NFRA* fedha nyingi wanunue mazao yote ya wakulima. Njia nyingine katika kuimarisha masoko ya ndani ni kuanzisha

miradi wa Liganga uanze kufanya kazi, watauza mazao yao kule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la Tume ya Umwagiliaji, inafanya kazi kule bila mawasiliano na Halmashauri. Wanaenda *site*, wanaongea na wakulima moja kwa moja; sehemu nyine wanafukuzwa na sehemu nyine kuna miradi ya ajabu kabisa ambayo Halmashauri hajui na mingine iko chini ya kiwango. Kwa mfano, tuna bwawa moja Rwanyo pale Igurusi la miaka mingi halifai na ni hatari kwa wananchi pale. Tuliomba Chuo Kikuu Mzumbe waje kutathmini namna ya kurekebisha, wakasema gharama ya marekebisho itazidi gharama hata ya ujenzi. Sasa fedha ya Serikali ndiyo imeisha hiyo, ni hasara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba, ili tuwe na usimamizi mzuri kwa Wilaya ya Mbarali, kwa kweli jimbo lile ni kubwa mno, tunaomba ligawike yawe majimbo mawili au Halmashauri mbili, kwa sababu inapitia mikoa mitatu; imeanzia Mbeya, Njombe, hadi Iringa; na ukiwa katikati pale kwenda upande wa mashariki ni kilomita 97, kwenda magharibi ni 134, jumla ni urefu wa kilomita 231. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtaalam kwenda kufanya *supervision*, akienda anarudi usiku kabisa na inhabidi anywe *Panadol* ndiyo alale usingizi na akirudia analazwa. Sasa kwa kweli tuna hali ngumu sana. Kuna miradi mikubwa na mizuri ya ujenzi wa madarasa; mnaenda kule mnaambiwa *cement* tulimwazima Mwenyekiti wa Kijiji, tuliona itaganda. Mbao, kiongozi fulani tuliona azitumie, fedha hatuna. Kwa kuwa ni mbali mno, tunaomba sana igawanywe iwe Halmashauri mbili na ikiwezekana na Mji wa Lujewa iwe mamlaka kamili.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. FRANCIS L. MTEGA Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nami kuweza kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi ambaye amenijalia pumzi na wakati huu nikaweza kusimama hapa kuelezea mchango wangu juu ya bajeti yetu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na walionitangulia kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na wasaidizi wake wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri kwa namna ambavyo wameanza kutelekeza majukumu/kazi yao na kuwajengea matumaini zaidi Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake Mheshimiwa Masauni pamoja na Watendaji wa Wizara ya Fedha kwa kuandaan pamoja na kutuwasilishia bajeti hii ambayo leo tuko hapa katika kuijadili; bajeti iliyooja matumaini na bajeti iliyobeba dhamira ya kuwaendeleza Watanzania. Hii ni ishara njema ya namna ambavyo Serikali yetu ya Awamu ya Sita inavyokwenda kutatua shida za wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa suala zima la uimarishaji wa elimu. Nichukue nafasi hii pia kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa namna ilivyojipanga katika suala zima la kuimarisha elimu Tanzania

kwa kujenga Shule za Sekondari nyingi, Shule za Msingi pamoja na kukarabati shule za zamani na isitoshe kuajiri walimu wengi kwa lengo la kuimarisha elimu na kuona watoto wetu wanapata elimu iliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili zaidi nitazungumzia wanafunzi wenyе ulemavu. Nachukua nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa namna walivyojali wanafunzi wenyе ulemavu na wakaweza kuwajengea mazingira mazuri. Ukiangalia uhitimу wa wanafunzi wenyе ulemavu kipindi cha nyuma na sasa hivi ni tofauti. Kwa sasa kila mwaka ufaulu wa wanafunzi wenyе ulemavu umekuwa ukiongezeka kwenda sekondari na hata vyuo, na wewe mwenyewe nadhani utakuwa shahidi. Hii yote inatokana na juhudи za Serikali kusomesha walimu wa kutosha ambaо wanasomea kuwafundisha watoto wenyе mahitaji maalum. Pia hii inatokana na jitihada za walimu hawa. Bila ya jitihada hii, hawa wanafunzi wasingeefika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kuangalia walimu wanaofundisha wanafunzi wenyе ulemavu kwa sababu walimu hawa wana kazi kubwa. Kumfundisha mwanafunzi mwenyе ulemavu ni tofauti na kumfundisha mwanafunzi wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu anayefundisha mwanafunzi mwenyе ulemavu anatumia masaa mengi zaidi. Kwa hiyo, tunahitaji kuwajengea uwezo lakini pia kuwapa motisha ili waweze kuwasaidia watoto wetu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo sasa, nataka kuzungumzia suala la tozo. Naunga mkono mapendekezo ya Waziri kuhusu kufanyia marekebishо Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara kwenda Zanzibar na zinazonunuliwa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara. Napongeza marekebishо haya kwa sababu yatakwendа kuondoa kero ya muda mrefu ambayo ilikuwa ikilalamikiwa na wafanyabiashara. Siyo tu kwa wafanyabiashara, hata kwa wananchi wa kawaida ambaо walikuwa wakinunua bidhaa zao kutoka upande

mmoja wa Muungano kwenda upande wa pili wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, suala hilo pia litaondoa zile hoja kwa wale wasioutakia mema Muungano wetu waliokuwa wakilitumia sana suala hili. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa tunatengeneza sheria nyingi na nzuri na pale ambapo tunahisi zinahitaji marekebisho tunafanya hivyo, lakini tunatengeneza sheria, tunafanya marekebisho, lakini shida inakuja katika utekelezaji wa sheria kutokana na baadhi ya Watendaji wetu kutokuwa na uaminifu na hii usababisha mambo yasiende kama yalivyopangwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika hilli, namwomba Mheshimiwa Waziri baada ya kufanya marekebisho haya, awe mfuatiliaji mzuri na timu yake hili kuona malengo ya Serikali yameweza kufikiwa. Pamoja na hayo, pia namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, atupe ufanuzi wa kina juu ya tozo hizi: Je, sitatusika mpaka kusafirisha magari? Kwa sababu unapotoa gari Zanzibar kule Bara ni shughuli; au unapotoa gari Bara kuleta Zanzibar ni shughuli. Aje atufanulie, tozo hizi ni vipi zitagusa masuala ya magari unapotaka kusafirisha? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine nitajikita katika suala zima la tozo katika kufanya miamala ya matumizi ya simu. Hili suala ni jema sana, Serikali yetu ipo katika kuona inatengeneza mazingira kwa maslahi ya wananchi wake. Kuna miradi mingi imepangwa, kuna shughuli nyingi zimepangwa katekelezwa na zote hizi zinategemea mapato. Kwa hiyo, naunga mkono suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hotuba yake hapa, kumekuwa na uelewa tofauti tofauti na watu wanazungumza maneno tofauti juu ya tozo hizi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja

kufanya majumuisho basi aje atoe ufanuzi wa kina juu ya tozo hizi kwa lengo la kuleta uelewa mzuri kwa wananchi kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika mchango wangu mwininge ambao unazungumzia miradi ya kimkakati inayoibuliwa na Halmashauri zetu. Kuna miradi ambayo huwa inaibuliwa na Halmashauri. Miradi hii inaibuliwa lakini kuna vigezo maalum. Kigezo cha kwanza, Halmashauri iwe na uwezo wa kuongeza mapato, iwe na uwezo na mpango wa kujitegemea na pia iwe na uwezo wa kuandika andiko la mradi. Hata hivyo, kuna Halmashauri zetu nyingine tunaona hazitaweza kukidhi hivi vigezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetunga sheria ya kuzitaka Halmashauri kuchangia asilimia 10 ya mapato yake. Tumeona katika ripoti, inaeleza kwamba kuna Halmashauri zimetimiza asilimia 100, kuna Halmashauri asilimia 30, na nyingine asilimia 50. Hata hivyo, kuna Halmashauri zimewezesha vikundi vingi, lakini kuna Halmashauri zimewezesha vikundi kidogo. Hii inatokana na uwezo wa Halmashauri zenyewe.

Kwa hiyo, kutokana na vigezo hivi, nahisi bado hazijatendewa haki zile Halmashauri zenyе uwezo mdogo; na lengo letu ni kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato na kuhudumia wananchi pamoja na kuleta maendeleo katika Halmashauri zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba sana iundwe timu ya wataalam iende kwenye Halmashauri, tuziangalie Halmashauri ambazo hazina uwezo, zijengewe uwezo hili waweze kuzitambua fursa zinazowazunguka ili nao waingie katika ushindani wa makusanyo. Kwa hiyo, Halmashauri hizi nazo zitaongeza uwezo wake na wataweza kutimiza matakwa ya sheria ya kukamilisha kwa asilimia 100 yale makusanyo ya asilimia 10 ya Halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makof/Vigelegele*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja hii. Nampongeza Rais wetu kwa bajeti hii nzuri, pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye kushauri. Nilikuwa naangalia hizi sekta zetu za kiuchumi na mchango wake katika pato la Taifa. Ukipititia zote, kwa kweli bado tunayo kazi kubwa ya kufanya. Ukiangalia kilimo kinachangia asilimia 26.9 kama takwimu zangu ziko sahihi; fedha na bima zinachangia asilimia 3.5; madini asilimia 6.9; viwanda asilimia 8.4; umeme asilimia 0.3; ujenzi asilimia 14.4; uchukuzi asilimia 7.5; na blashara asilimia 8.7. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia jiografia ya nchi yetu, mimi nadhani sekta nyingi kwa kweli tuko chini pasipo sababu yoyote ya msingi. Kwa mfano uchukuzi, kwa jiografia ya nchi yetu, bandari zetu, nchi tunazopakana nazo, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri, tujipe mkakati wa kukatisha baadhi ya sekta mchango wake katika pato la Taifa uende zaidi ya asilimia 10. Tupende tusipende lazima tuwe na mkakati wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya uchukuzi tuna viwanja vyetu vya ndege, lakini kanda ya ziwa tuna uwanja wa ndege wa Mwanza. Zamani mazao ya uvuvi yalikuwa yanasafirishwa kwa ndege kutoka uwanja wa ndege wa Mwanza kwenda nchi za nje, lakini hivi sasa tunavyoongea, mazao yote ya uvuvi ili yaende kwenye masoko ya nje, lazima tuyasafirishe kwa malori tuyapeleke Entebbe au Nairobi. Ukijuliza, kwa nini mazao yetu ya uvuvi yaende Entebbe au Nairobi? Hatuna sababu yoyote ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani uwanja wetu wa ndege haukuwa na *facility* ya kuhifadhi hii minofu ya Samaki, lakini hivi tunavyoongea, Serikali yetu kupitia *TAA* wamejenga

facility nzuri sana ambayo ukilinganisha na nchi jirani *actually facility* tuliyonayo pale Mwanza ni nzuri na bora kuliko *facility* zote za Afrika Mashariki na Afrika ya Katì. Tatizo tulilonalo, hatujaisajili kupata *FOB* Mwanza na ndio maana mashirika ya ndege kama *Air Rwanda* walipojaribu kusafirisha minofu yetu ya samaki kutoka Mwanza, wameshindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, kwa kuwa tumeshawekeza pesa yetu pale Mwanza, tumejenga *facility*, tutafute *registration*, tupate *FOB* Mwanza ili mazao yetu ya uvuvi yasafirishwe moja kwa moja kutoka Mwanza kwenda nchi za nje. Hii kwanza itaongeza chachu kubwa ya kuwekeza viwanda hapo Mwanza au Kanda ya Ziwa. Pili, zile pesa ambazo tunazilipa Entebbe na Nairobi zitabaki kwenye nchi yetu, tutaongeza pato kwa sekta ya uchukuzi na sekta ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu kilimo. Ukiangalia sekta ya kilimo, mchango wake ni mdogo. Wachangiaji wengi wamesema hapa, tuna vijana wengi huko mitaani hawana kazi, lakini hawawezi kwenda kwenye kilimo kwa sababu ukiwaambia wanasesma hawana mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu kitengo cha *JKT* wanafanya vizuri sana kwenye kilimo. Nashauri tuwaongezee pesa wakajikite kwenye kuzalisha mazao ya kilimo. Kwa sababu wana uwezo, watalisha, watayaongezea thamani na wanawenza kupata masoko kirahisi kuliko mkulima mmoja mmoja. Hata kilimo ambacho tunakizalisha, hapa tunaongea lakini nadhani hatuna mkakati wa madhubuti kuhakikisha kwamba tunaongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Kagera tunazalisha kahawa. Tumejiga kelele sana hapa, tumejema hebu ruhusuni wafanyabiashara wakanunue hizi kahawa. Kuna watu wamewekeza kwenye viwanda pale, lakini tunawewekea figisufigisu hatuwapatii vibali. Msimu wa kahawa ulianza mwezi wa Nne, lakini tunavyoongea leo, vyama vyetu vya msingi havijafungua masoko, hata

wafanyabiashara binafsi ambao wangenunua kahawa, hawajapewa vibali. Ukiijuliza wakati mwingine, tunadhamiria nini? Tunalenga kufanya nini? Ndiyo maana sekta nydingi kama hizi kutokana na kanuni zetu tulizojiwekea, hatufanyi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwamba hizi posho ambazo walikuwa wanalipwa Madiwani sasa Serikali inazibeba. Hata hivyo nikiangalia hizi posho zao hawa Madiwani wenzetu, pamoja na kwamba naishukuru Serikali kwamba imezibeba, itazilipa kwa wakati, lakini tuziangalie hizo posho, bado ni kidogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Madiwani wenzetu ndio tunawaachia majimbo yetu, ndio wanafanya kazi kwenye kata zetu, ndio wanafanya kazi ya kuhamasisha kukusanya mapato ya Halmashauri zetu. Napendekeza kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, tuiangalie hii posho ya Madiwani, tuwaongezee angalau kidogo nao wakajisikie na wakafurahie kazi wanayoifanya huko kwenye Halmashauri zetu na waweze kutulindia majimbo yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa posho zilizopendekezwa kwa ajili ya Watendaji wa Kata na Maafisa Tarafa. Nawashukuru sana. Hata hivyo, kuna kundi ambalo tumelisahau; kundi la wazee. Nimefurahi kule upande wa pili wa nchi yetu, Zanzibar wanawalipa wazee posho ya shilingi 25,000/= kila mwezi; wanafanya vizuri. Ila kwa upande wa Tanzania Bara tuna makundi ya watu wenye mahitaji maalum; tunaongelea watoto, wanawake na vijana ambao wanapewa mikopo, lakini tumesahau hili kundi muhimu la wazee na ambalo katika maisha yao wamelitumikia Taifa hili na kwa kweli wanaishi kwa kusononeka, baada ya kuingia kwenye hili kundi la wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu na tujuwe kila mmoja wetu tunaelekea kwenye uzee, tuwatengue na wenyewe posho kidogo ambayo itawapatia furaha katika maisha yao. Hii inawezekana. Baadhi ya taasisi

kwa mfano ninakotoka kwenye jimbo langu, kuna *NGO* tu; kuna mzee mmoja Mswisi, ameishi pale zaidi ya miaka 10. Aliamua yeye kwa pesa yake kuwalettea raha wazee wenzake, kila mwezi anatumia zaidi ya shilingi milioni 16 kuwapa posho hawa wazee. Anawalipa posho zaidi ya wazee 1,000; na kwa mwaka anatumia zaidi ya shilingi milioni 195 kwa pesa yake na pesa ambayo anaitafuta nje. Huyu mzee amekaa hapa muda mrefu sana, lakini alijaribu hata kuomba na uraia tukamnyima. Naona Waziri wa Mambo ya Ndani yuko hapa. Huyu mzee amefanya mambo mengi mazuri na anawasaidia wazee na anawapa raha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema kuwalipa posho wazee siyo suala la pesa unawalipa kiasi gani? Kinachofanyika ni kwamba, wanajiona wamethaminika, wanajiona wanapendwa, wanajiona wana thamani katika nchi yao, hata tukiamua tuwepe shilingi 10,000/= tu, watafurahi, wataishi maisha marefu zaidi na watafurahia nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili tuliangalie, tulitafakari na tulitathmini. Sasa hivi wazee tunasema ni wachache lakini tuendako zaidi ya miaka 10 ijayo, wazee tutakuwa wengi, tunazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga hoja mkono, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kikoyo uliposema wazee tutakuwa wengi, nikaona Wabunge kadhaa wamekugeukia, hawajaelewa kama nao watakuwa sehemu ya hilo kundi la wazee. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa michango mbalimbali ambayo mmeitoa, ambayo naamini inamsaidia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Serikali kwa ujumla kuona namna ambavyo wanaweza wakaboresha utekelezaji wa bajeti hii na pengine huko mbele wakaona mambo kadhaa ya kuboresha.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Prof. Patrick Ndakidemi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, lakini wanatoka Jimbo la Moshi Vijijiini. Kwa hiyo wamekuja kumtembelea Mbunge wao na kuona Bunge namna linavyofanya kazi. Karibuni sana vijana kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Naamini katika kundi hili hamna mwenye mpango wa kumtoa Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kule Moshi Vijijiini. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Ijumaa,
Tarehe 18 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*